ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	- SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake

37.Mhe. Ashura Sharif Ali - Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Tano – Tarehe 23 Juni, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Salum Haji (Kny: Mhe. Hamza Hassan Juma) Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea na maswali nashukuru kwamba katika Baraza letu kumekuwa na utamaduni wa kupata wageni mara kwa mara. Moja kwa sababu ya kuja kuona jingo lao. Lakini pili kwa sababu ya umuhimu wa shughuli inayoendelea hivi sasa yaani Mkutano wa Bajeti. Leo pia tumepata wageni ambao wapo pale juu na hawa ni wageni ambao wanahusiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Wageni hawa ni walimu wakuu wa Wilaya ya Mjini wamejikusanya pamoja na kuunda jumuiya yao ya walimu wakuu wa Wilaya ya Mjini, wapo jumla ya walimu wakuu 41wote wa Wilaya ya Mjini.

Nichukue nafasi hii basi Waheshimiwa Wajumbe niwaombe walimu wakuu hawa 41 wasimame ili kusalimiana na Waheshimiwa Wajumbe. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Lakini pia kuna wanafunzi wa skuli ya Lumumba ambao nao wamehamasika leo hii waje ili kuona wazee wao katika Baraza hili wanafanya nini hasa hasa katika bajeti hii ambayo inaendelea. Wanafunzi hao wa skuli ya Lumumba jumla yao ni sita naomba nao wasimame ili kuwasalimu Waheshimiwa Wajumbe. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe hao ndio wageni wetu kwa leo wamekuja ili kujionea wenyewe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakishughulika na masuala ya kitaifa kwa kupitisha Bajeti ya Serikali ambayo imemalizika jana, lakini leo tukiwa tunaendelea na shughuli nyengine baada ya maswali kusikiliza Hotuba ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni. Ahsanteni sana.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 166

Fursa/Haki ya Kutembelea Jengo la Kisiwandui

Mhe. Omar Ali Shehe - Aliuliza:

Historia ya siasa ya nchi yetu pamoja na mambo mengine imeainisha tokeo la kuuawa kwa aliyekuwa Muasisi wa Taifa Sheikh Abeid Amani Karume hapo katika jengo lililokuwa la ASP (jengo la CCM kwa sasa) Kisiwandui.

Kwa kuwa yeye mwenyewe na tokeo la mauaji yake ni sehemu ya historia kwa kizazi cha sasa na cha baadae. Je, serikali inawapa haki au fursa gani waliokuwa wana ASP na Wazanzibar wengine ambao kwa sasa hawako katika itikadi ya CCM kuweza kwenda na kujionea sehemu hiyo ya historia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 166 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba historia ya siasa ya nchi yetu inajumuisha tukio la kuuawa kwa Mwasisi wa Taifa letu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Kutokana na historia hiyo ndio maana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu zake zote imekuwa ikiweka na kuhifadhi kumbukumbu za muasisi wetu na kuifanya tarehe 7 Aprili ya kila mwaka kuwa Siku ya Maadhimisho ya Kitaifa ya Kifo cha Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.

Mhe. Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba upo utaratibu kwa wananchi, viongozi mbali mbali wa ndani na nje na watafiti kutembelea sehemu alipouawa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na kuliona kaburi lake na kupata maelezo sahihi juu ya tukio hilo la kihistoria hapo katika Jengo la CCM Kisiwandui. Hivyo namuomba Mwakilishi na wananchi wanaotaka

kutembelea maeneo hayo waonane na wahusika ambao ni uongozi wa Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui na wataelekezwa juu ya utaratibu unaopaswa kufuatwa.

Mhe. Spika, hadi sasa hakuna vikwazo wala gharama za malipo yoyote yanayotozwa kwa kutembelea maeneo hayo. Naomba kutoa wito kwa wananchi kutembelea eneo hilo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba pale ni jengo la Kisiwandui pamoja na tokeo la mauaji ni sehemu ya historia. Kwa kuwa katika nchi yetu tuna idara inayoweka kumbukumbu za historia na mambo ya kale. Je, Afisi ya CCM Kisiwandui ina mahusiano gani na Idara ya Nyaraka na Mambo ya Kale.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Abeid Amani Karume mzee wetu muasisi wetu licha ya kuwa ni muasisi wa taifa letu na Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 lakini pia alikuwa muasisi wa Chama cha Afro Shirazi. Kwa kuwa wakati huo Chama cha Afro Shirazi ndio kilichokuwa kinaongoza serikali na lile limekuwa jengo lake. Kwa ajili ya kuweka kumbukumbu vizuri na mahali ambapo ameuawa na ndipo hapo hapo amezikwa ndio maana watu wa CCM Kisiwandui wamechukua jukumu hilo la kuliendeleza. Kwa kuwa wamefanya vizuri Mhe. Spika, hatuoni sababu kwa nini wasiendelee kufanya shughuli hiyo. Taarifa zake marehemu muasisi wetu bado zipo Idara ya Kumbukumbu na Mambo ya Kale hivyo nao wakiwa na mahitaji ya aina yoyote kwa ajili ya kuimarisha michoro hiyo wanakwenda pale na hakuna tatizo la aina yoyote.

Mhe. Salehe Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Afro Shirazi, CCM na sisi Wazanzibari wote tunaamini kwamba Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ameuawa na amezikwa, lakini kilichokufa na kuzikwa ni kiwiliwili chake tu, mawazo, fikra, busara na maazimio yake yapo pale pale.

Kwa kuwa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume aliondoka katika nchi hii akifuatia matunda ya mapinduzi kwa maana ya elimu bure, matibabu bure na maji bure.

a) Je, kuendelea kuwachangisha wananchi katika mambo ya elimu, afya na maji si kwenda kinyume na ile hazina aliyotuachia muasisi wetu wa taifa hili.

b) Ni lini serikali ya awamu ya saba itatuwekea hotuba za mwanzo zile za Marehemu Karume zikiwemo zile za Muungano pamoja na *Article of Union* ili tujue vya kuuenzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kama alivyosema sisi sote tunaamini kwamba kilichokufa ni kiwiliwili tu cha Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, lakini mipango, mawazo na fikra zake zipo pale pale na zitaendelezwa milele. Awamu zote za serikali yetu zimechukua jitihada hiyo ya kuendeleza fikra na mipango hiyo. Mpaka hii leo Mhe. Spika, elimu ama afya yale yanayosaidia wananchi katika kuchangia kidogo si kwamba ni mambo ya lazima wananchi wayachangie. Yale yemewekwa kwa utaratibu makusudi wa kusaidia kwa wale wenye uwezo. Wale wananchi ambao hawana uwezo basi Mhe. Spika, serikali zetu zinakubali kusaidia wananchi wetu.

Kwa sababu mpaka hii leo huduma hizi za elimu na afya zinazotolewa hazitolewi kwa malipo yoyote. Kile kinachotolewa ni mchango kidogo kwa wale wenye uwezo ili kusaidia jitihada zetu za kuimarisha elimu na afya nchini.

Kuhusu mikataba mbali mbali ya Muungano ningemshauri Mhe. Mwakilishi aende *Archives* ataiona mikataba hii na mambo yote yapo pale atapata taarifa za kutosha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na kwa mtiririko huo huo nilikuwa naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kila nchi duniani huwa na kiongozi mwenye alama ya utambulisho wa taifa *(symbol of the nation).* Kwa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ndio alama ya utambulisho wa taifa hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, unapotembelea ofisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ujumla kwa miaka mingi tumeachana na utamaduni wa kutundika picha ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na badala yake unaikuta picha ya Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere peke yake kama Muasisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia kumekuwa na kutangazwa kwamba Marehemu Mwalimu Nyerere ndie Baba wa Taifa kama vile kwamba mataifa haya yote mawili yaliyounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yalikuwa yameasisiwa na yeye.

(a) Je, Mhe. Waziri lini atachukua hatua ya kutangaza Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwamba ni Baba wa Taifa la Zanzibar kama ilivyokuwa mwaka 1964.

(b) Ni lini atatoa agizo ili picha za Marehemu Mzee Karume zirejee katika ofisi zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuashiria kwamba huyu ndio alama ya utambulisho wa taifa la Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza ningependa kusema kwamba katika jibu langu la msingi nimeeleza wazi kwamba Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ni Baba wa Taifa. Napenda nirudie Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ni Baba wa Taifa la Zanzibar.

Aidha, nataka nimhakikishie kwamba hatua zitachukuliwa kwa zile wizara ama taasisi za serikali pale ambapo picha ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume haipo kuhakikisha kwamba picha hizo zinakuwepo.

Nam. 109

Uimarishaji wa Vituo vya Zimamoto na Uokozi katika Bandari za Zanzibar

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza:

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ni sehemu muhimu inayoweza kuwavutia wawekezaji na kukuza uchumi wa Zanzibar kutokana na jukumu lao la kuhakikisha usalama unapatikana katika bandari na viwanja vya ndege vya Zanzibar. Hata hivyo, jambo la kusikitisha ni kwamba hadi hii leo hakuna kituo cha Zimamoto kinachotoa huduma zake katika bandari zetu.

(a) Je, serikali inawaeleza nini wananchi kuhusiana na hali hiyo.

(b) Je, serikali inatoa ahadi gani kwa mwaka huu wa fedha itakayopelekea kuanzisha vituo vya Zimamoto kwa kuanzia katika bandari ya Malindi na bandari ya Mkoani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 109 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi juu ya umuhimu wa kuwepo kituo cha Zimamoto katika bandari zetu kwa ajili ya usalama wa raia na pia wa maboti dhidi ya matukio ya moto hapo bandarini.

(a) Kwa hivi sasa Mhe. Spika, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kinashirikiana kwa karibu sana na Uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar ili kupata eneo muafaka kwa kuanzia katika bandari ya Malindi Unguja kwa ajili ya kuweka kituo hicho. Hatua kama hiyo itachukuliwa pia katika bandari nyengine ikiwemo bandari ya Mkoani.

(b) Hata hivyo, Kikosi cha Zimamoto na Shirika la Bandari kwa pamoja wanahakikisha kwamba kila siku kuwepo vifaa vya tahadhari vya kukinga moto na vile vya huduma ya kwanza katika kuzimia moto katika bandari zetu. Yaani vifaa hivyo viwepo katika hali nzuri na vinakaguliwa kwa wakati ili kuepusha maafa.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Kikosi cha Zimamoto kina idadi ndogo sana ya askari kulingana na kazi zao. Je, Mhe. Waziri kwa mwaka ujao wa fedha wizara yako ina mpango gani wa kuongeza askari katika idara hii muhimu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kwa mahitaji yalivyo inabidi tuwe na wapiganaji zaidi katika sehemu nyingi. Lakini si rahisi hujui moto utatokea wapi na siku gani.

Kwa hiyo, nafikiri cha kujiandaa ambacho kikosi chetu na serikali yetu inafanya ni kutoa mafunzo kwa taasisi mbali mbali ili taasisi zenyewe kuweza kujikinga na moto utakapotokea pale. Kama nilivyosema muhimu tushirikiane kuweka vile vifaa vya zimamoto *(fire extinguishers)* na halafu tupate mafunzo yake ya kuvitumia. Vinaweza kuwemo lakini huna mafunzo, pale unaambiwa ligeuze uligonge lipasuke mwengine hata kulisogelea atashindwa.
Kwa hiyo, tunaomba sana Mhe. Spika, taasisi zote za serikali na hata za binafsi tushirikiane na mabingwa wetu hawa wa Zimamoto wapate mafunzo na hili tumeshalisema sana. Vifaa vipo au tutashirikiana nao wenyewe watavinunua na kuviweka. Hilo ndio suala la msingi kabisa tunalolipigania kwanza.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tunaelewa visiwa vyetu hivi vya Unguja na Pemba jiografia yake imekaa nyengine inakwenda nyuma nyengine inakwenda mbele inarudia kule kule. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba sasa imefika wakati kwa kila mkoa angalau kuwa na gari la Zimamoto.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubaliana nae moja kwa moja na ushauri wake na hiyo ndio sera hasa ya serikali yetu. Tunajitahidi mbali ya kuweka vituo lakini pia kuwa na zana kwa sababu kuweka vituo bila ya zana haitosaidia. Mhe. Spika, tunajitahidi tuwe na zana na *Alhamdulillah* kwa sasa niseme hatuna vingi lakini tunavyo vifaa vya kutosha kiasi ya kuvigawa katika mikoa yetu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa na mimi fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Zanzibar ni visiwa na Kikosi cha Zimamoto kwa Zanzibar kinaitwa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Kwa sababu Zanzibar ni visiwa tuna mameli, maboti, majahazi na yote hayo yanafanya kazi baharini. Wakati wanafanya kazi baharini mnakuwa mnatokea aidha moto mara kwa mara au ajali nyengine.

Kwa sababu Kikosi cha Zimamoto ni Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na wakati Zanzibar mpaka sasa hivi sijaona kuwa tuna zana zinazoweza kuzima moto baharini wakati unapotokea.

Je, ni lini serikali yetu kupitia wizara yake itajipanga ili kupata zana inapotokea ajali ya moto baharini waweze kufika na kwenda kuuzima.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba ni kweli nchi yetu ni ya visiwa na kuna haja ya kuwa na vyombo vya kufuatilia vyombo vyetu au wananchi wetu ambao wengi ni wavuvi na wanaovua nyakati za usiku na hutumia kidogo vibatari au taa ambazo zinaweza kusababisha moto. Kukabiliana na hayo serikali ina mipango ya kufanya manunuzi ya boti za kuzimia moto *(fire fighting boat).*
Lakini pia suala la msingi ni suala la mawasiliano ya uhakika ndani ya kikosi na wananchi wenyewe. Hili nalo tutalipa kipaumbele angalau kuwa tuna *redio call* katika sehemu zetu zote hizi za bandarini ili matukio yanapotokea tu basi hawa ndugu zetu wa Zimamoto waweze kujulishwa haraka sana na kuanza kuitikia ule wito wa kwenda kuhami hali.

Nam. 136

Serikali kushindwa kulipa Fedha kwa Wakati

Mhe. Salum Amour Mtondoo - Aliuliza:

Ni muda mrefu sana serikali imeshindwa kuwalipa fedha waliokuwa wanaushirika wa *Beit-el-Ras Building Brigade (BBB)* baada ya eneo na mali

zao kuuziwa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) hapo Mtoni. Jambo hilo limewasababishia usumbufu mkubwa waliokuwa wanaushirika huo.

(a) Je, serikali inatoa tamko gani kwa waliokuwa wanaushirika hao.

(b) Kwa kuwa serikali imeshindwa kulipa kwa wakati kama mkataba unavyoeleza. Je, Mhe. Waziri kuna malipo yatakayotolewa kutokana na usumbufu uliowapata wahusika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 136 lenye kifungu (a) na (b) lakini kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Spika, Kampuni ya *Beit- el - Ras Building Brigade Co-operative Society (BBBCS)* ilikuwa inaidai serikali jumla ya Tsh. 292,750,000/= (Tsh. Milioni mia mbili tisini na mbili laki saba hamsini elfu tu) kutokana na eneo na mali zao zilizokuwepo katika eneo la Mtoni kuuziwa Jeshi la Kujenga Uchumi mnamo mwaka 1999. Kati ya fedha hizo Tsh. 250,000,000/= (Tsh. Milioni mia mbili na hamsini tu) ni deni la msingi *(principal)* na Tsh. 42,750,000/= (Tsh. Milioni arobaini na mbili laki saba hamsini elfu tu) ni riba iliyotozwa na Ushirika baada ya Serikali kuchelewa kulipa deni hilo kutoka mwaka 1999 hadi mwaka 2007.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa makubaliano baina ya ushirika na serikali kwa barua yenye kumbukumbu nambari KU/BBCS/2009/VOL II/3/5 ya tarehe 11/03/2009 na barua yenye kumbukumbu nambari KU/BBCS/2009/VOL II/3/9 ya tarehe 20/04/2009 zinahusika. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imelipa jumla ya Shs. 291,850,000/= milioni na Shs.900,000/= zilizosalia kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa baina ya makubaliano ya serikali na ushirika zimesamehewa.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:-

a) Tamko la serikali kuhusu suala hili ni kama nilivyoeleza kwenye utangulizi ni kuwa kumbukumbu zinaonesha deni lote limelipwa.

b) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwenye utangulizi kuwa serikali imelipa jumla ya Shs. 41,850,000/= milioni ikiwa ni fidia kwa usumbufu walioupata wanaushirika wa kuchelewa kulipwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri na ya fasaha. Lakini pamoja na hayo naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenvye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mbali na waathirika ambao Mhe. Waziri amewataja yaani *Beit El Ras Building Brigade Co-operative Society (BBBCS)*, lakini pia wananchi wa Mtoni walipata madhara ya kuvunjiwa nyumba zao na wakaondoshwa hapo.

b) Mhe. Spika, serikali iliunda tume ya kufanya makadirio na tathmini ya wananchi hao na tume hiyo ikapendekeza kwamba wananchi hao wapatiwe fidia ikiwa ni pamoja na kupewa viwanja kwa ajili ya kujengwa nyumba. Tangu nyumba hizo zivunjwe sasa ni miaka 15. Naomba kujua nini maamuzi ya serikali wakati ni tume na serikali iliyopendekeza kwamba wananchi wapewe fedha na viwanja vya kujenga nyumba hizo.

   Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri ameonesha kuwa serikali imeitikia wito wa kulipa deni hili. Je, anasemaje kwa maeneo mengine ambayo serikali huvunja nyumba na kuchukua viwanja na hadi leo hii hawajalipwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kuhusiana na fidia pamoja na maamuzi ya kupewa viwanja kwa wananchi katika maeneo ya Mtoni.

a) Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba anipe nafasi nilifuatilie suala hili ili na mimi niweze kuliendea kwa kina na baadae nitampa majibu yangu kwa maandishi.

b) Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe ametaka kuelewa katika maeneo mengine serikali inazungumzaje kuhusu fidia pale tunapotaka kutumia maeneo yale kwa maendeleo ya nchi.

Mhe. Spika, nataka niseme tu kwamba huko nyuma kulikuwa kuna utaratibu kwamba fidia haioanishwi na mradi na ndio maana muda mrefu serikali imekuwa ina madeni ya fidia. Lakini sasa tumebadilisha utaratibu, mradi wowote unaokwenda katika maeneo ya wananchi kama kutakuwa kuna uharibifu basi mradi ule unaunganishwa na fidia. Kwa maana hiyo nadhani katika kipindi hiki fidia zinatoka tatizo ni kwamba labda huwa zinachelewa tu. Basi tutahakikisha kuwa fidia hizo zinatoka kwa wakati ili kabla mradi kuanza wale wananchi wawe wanapata fedha zao.

Nam. 124

Ajira ya Ualimu kwa Wahitimu wa Ngazi ya Cheti wa Mwaka 2007

Mhe. Mussa Khamis Silima – Aliuliza:-

Serikali iligharamia kuwasomesha vijana mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti ambao walihitimu mafunzo hayo mwaka 2007. Baadhi ya vijana hao tayari wameajiriwa na Wizara yako, lakini wapo wengi ambao hawajaajiriwa hadi leo na hasa wa Mikoa ya Kusini Unguja na Mjini/Magharibi.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwaajiri vijana hao.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 124. Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa ni baadhi tu ya wahitimu waliomaliza mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti mwaka 2007 walioajiriwa na baadhi yao hawajaajiriwa hadi hii na hasa wahitimu wanaoishi katika Mikoa ya Kusini na Mjini/Magharibi, Unguja, Wilaya ya Wete na Wilaya ya Chake-Chake hupo Pemba. Baada ya Maelezo hayo naomba kujibu kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, katika mwaka wa Fedha 2011/2012, Wizara yangu inakusudia kuajiri baadhi ya walimu waliomaliza mafunzo ya Shahada, Stashahada na Cheti cha Ualimu ili kupunguza ukosefu wa walimu katika baadhi ya skuli. Ajira hiyo itazingatia mahitaji halisi ya skuli na wala sio mwaka ambao mhitimu amemaliza mafunzo yake au Mkoa au Wilaya anayotoka. Kwa wahitimu waliomaliza mafunzo ya cheti cha ualimu mwaka 2007 na ambao wanaishi katika Mikoa na Wilaya ambazo ajira haikufanyika siku za karibuni, watapewa kupaumbele iwapo skuli za Mikoa na Wilaya zao zina mahitaji ya walimu na wanatimiza sifa za kielimu zinazotakiwa. Walimu wanaohitajika sana katika skuli zetu ni walimu waliofuzu na wana sifa za kufundisha masomo ya Sayansi. Hesabati, Sayansi Jamii na Kiingereza.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Kutokana na umuhimu na ukubwa wa elimu na kwa vile vijana hawa wanakaa muda mrefu nje baada ya kumaliza

mafunzo yao ya ualimu. Je, wizara haioni kwamba kuwaajiri moja kwa moja bila ya kuwapatia mafunzo ya ndani kunawapelekea kutokuwa na ufanisi wanapokwenda kufanya shughuli yao ya ualimu.

(b) Ni wale ambao wamemaliza masomo na ambao wizara itawahitaji. Je, hakuna utaratibu mwengine wa kuwawezesha ili kuwafanya waendelee kusomesha, lakini wakawa wanawangojea badala ya kuwaweka nje na kuanza kupoteza ile taaluma yao ambayo wanayo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakubali kwamba vijana hawa wamekaa nje kwa muda mrefu. Nataka kueleza wazi katika Baraza hili kwamba vijana hawa ambao wamekaa nje kwa muda mrefu karibu wote ni walimu wa *art* na ni walimu ambao wanaweza kusomesha madarasa ya chini, yaani darasa la kwanza mpaka nne la saba na ni wengi.

(a) Mhe. Spika, najua kuwa katika hali hiyo wataweza kupata tatizo kidogo la kusahau baadhi ya mambo, lakini hata hivyo kwa sababu uwezo wetu wa kuwaajiri kwa sasa hivi haupo, kwa hivyo inabidi wasubiri kidogo na tutawapunguza kidogo kwa mwaka huu unaofuatia wa 2011/2012.

(b) Mhe. Spika, kama ingekuwa vijana hawa wanakubali kusomesha bila ya kulipwa, jambo ambalo nadhani haliyumkiniki ni lazima watakataa. Kwa sababu madhumuni ya kutafuta ajira ni kutaka kupata malipo ili wajiendeshe maisha. Sasa kuwachukua ukawaingiza maskulini hawa bila ya kulipwa nadhani itakuwa haiyumkiniki.

Lakini kama waheshimiwa wanaweza kuwashawishi wakaweza kufanya hivyo, sisi katika baadhi ya Wilaya matatizo ya upungufu wa walimu tunayo, tukiacha Mkoa wa Mjini/Magharibi ambao hauna upungufu wa walimu, kuna upungufu wa walimu wa sayansi.

Nam. 45

Kunyanyua Vipaji vya Wanamichezo

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza:-

Katika kunyanyua vipaji vya wanamichezo wetu Serikali imejenga kijiji cha wana michezo huko Dole. Kwa upande wa Kisiwa cha Pemba ujenzi wa kijiji cha wanamichezo unasuasua ingawa eneo maalum limeshatengwa kwa kazi hiyo huko Gombani.

(a) Je, eneo lililotengwa kwa ajili ya wanamichezo limeshapimwa na kupatiwa hati miliki.

(b) Eneo hilo sasa limeanza kuvamiwa kwa ujenzi. Je, hatua gani zimechukuliwa na Serikali kulinusuru lisivamiwe zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika kunyanyua vipaji vya wanamichezo wetu Serikali imejenga kijiji cha wanamichezo huko Dole. Kwa upande wa Kisiwa cha Pemba ujenzi wa kijiji cha wanamichezo unasuasua ingawa eneo maalum limeshatengwa kwa kazi hiyo huko Gombani.

(a) Mhe. Spika, eneo lililotengwa kwa shughuli hizo ni eneo lililopo hapo katika uwanja wa Gombani Pemba, tayari eneo hilo limeshapimwa na tayari limeshapatiwa hati miliki. Mbali na ujenzi wa Kijiji cha michezo, eneo hilo pia litajengwa Hoteli kubwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanamichezo mbali mbali watakaotumia eneo hilo.

(b) Ni kweli eneo hili lilianza kuvamiwa na hasa katika kipindi cha 2000–2005, lakini juhudi zimechukuliwa kudhibiti uvamizi huo na tayari yangu imeshaweka nguzo kuzunguka na kudhibiti eneo hilo.

Mhe. Viwe Khamis Abdallah: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri hoteli hiyo ambayo itajengwa katika uwanja wa Gombani itakuwa chini ya udhamini wa nani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kuhusu nani mdhamini mkuu wa hoteli hiyo ni wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Ali Salum Haji: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Katika majibu yake mama ameeleza kuwa ujenzi wa Pemba unasuasua na kwa sababu serikali yetu inathamini shughuli za michezo. Je, wizara yake ina jitihada gani za uharakishwaji wa ujenzi huo

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli nimejibu kwamba ujenzi wa kijiji cha wanamichezo Pemba unasuasua. Ni kweli lakini tuna mipango thabiti ya kuweza kulitekeleza suala hili.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, mchezo wa mpira wa miguu ni mchezo unaopendwa Zanzibar na ulimwenguni kwa jumla. Tunaipongeza serikali katika kuwekeza katika kujenga vituo hivi vya michezo.

Mhe. Spika, swali langu ni kwamba mchezo huu unakwenda kisayansi na kiteknolojia. Wenzetu Ghana, Nigeria na nchi nyengine kama Senegal katika nchi za Afrika ya Kati huko wamewekeza katika kujenga hivi vituo na kuwaajiri makocha kutoka nje ili kuja kuviinua vipaji hivyo.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kuleta walimu wenye ujuzi na sifa kwa ajili ya kuinua vipaji vya watoto wetu.

(b) Mwaka 2009 Zanzibar katika Mkoa wa Mjini/Magharibi uliweza kutoa kombe la Kopa Cocacola kwa vijana ambao walikuwemo kwenye timu ile na Mhe Rais wakati tulipokwenda kula chakula cha pamoja katika kuwapongeza vijana wale alitoa ahadi ya kuwaendeleza vijana wale. Je, serikali ina mpango gani na wala hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kuwaendeleza vijana wale. Je, serikali ina mpango gani wa kuwakumbuka vijana wale.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru. Hivi sasa wizara yangu ina mpango wa madhubuti. Kwanza kuhakikisha kwamba tunafufua, licha ya mpira lakini kufufua michezo yote ambayo ilikuwa ni maarufu hapa visiwani na tutashirikiana na Baraza la Michezo ili kuhakikisha kwamba michezo yote ambayo ilikuwa maarufu kwa vipaji ifufuliwe yote.

Mhe. Spika, tumekusudia kwamba suala hili tutalianzia kwa ngazi ya maskuli, kwa sababu tumegundua kuwa kwenye maskuli ndimo ambamo kuna vipaji

vingi tu. Suala hili tayari tumeshaanza mazungumzo na mawizara ili tuhakikishe kila wizara iwe na timu. Ninaposema timu sikusudii ya mpira tu lakini kwa michezo yote ambayo ilikuwa maarufu hapa Zanzibar.

Halafu suala pili ni kuhusiana na mwaka 2009, kwa kweli hilo nilikuwa sina taarifa nalo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe anipe muda ili nilifuatilie na nitamjibu kwa kimaandishi.

Nam. 228

Utaratibu wa Serikali Kuhifadhi Watoto

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla sijajibiwa swali langu nambari 228 kwanza nataka nimpongeze waziri wa wizara husika kwa mashirikiano aliyotupa kwenye kamati. Ni mchapakazi mmoja mzuri sana. Vile vile nataka nimpe pole kwa kupoteza nguzo muhimu katika Wizara yake *Inna Lillah Wainna Ilahi Rajiun.* Sasa naomba nijibiwe swali langu.

Haki za watoto ni jambo muhimu la kuzingatiwa kwa makini katika maslahi ya mtoto na taifa kwa jumla. Njia mojawapo ya kuzilinda haki hizo ni kuwapa hifadhi watoto wote ambao wanashindwa kuhudumiwa ipasavyo na wazazi au walezi wao.

(a) Je, Mhe Waziri, kwa hali ilivyo sasa Serikali inatekeleza ipasavyo wajibu wake katika hili.
(b) Kama serikali inatekeleza wajibu wake ni utaratibu gani unaotumika kuwafikisha watoto kwenye mikono ya serikali.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto) - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 228 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-
Kabla ya kujibu swali, naomba nikubaliane naye kwamba kwamba haki za watoto ni jambo muhimu la kuzingatiwa kwa makini katika maslahi ya mtoto na taifa kwa ujumla. Njia mojawapo ya kuzilinda haki hizo ni kuwapa hifadhi watoto wote ambao wanashindwa kuhudumiwa ipasavyo na wazazi wao. Aidha, hii ni miongoni mwa misingi ilioelezwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto (*CRC*) pamoja na makubaliano ya nchi za Bara la Afrika.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sera ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mtoto, naomba kumfahamisha Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu kwamba suala la Haki za Mtoto linaanzia katika familia na ni jukumu la mzazi au mlezi kutekeleza majukumu hayo. Aidha, dhamana na majukumu ya mzazi/mlezi ni haya yafuatayo: Kuhakikisha mtoto anapata haki ya kuishi, utu, heshima, uhuru, afya, elimu, kinga, makaazi na mengine yoyote ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya mtoto kimwili, kiakili, kiroho, kimaadili na kijamii.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, Serikali inatekeleza ipasavyo wajibu wake katika hili. Katika kutekeleza wajibu huo Kitaifa, Serikali kupitia Wizara imeandaa mifumo ya kitaasisi na kiutendaji ikiwemo:

- Kuwepo kwa Idara inayoratibu masuala ya watoto, Kitaifa na Kimataifa.
- Kuwepo kwa Idara inayoshughulikia watoto wanaoishi katika mazingira magumu.
- Kuwepo kwa Sera ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mtoto.
- Wizara imeandaa Sheria ya Mtoto, ambayo imeshapitishwa na Baraza lako hili tukufu.
- Kuwepo kwa nyumba za kulelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu.
- Wizara imeandaa taratibu mbali mbali za kuijengea uwezo jamii na taasisi zinazoshughulikia watoto
- Miongozo mbali mbali imeandaliwa inayoelekeza taratibu za kutoa na kupatikana kwa huduma za watoto.
- Wizara inaendeleza mashirikiano ya ndani na nje ya nchi katika kuhakikisha maslahi ya watoto yanafikiwa.
- Wizara inafanya ufuatiliaji na tathmini ya hali inayoendelea katika makuzi na huduma za watoto.

(b) Mhe. Spika, naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako tukufu, Wizara yangu kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii imeandaa utaratibu ufuatao:-

Mzazi au Mlezi wa Mtoto anayetaka hifadhi au msaada, hupaswa kuleta barua ya maombi kupitia kwa Sheha wa eneo analoishi ambapo Ofisa Malezi akifuatana na Sheha hufuatilia makaazi ya mtoto huyo kwa ajili ya kufanya tathmini na kuandika ripoti ambayo hupelekwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii. Matokeo ya ripoti hiyo ndiyo yatakayothibitisha kuwa kweli mtoto huyo anastahiki hifadhi au msaada.

Kwa upande wa watoto wanaotupwa, kesi hizo huripotiwa Polisi na baadae kupelekwa hospitali na hatimae kupelekwa nyumba ya kulelea watoto. Mfumo huo hutumika kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Jaku Hassim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Sayyidna Abubakar kwa majibu yake mazuri aliyonipa. Vile vile hili suala kwa upande mmoja litakuwa limefika pahala ndipo.

(a) Je, watoto walioko magerezani serikali ina mpango gani wa kuwaangalia kutokana na vitendo viovu vilioko huko gerezani.

(b) Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ina mpango gani wa kujenga nyumba ya kulelea watoto katika kisiwa cha Pemba kama ilivyokuwepo Mazizini. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, ni kweli na hata wizara na serikali kwa jumla inaumia sana kuona kwamba watoto walioko magerezani wanawekwa pamoja na watu wazima. Hili ni jambo ambalo serikali hailipendi hata kidogo.

Hivi sasa wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, tuna utaratibu ambao tunauandaa ili kuhakikisha kwamba watoto wote watakaopata hatia na kupelekwa gerezani, basi hawatowekwa pamoja na watu wazima.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Pemba hakuna nyumba ya kulelea watoto, tulianza kwa hapa Unguja tukajenga nyumba nzuri ya kulelea watoto. Hivi sasa tunaandaa utaratibu ili tuweze kujenga nyumba kama hiyo kwa upande wa Pemba. Lakini kwa hivi sasa watoto ambao wanapata mazingira magumu na wanaohitaji msaada wa serikali baada ya kwishakukamilisha utaratibu

niliioueleza hapo basi wanachukuliwa na kuletwa Unguja. Lakini hatua zipo na tunaziendeleza ili tuweze kupata nyumba kama hiyo kwa kisiwa cha Pemba.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri huko nyuma watoto walikuwa katika jengo la Forodhani na waliwekwa na Mhe. Abeid Aman Karume.

(a) Je, Mhe. Waziri ni sababu gani zilizopelekea watoto wale wakahamishwa na wakapelekwa katika eneo ambalo tumeambiwa ni la ZAYEDESA ambayo hiyo ni *NGOs*.
(b) Je, hiyo ZAYEDESA imewapa serikali hati miliki.

Mhe. Spika: Hili swali liliwahi kujibiwa huko nyuma na ni hivi hivi alivyoliuliza Mhe. Mjumbe. Kwa hivyo, sikumbuki ni swali gani lakini katizame *Hansard* utapata hilo jibu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana. Mhe. Spika, Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto ni kitengo muhimu sana, na hivi sasa kitengo hiki afisi yake ni kwenye uchochoro mdogo sana ambao hauwezi kutoa nafasi kwa mtoto na hata walezi wake kusikilizwa matatizo yao.

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa makaazi ni moja ya haki ya mtoto kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa. Je, serikali kwa kupitia wizara yake Mhe. Waziri itafanya nini ili kitengo hiki kukipatia afisi nzuri na ya kisasa ili hifadhi ya mtoto iweze kulindwa.
(b) Kwa kuwa Mhe. Waziri alipata msiba mkubwa wa kufiliwa na Katibu Mkuu wake mwanamke na kwa kuwa Mhe. Rais kwa busara zake amemteua tena Katibu Mkuu mwanamke. Je, anaweza kuniambia mashirikiano yake na Katibu Mkuu yataongezwa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, unajua maneno yake kidogo kutokana na hali alivyo, sasa hili swali la mwisho sikulisikia. Kwa hivyo, naomba alieleze kidogo.

Mhe. Spika: Rudia swali la mwisho kwa taratibu kidogo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, swali la mwisho ni kwamba Mhe. Waziri wa wizara hii alikuwa na mashirikiano makubwa sana na Katibu Mkuu

aliyefariki, kwa kuwa na mara hii Mhe. Rais amemteua tena Katibu Mkuu mwanamke. Naomba kujua je, mashirikiano haya yataendelea.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Mjumbe kwa maswali yake mawili. Mhe. Spika, sote tunajua kwamba wizara nyingi ambazo tunazo majengo yake hayako katika hali nzuri. Ni *policy* ya serikali kwamba kila wizara inatakiwa ifanye juhudi ili iweze kujenga afisi nzuri kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wake.

(a) Miongoni mwa *policy* hizo ni pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kuhakikisha kwamba tutajitahidi kujenga majengo mazuri na afisi nzuri kwa kutoa huduma zinazohusika.

(b) Ni kweli tulikuwa tuna ushirikiano mzuri na Marehemu Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema, Amin.

Vile vile tumepata Katibu mwengine ambaye ni mwanamke na tunaahidi kwamba tutaendeleza ushirikiano huo, ushirikiano wetu utakuwa mzuri tena wa kupigiwa mfano na nyote mtauona. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, baada ya semina kubwa sana iliyotolewa kwa kweli naamini ahadi yake itakwenda sawa.

Nam. 147

Kuimarishwa Kiuchumi Wananchi wa Pemba

Mhe. Rufai Said Rufai – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu wananchi wa Pemba wamekuwa wakitegemea karafuu kama zao la biashara. Hivi sasa zao hilo limepungua kwa zaidi ya asilimia 40%.

Je, wizara yako imejipangaje kuwanyanyua wananchi hao waliotegemea zao hilo la karafuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 147 kwa utangulizi ufuatao:-
Ni kweli Mhe. Spika nakubaliana naye kwamba zao la karafuu ni moja kati ya mazao yenye tija na umuhimu mkubwa wa uchumi wa Zanzibar na wananchi

wake, kwa muda mrefu wananchi wa Pemba wamekuwa wakitegemea zao la karafuu kama zao la biashara.

Pamoja na kupungua kwa uzalishaji wa zao hili bado takwimu zinaonesha kuwa katika msimu wa mwaka 2008/2009 – 2009/2010 karafuu zenye wastani wa tani 2,673 zimeuzwa na kwamba wakulima wa zao hilo hilo wanafaidika na malipo ya ununuzi wa karafuu hizo, ambapo mauzo yalifikia kati ya shilingi 7,000 milioni na 12,000 milioni.

Mhe. Spika, katika kukabiliana uendelezaji wa zao la karafuu na biashara yake. Serikali imeamua kufanya mageuzi makubwa ya uendelezaji wa zao la karafuu pamoja na kulifanyia mabadiliko ya kimuundo na kisheria Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC*), ili liweze kukabiliana na changamoto hizo. Mageuzi hayo yatajumuisha mambo makuu yafuatayo:-

- Kuandaa Sheria mpya ya *ZSTC*, ambayo itaainisha majukumu mapya ya shirika hilo katika kuendeleza biashara ya karafuu.
- Kuandaa muundo wa shirika pamoja na kupendekeza wafanyakazi wanaohitajika na aina ya taaluma (*skills*) zinazohitajika.
- Kufanya mapitio ya gharama za uendeshaji wa shirika hilo.
- Kuandaa Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Karafauu (*Clove Development Fund*), ambao utafanya pamoja na mambo mengine, kazi ya kuendeleza uzalishaji wa zao la karafuu pamoja na kulinda mapato ya wakulima wa karafuu, iwapo zao litakosa wanunuzi katika Soko la Kimataifa.

Vile vile Mhe. Spika, tutakumbuka katika Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo jana, alizungumzia juu ya kuandaa utaratibu wa kuwasiliana na mtumiaji wa karafuu moja kwa moja badala ya kuendelea na utaratibu unaotumika hivi sasa wa kumtumia mtu wa kati, yaani *middle man*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, matayarisho ya mapendekezo ya sheria hizo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo ikiwemo uendelezaji wa zao hili muhimu la karafuuu tunatarajia itakamilika hivi karibuni na kuwasilishwa rasmi. *(Makofi)*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kuna usemi kwa wakulima wa zao la karafuu, yaani mkarafuu umefika muda wa kuondoka duniani. Je, usemi huu Mhe. Waziri yako unachukua hatua gani kama tayari umeshapata kuusikia?

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nadhani ni vyema uukarudia kidogo na kielekee kitu cha kuzungumzia.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, kuna usemi kwa wakulima wa karafuu, kwamba hivi sasa mkarafuu umefikia muda wa kuondoka hapa ulimwenguni, kwa sababu iliopo inakufa na ile inayopandwa pia haioti. Mhe. Spika, kwa ushahidi baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walizungumza ndani ya Baraza walisema kuwa wamepanda 20 na umekua mmoja na wengine wamepanda kumi na wala hakuna hata mmoja.

Kwa hivyo, wakulima wa karafuu wanasema mkarafuu kuishi duniani umeshamaliza muda wake wa kuishi duniani. Sasa je serikali au wizara usemi huu wanaufahamu au ni *propaganda* za wakulima wa karafuu?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, mikarafuu ikipandwa na kuzingatia utaratibu wa wataalamu inaona. Kwa hivyo, nataka nimfahamishe Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba kufuatia ziara ya Mhe. Rais hivi karibuni katika mikoa yote ya Unguja na Pemba.

Tulikwenda kisiwani Pemba na tukaona mikarafuu ambayo imeoteshwa na imestawi tena kwa muda mfupi tu wa miaka mitano tayari imeshaanza kutoa maua na inaonesha uzazi wa mikarafuu hiyo ni mikubwa sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe astahamili pamoja na utaratibu huo mzuri wa kuotesha upya mikarafuu. *(Makofi)*

Lakini kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi ni kuwa utaratibu unaandaliwa na serikali wa kuliwezesha Shirika hili la *ZSTC*, ili hatimaye wakulima wetu pamoja na nchi kwa jumla tuweze kufaidika na zao hili. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika takwimu zilizopo kila wakati wa msimu unapofika idadi ya karafuu zinazochumwa kupelekwa Shirika la *ZSTC* kwa ajili ya kuuzwa inapungua. Vile vile kuna karafuu zinazotoka nyingi kwa biashara ya magendo hata kwenye bajeti iliyopita taarifa hiyo ilikuwemo.

Mhe. Spika, kwa sababu kazi ya magendo ni kazi mbaya sana na kama mtu akikamatwa adhabu yake anayoipata ni kubwa sana. Lakini watu wanaacha kuuza karafuu kwenye Shirika la *ZSTC* na kujitolea maisha yao kwa kutumia njia ya magendo. Hali hii husababishwa na kupata bei nzuri sana.

Kwa kuwa serikali imeshaona na kuamua kumbe sababu ya wananchi kupata bei ndogo ya karafuu ni kwa kuwa walikuwa wakiziuza kwa mtu wa katikati na siye yule mnunuzi hasa.

(a) Swali langu lipo hapa, taarifa hii Shirika lilikuwa linauza kwa mtu ambaye siye mstahiki kwa wananchi lilijulikana lini?

(b) Ni kiasi gani cha fedha za hasara zilizopatikana kwa hizo karafuu zilizouzwa na Shirika la *ZSTC* kwa mnunuzi huyo wa katikati angalau kwa msimu huu wa chumo la karafuu?

(c) Je, mpango huu mpya wa kuziuza karafuu kwa huyo mstahiki hasa kwa manufaa ya wakulima wa karafuu na nchi kwa jumla utaanza lini?

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, maswali yetu yawe mafupi na hasa kama yanatofautiana hayana mtiririko, basi inafanya swali kuwa refu. Kwa hivyo, tujitahidi tufupishe maswali hasa ya nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, nimezungumza katika majibu ya swali mama kwamba kwa kuzingatia hayo yote ambayo ameyauliza ndio maana serikali kupitia Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko inataka kulifanyiakazi hilo.

Katika kulifanyiakazi tatizo hilo Mhe. Spika, ndio maana nimeorodhesha na kuyasoma mbele ya Baraza lako hili tukufu mambo haya matano ikiwemo kutoa tatizo hili la huyu mtu wa kati, ili tuweze kuwasiliana na mtumiaji moja kwa moja, lakini pamoja na jinsi ya kukabiliana na hili tatizo la magendo.

Mhe. Spika, tunatoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wote ambao ndio wenye wananchi karafuu ziuzwe katika Shirika letu la *ZSTC*, kwa sababu ndio tutapata huduma zile muhimu kutokana na mapato haya. Kwa hivyo, kama zitauzwa kimagendo Mhe. Spika, basi huduma nyingi muhimu ikiwemo afya na elimu kwa watoto wetu pamoja na barabara inakuwa ni matatizo, kwa sababu fedha hizo zinakwenda kwa nchi jirani.

Lakini ubora wa karafuu Mhe. Spika, kwa kweli karafuu za Zanzibar zina ubora wa pekee katika Soko la Dunia na zinatambulikana. Kwa hivyo, ndio maana hivi sasa serikali imeamua kuifanyia *branding* karafuu ya Zanzibar, ili popote pale itakapouzwa ijulikane kwamba hii ni karafuu ya Zanzibar na hizo za Lindi na sehemu nyengine basi zitajulikana kama sio za Zanzibar Mhe. Spika. *(Makofi)*

Nam. 19

Kulipa Fidia kwa Barabara ya Chwale – Likoni

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Barabara ya Chwale – Likoni imefanyiwa tathmini ya nyumba na vipando kwa zaidi ya miezi mitano. Lakini hadi leo malipo ya nyumba na vipando hivyo hayajafanyika wala hatuelewi ni lini ujenzi huo utaanza na kwa kiwango gani.

(a) Ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza na kukamilika.

(b) Je, barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami au kifusi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako kabla sijamjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 19 lenye kifungu (a) na (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, barabara ya Chwale hadi Likoni ni miongoni mwa barabara sita, zilizomo katika orodha ya Ufadhili wa Mradi wa Shirika la Maendeleo la Marekani *MCC* na barabara hizo kwa ujumla zina urefu wa kilomita 35.

Barabara hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Barabara ya kutoka Kipangani hadi Kangani yenye urefu wa kilomita 2.7;
(ii) Barabara ya Chwale hadi Likoni Kojani yenye urefu wa kilomita 1.9;
(iii) Barabara ya Mzambarautakao Pandani hadi Finyi yenye urefu wa kilomita 7.9;
(iv) Barabara ya Mzambaraukarimu hadi Mapovu yenye urefu wa kilomita 8.7;
(v) Barabara ya Bahanasa Daya yenye urefu wa kilomita 6.7 na
(vi) Barabara ya Makongeni Daya hadi Mtambwe yenye urefu wa kilomita 7.1. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa barabara hizo utaanza mara baada ya kukamilika taratibu za kumpata Mkandarasi. Kwa hivyo, mategemeo yetu kwamba katika

kipindi hiki kutoka mwezi wa Juni na Julai Mkandarasi tayari atakuwa ameshapatikana na ujenzi utaanza mara moja.

(b) Barabara hiyo pamoja na nilizozieleza hapo awali zote zitajengwa kwa kiwango cha lami.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, hivi sasa nitauliza swali moja dogo. Mhe. Naibu Waziri wakati alipokuwa akielezea hizi barabara zitakazojengwa moja ni Bahanasa Daya na nyengine Daya Makongeni, lakini pia kulikuwa na Daya Uondwe. Je, hii imefutwa hakuitaja.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, naomba urudie tena.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, wakati Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akitaja hizi barabara zitakazojengwa, sasa alipotaja barabara ambazo zimo ndani ya Jimbo langu alitaja Bahanasa Daya na Daya Makongeni, lakini Daya Uondwe sikuisikia tuseme kipande hiki kimefutwa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, mradi huu kama ulivyoelezwa kwenye jibu la swali mama kifungu cha (b) wenye urefu wa kilomita 35. Moja miongoni mwa barabara ambayo tunaijua kwa jina moja tu Bahanasa Mtambwe, lakini imegawika sehemu mbili, kwa sababu Bahanasa Mtambwe ni barabara itakayoanza Bahanasa mpaka Daya, kutoka pale inakwenda kusini mpaka Makongeni, lakini hapo hapo Daya inakwenda mpaka Skuli ya Uondwe.

Kwa hivyo, barabara ambayo kama ina *shape* ya T, yaani ukifika Daya unakwenda kusini Makongeni na pia unaweza kwenda kaskazini Skuli ya Uondwe na pale ndipo barabara chini ya ufadhili huu itakapoishia na itakuwa kwa kiwango cha lami. Mhe. Spika, kutoka Uondwe mpaka Nyali baharini itafanywa na serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana. Kwa hivyo, naomba kujua barabara ya Chwale Likoni bado haijajengwa, lakini tayari wananchi wame wameshapewa fidia, barabara ya Mtambile Mwambe imejenga na tayari imeshakamilika na wala hakuna suala ya fidia na wala serikali haijatoa kauli.

Kwa hiyo, naomba kujua kwamba serikali imechukua kigezo gani kwamba yule ambaye bado hajajengewa akalipwa na yule ambaye ameshajengewa hajalipwa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika ujenzi wa barabara ziko namna tatu kutokana na ufadhili wenyewe. Kwanza kuna barabara zinazojengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar peke yake. Kwa mfano, barabara ya Kiwani Mtuhaliwa. Pili ni ufadhili wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na mfadhili mwengine ama ni benki au nchi. Kwa mfano, Wete Gando, Wete Konde. Tatu ni ufadhili ni mmoja tu. Kwa mfano, ni hizi barabara sita za *MCC*. Sasa kila mmoja anao utaratibu wa ujenzi huo na namna ya kulipa fidia.

Kwa hivyo, ujenzi huu wa barabara sita chini ya ufadhili wa *MCC* kila kitu, yaani kuanzia vipimo, thathmini, ulipaji wa fidia, namna ya kutafuta mkandarasi, ujenzi unafanywa na *MCC* ni *totality*. Kwa maana hiyo, serikali kazi yake ni kutoa taarifa na *information* zinazohusika na ikiwezekana pale ambapo wanatakiwa watu maalum.

Hivyo, miradi ya kundi la kwanza na la pili inayofadhiliwa na serikali peke yake au serikali na mfadhili mwengine fidia zake, basi fidia zake zinalipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na inalipa kutokana na uwezo wa serikali. Kutokana na hali hiyo, hii barabara inayojengwa hivi sasa ambayo anayoizungumzia Mhe. Mjumbe na hizi ni barabara zote sita za Kusini, basi fidia inalipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ndio maana hatujalipa fidia kwa vipando na vitu vyengine isipokuwa majengo.

Kwa upande wa kundi la tatu kwa hivi barabara sita ambazo zimetajwa hapa hizi zimelipwa na *MCC* na ndio maana kwamba wamelipwa fidia ya vipando, majengo na ujenzi unaweza kuanza wakati wowote. Kwa kweli haya ni maamuzi ya serikali baada ya kuona kwamba hawatoweza kufanya vitu vyengine au vyenginevyo msaada huu kama si masharti hayo, basi ingebidi tuukose, nadhani ni kwa faida zaidi kwamba watu wamelipwa ndio ujenzi unaanza.

Mhe. Spika, nafikiri ni vizuri kwa taarifa ya Waheshimiwa Wajumbe wote, kuwa tunazo namna tatu za ujenzi pamoja na ufadhili au kugharamia ujenzi huo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Nam. 116

Serikali Kuondosha Adhabu ya Kifo Zanzibar

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza:-

Wanaharakati wa masuala ya Sheria na Haki za Binaadamu wanapinga kuendelea kwa adhabu ya kifo. Hata Katiba ya Zanzibar inaheshimu haki ya kuishi kwa wanaadamu wote, jambo ambalo hata Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binaadamu wa mwaka 1948 unaiheshimu. Hata hivyo, Sheria ya Adhabu ya Zanzibar (*Penal Act* Nam.6 ya mwaka 2004) inaruhusu kutolewa kwa adhabu ya kifo kwa mshtakiwa kunyongwa hadi kufa.

(a) Je, Mhe. Waziri, huoni kuwa Sheria hii ama vifungu hivi vya Sheria vinavyoruhusu adhabu ya kifo, vinakwenda kinyume na Katiba ya Zanzibar na matakwa ya Mikataba ya Kimataifa.

(b) Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba, wakati sasa umefika wa sheria hii kuondolewa kwenye vitabu vya Sheria za Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 116 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binaadamu wa mwaka 1948 na hata Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 zinaheshimu haki ya kuishi kwa wanadamu wote.

(a) Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya mwaka 2004 (*Penal Act*) kupitia kifungu cha 26 (a) inaruhusu Mahakama kutoa adhabu ya kifo kwa baadhi ya makosa. Kwamba mtu yeyote atakaetiwa hatiani kwa kosa ambalo linatoa adhabu ya kifo pale inapoona inafaa Mahakama inaweza kutoa adhabu hiyo. Mahkama wanaweza kuendelea kuitoa adhabu hiyo kwa vile bado sheria inaruhusu kufanya hivyo.

Mhe. Spika, kutoa adhabu ya kifo Mahakamani si kwenda kinyume na Katiba ya Zanzibar wala Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki za Kibinaadamu. Katiba ya Zanzibar kifungu 24 inaelezea mipaka ya uhuru wa mtu na hifadhi, kwa haki na wajibu, kwa maana hiyo uhuru wa mtu unaweza kubanwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi (kifungu 24 (1) iwapo tu kibano hicho ni lazima.

Kwa msingi hii ndio Sheria No. 6 ya mwaka 2004 (*Penal Act*) kifungu 26 (a) kikaruhusu kutoa adhabu ya kifo kwa baadhi ya makosa. Kifungu 25 (i) cha Katiba kina sisitiza zaidi kwamba uhuru wa mtu lazima uwe unaheshimu haki na uhuru wa mwengiane na iwe kwa faida ya jamii.

Kwa maana hiyo, kwa mfano huwezi ukasema wewe una uhuru wako na ukaenda kumchukulia maisha yake mtu mwengine. Hilo ni kosa kubwa na ndio maana Katiba ikakataza uhuru wa namna hiyo na kuruhusu ifanywe sheria ya kutoa adhabu kwa watu aina hiyo.

(b) Adhabu ya kifo bado inamjadala mkubwa duniani kama iondolewe au la. Kundi moja linafikiria kwamba adhabu hii isiondolewe kwa sababu mtu anaefanya kosa hili, basi lazima na yeye ajuwe kama akipatikana na hatia naye atanyongwa. Kundi la pili linasema kuwa adhabu hii inaongeza vifo kwa sababu jambazi wa kutumia silaha anapokwenda kuiba, basi yeyote ataemuona atamuuwa kwa sababu ya kuficha ushahidi wake.

Mhe. Spika, bado suala hili halijapata ufumbuzi wa kudumu. Kwa hapa Zanzibar ni wajibu wetu kuelimishana na kupata maoni ya wananchi pamoja na vyombo husika kama vile Tume ya Kuchunguza Sheria, wananchi wa kawaida, wizara, Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Mahakama na vyombo vyenginevyo.

Nimatumaini yangu baada ya kupata maoni hayo. Serikali hapo itazingatia kwa pamoja na baadaye kuweza kuamua moja kwa moja kama adhabu ya kifo iendelee kuwepo Zanzibar au ifutwe katika vitabu vyetu vya Sheria za Zanzibar.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, naomba nimuulize swali moja la nyongeza ambalo litakuwa na maelezo kidogo.

Mhe. Spika, miongoni mwa makosa ambayo mtu akiyatenda huhukumiwa kifo kwa mujibu wa Sheria zetu za Zanzibar ni Uhaini na Kuua kwa Makusudi. Kwa mfano, mwaka 2000 Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ilisema kwamba Zanzibar haiwezi kufanyika uhaini.

Mhe. Waziri swali langu lipo hapa marekebisho ya kumi ya Katiba ya Zanzibar, ambayo kwa sasa inaitaja Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je, hivi sasa Zanzibar inawezekana kufanyika kwa uhaini?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, utaratibu wa Mahakama ni kwamba Jaji anapotoa hukumu ile inaitwa ni *opinion* yake. Kwa mfano, Majaji wanaweza kusema hiki ndivyo kilivyo, lakini wengine wakasema hiki sivyo kilivyo na huo ndio utaratibu wa Mahakama popote ulimwenguni.
Mhe. Spika, ni kweli Mahakama ya Rufaa ilisema kwamba huwezi kufanya uhaini Zanzibar. Mimi binafsi kama ni Jaji mzoefu wa siku nyingi kama ni Mwanasheria mzoefu wa siku nyingi, basi nasema hukumu ile siikubali. Kwa mfano, unaweza kufanya uhaini Zanzibar na hapa ukitaka kupindua serikali tutakunyonga. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Hivi tokea sheria hii kupitishwa ni watu wangapi wameingia kwenye hatia na adhabu zao kutelelezwa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, adhabu ya kifo inao utaratibu wake hata kama Mahakama imesema mshtakiwa huyu amepatikana na hatia na anyongwe. Kwa hivyo, hawezi tu kunyongwa, baada ya hapo *file* lake lote lile linakwenda kwa Rais wa nchi na kipindi hiki ni Marais wengi wamekuwepo katika nchi yetu.

Sasa wakati anapopelekewa *file* lile kwamba huyu raia wako amehukumiwa kunyonywa kwa sababu moja, mbili, tatu. Mhe. Spika, Rais ambaye yupo Madarakani kwa wakati ule anaweza kulipitia na kusema basi mimi namsamehe kutoka kunyongwa, basi afungwe tu au apewe adhabu nyengine *final disition* ya kunyongwa iko, sasa kutokana na suala lako siwezi hapa kukwambia ni adhabu ngapi ambazo zimetolewa na kutekelezwa kwa sababu lazima tutizame yale majalada na ule uamuzi aliotoa kiongozi mkuu wa nchi.

Nam. 53

Wizara Kuanzisha Umeme wa Upepo na Umeme wa Jua

Mhe. Mohammed Haji Khalid - Aliuliza:

Kwa kuwa umeme unaotumika katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba unatoka Tanzania Bara na gharama za umeme huo nazo zinaongozeka mara kwa mara, hali itakayopelekea wananchi wetu wengi wanaoishi vijijini kushindwa kumudu matumizi ya umeme.

Je, Wizara haioni kwamba sasa wakati umefika wa kutumia rasilimali ya upepo na jua kwa lengo la kuzalisha umeme.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 53 kama ifuatavyo:

Napenda kumjuilisha Mhe. Mwakilishi kuwa Wizara yangu imeliona tatizo hilo, na imo mbioni kutafuta umeme mbadala wa Jua, Upepo na Mawimbi ya Bahari, ili kuhakikisha kufanikiwa kwa upatikanaji wa umeme huo ndio imeliingiza suala hili katika Sera ya Nishati.

Na tayari Makampuni kadhaa yamejitokeza na kuonesha nia ya kutaka kuwekeza katika umeme mbadala wa Jua, Upepo na Mawimbi ya baharini.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Kumekuwa na tatizo la kupata umeme wa mgao hapa Zanzibar kwa kipindi kirefu tukisingizia kwamba mvua hakuna au maji ni mahaba, lakini tumeona mvua zimeshanyesha nyingi sana sasa hivi lakini bado mgao ule unaendelea.

Ni lini mgao huu utamalizika na nini hasa tatizo la mgao wa umeme hapa Zanzibar ?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ni kweli Zanzibar pana tatizo la mgao wa umeme katika kipindi hiki tatizo ambalo linasababishwa na udogo wa kebo yetu iliyopo baharini ambayo inatoa umeme kutoka Kiromoni hadi Fumba, mahitaji ya umeme kwa Zanzibar kwa sasa inatakiwa MW 60 ha 65 kebo yetu iliyokuwepo baharini ina uwezo wa kuchukua MW 45 na kwa kuhofia tatizo lililotokea kipindi cha nyuma kwa sasa kebo hiyo tunaipa umeme wa MW 30 hadi 40.

Mhe. Spika, tatiizo hili litaondoka baada ya muda mdogo tu kwa kutandika kebo mpya ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua MW 100 tunategemea tatizo hili litaondoka kwa Zanzibar.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe leo ni hotuba yetu ya Makamo wa Pili wa Rais kwa maana hiyo nichukue nafasi hii kumkaribisha sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Mheshimiwa karibu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe**.** Spika**,** Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili lipokee, lijadili na hatimae liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe**.** Spika**,** Kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia afya njema na uzima wakati huu tukiwa pamoja katika kikao hiki cha kwanza cha bajeti, tangu kuanza kwa Serikali ya Awamu ya Saba yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Mhe**.** Spika**,** Napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa na wananchi kuongoza nchi yetu katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2010. Hii inaonyesha imani kubwa ambayo wananchi wa Zanzibar waliyonayo juu yake. Aidha, nampongeza Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo wa Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika**,** Namshukuru kwa dhati Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniteua kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Namuahidi kuwa nitamsaidia kadri ya uwezo wangu na nitatumia hekima na busara zangu katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Nakupongeza kwa dhati wewe binafsi Mheshimiwa Pandu Ameir Kificho na Naibu Spika Mheshimiwa Ali Abdalla Ali kwa kuchaguliwa kwenu kuongoza Baraza letu Tukufu. Nawapongeza pia Wenyeviti wetu, Mheshimiwa

Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi wa Viti Maalum na Mheshimiwa Mahmoud Mohammed Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kuteuliwa kwao kuwa Wenyeviti wa Baraza letu la Wawakilishi. Tuna matumaini makubwa kwamba mtaliongoza vyema Baraza letu katika kipindi hiki. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wote na Makamu Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kuchaguliwa kuongoza Kamati hizo. Pia nimpongeze Katibu wetu kwa kuteuliwa tena kuwa Katibu wa Baraza hili na nawapongeza wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa bidii yao katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, Napenda pia kutoa pongezi maalum kwa Chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa kuandaa na kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2010 - 2015 na Ilani zilizotangulia ambazo zimewezesha nchi yetu kupiga hatua ya maendeleo.

Napenda kutoa pongezi za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu wote na kuwatakia kheri, afya njema na baraka nyingi kwa Mwenyezi Mungu katika kutekeleza majukumu yao, pamoja na changamoto nyingi ambazo wamepania kuzikabili.

Mhe. Spika, Napenda kuwashukuru kwa dhati kabisa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Katibu Mkuu Dkt. Khalid Salum Mohamed na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Said Shaaban Said, wakurugenzi, watendaji na wafanyakazi wote wa Ofisi yangu kwa mashirikiano yao makubwa wanayonipa ambayo yamekuwa chachu ya mafanikio ya Ofisi yetu, na pia kwa kunisaidia kuiandaa hotuba hii.

Mhe. Spika**,** Napenda kwa njia ya pekee kuishukuru sana familia yangu kwa ustahamilivu wao na msaada mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Nawatakia kheri na Baraka za Mwenyezi Mungu. Vilevile, nachukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Kitope kwa mashirikiano yao ya dhati kwangu.

Mhe. Spika**,** Ni jambo la kufurahisha na kutia moyo kuona kwamba kikao cha Bajeti cha mwaka huu kinafanyika katika hali ya umoja, amani na utulivu ndani ya nchi yetu tukiwa na imani thabit na nia ya kushirikiana na wananchi katika kuleta maendeleo ya nchi yetu bila ya kujali itikadi za kisiasa. Aidha, nchi wahisani na mashirika mbali mbali ya kimataifa wanaendelea kutuunga mkono katika harakati za kuleta maendeleo kutokana na mazingira mazuri ya kisiasa yaliyojengeka ndani ya nchi yetu.

Namshukuru sana Mheshimiwa Rais akiwa ndiye Jamadari Mkuu wa kusimamia mabadiliko haya ambayo ulimwengu mzima unasifu juhudi zetu hizo. Hivyo, ni wajibu wetu sote kuzilinda na kuziendeleza. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza Wananchi na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili kwa kukubali mabadiliko ya kisiasa na mfumo mpya wa uendeshaji Baraza letu. Ni matumaini yangu kuwa tutajadiliana kwa hoja na si kwa jazba ili kuisaidia Serikali yetu kwa kuwajali zaidi wananchi wetu.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeonyesha mfano bora wa kuratibu na kusimamia kura ya maoni iliyofanyika mwezi Julai 2010 ambayo imeleta muundo mpya wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Hivyo, tunawashukuru wananchi wote kwa kushiriki kikamilifu katika kura ya maoni na Uchaguzi Mkuu kwa utulivu na maelewano makubwa. Aidha Tume iliendesha Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010 pamoja na Uchaguzi mdogo wa Udiwani kwa wadi ya Mwanyanya kwa mafanikio makubwa nawapongeza sana watu wa Mwanyanya kwa kupata diwani wao mpya..

Mhe. Spika, Kama nilivyosema awali kuwa hiki ni kikao cha kwanza cha Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ni wazi kuwa wajumbe wa Baraza lako tukufu inatubidi kujifunza kwa haraka taratibu mpya ambazo zinatawala uendeshaji wa vikao vya Baraza la Wawakilishi na Kamati zake hasa wakati huu wa Kikao cha Bajeti. Naamini kutokana na wajumbe wa Baraza kushiriki katika semina za mafunzo na kuchangia mada mbali mbali zilizowasilishwa katika semina hizo elekezi, sina shaka taratibu zitafuatwa ili kupata mijadala yenye ufanisi na tija.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa imeweka mkazo katika usimamizi mzuri wa mapato ya Serikali, utunzaji na utumiaji mzuri wa rasilimali, nidhamu ya kazi, na uwajibikaji kwa viongozi, watendaji na watumishi wa Serikali. Katika kufikia azma hii ni lazima sasa wote Tubadilike kwa kuweka maslahi ya Taifa letu na wananchi mbele badala ya kuendekeza maslahi yetu binafsi, ambayo hayawasaidii wananchi wetu.

Mhe. Spika, Lazima pia Viongozi na watendaji wa Wizara, Idara, Mikoa, Wilaya, Shehia na Taasisi za Serikali zinazojitegemea wawajibike ipasavyo ili kuongeza ufanisi katika shughuli za Serikali. Aidha, nawaomba wananchi kuunga mkono jitihada za Rais wetu za kuleta na kurejesha ari na moyo wa kujitolea katika kujenga Nchi yetu. Huo ni wajibu wetu sote na hatuna budi kuuendeleza.

Hali ya Siasa

Mhe. Spika, Kwa sasa nchi yetu ipo katika utulivu mkubwa na umoja ambao chanzo chake kinatokana na maridhiano yaliyofikiwa na vyama vyetu viwili vya CCM na CUF. Hali hiyo imejenga utamaduni wa kuvumiliana kisiasa. Hatua hii pia imejenga sura ya Zanzibar mpya yenye umoja, maendeleo na matumaini mapya.

Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba imejenga mazingira mazuri ya mashirikiano baina ya viongozi na wananchi na kila moja wetu kuweka mbele maslahi ya Taifa letu jambo ambalo limetuwezesha kufanyakazi kwa pamoja katika nchi yetu. Jitahada zetu hizi zinapongezwa na Jumuiya za Kimataifa na Washirika wetu wa Maendeleo. Hivyo, hatuna budi kuendelea na juhudi zetu.

Mhe. Spika, Katika hali hii ya sasa ya maelewano na mashirikiano, inatuweka mahali pazuri pa kuweza kupiga hatua kubwa kimaendeleo, kwani inaruhusu uwekezaji, biashara na kutoa nafasi kwa wananchi kufanya shughuli zao kwa ufanisi na tija. Hatuna budi kuipongeza sana Serikali yetu na Taasisi zake na zaidi wananchi na wakaazi wote wa Unguja na Pemba kwa kusahau tofauti zao za kisiasa.

Kuimarisha Muungano

Mhe. Spika, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni urithi wa Taifa letu, hivyo hatuna budi kuuenzi, kuulinda na kuuimarisha kwa maslahi ya pande zote mbili za Muungano. Serikali yetu ya Awamu ya Saba itasimamia na kuheshimu yale yote yaloainishwa katika Katiba zetu mbili, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na Katiba ya Zanzibar ya 1984, ambayo imefanyiwa marekebisho kuoanisha na mabadiliko yaliyotokea katika nchi yetu kufuatana na muundo wa Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar napenda kuchukua fursa hii kupitia Baraza lako Tukufu kumpongeza aliekuwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambae kwa sasa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa usimamizi wake mzuri na mahiri katika vikao vya Kamati ya pamoja vinavyohusiana na Kero za Muungano.

Katika kipindi chake cha Uenyekiti wa Kamati hii ameweza kufanikisha mambo mengi ambayo kwa sasa sio kero tena. Aidha, Mheshimiwa Shein amejenga misingi madhubuti juu ya namna ya kuendeleza mazungumzo na kuzipatia ufumbuzi kero zilizopo na zitakazojitokeza. Vile vile, napenda kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa nia yake thabit na kuunga mkono jitihada za

kuondoa kero za Muungano pamoja na kuimarisha Muungano wetu. Tunamuombea mafanikio makubwa katika uongozi wake.

Mhe. Spika, Napenda kulihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba chini ya Ofisi yangu tutaendelea kufuata nyayo za Rais wetu mpendwa Mhe. Dkt Ali Mohamed Shein katika kuviendesha na kusimamia vikao hivyo vya kero za Muungano kwa lengo la kuimarisha Muungano wetu wenye maslahi kwa Pande zote mbili za Muungano.

Mhe. Spika, Nafuraha kusema kwamba yapo maeneo ambayo yameshapata ufumbuzi kwa kuchukuliwa hatua nzuri za utekelezaji kupitia Kamati ya Pamoja ya kushughulikia kero za muungano. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

a) Suala la utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binadamu Zanzibar limepatiwa ufumbuzi kwani Sheria ya Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora imefanyiwa marekebisho. Sasa Tume ya Haki za Binaadamu inafanya kazi pande zote mbili za Muungano.

b) Suala la malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili pia limepatiwa ufumbuzi. Bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha taratibu zote za kiforodha kupitia kituo chochote rasmi cha Forodha zitahesabiwa kuwa zimeingizwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na hazipaswi kulipiwa kodi mara mbili. Katika kuhakikisha kuwa tatizo hilo halijitokezi tena, Mamlaka ya Mapato Tanzania itachukua hatua za kinidhamu kwa watendaji wanaotumia vibaya fursa ya ukadiriaji wa thamani za bidhaa.

c) Suala la mgawanyo wa mapato yanayotokana na misaada kutoka nje ya nchi pia limeshughulikiwa. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inapata asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti. Aidha, katika mwaka wa fedha 2009/2010, SMZ imeweza kunufaika na asilimia 4.5 ya mikopo ya kibajeti katika *"General Budget Support (GBS-C)"*.

Mhe. Spika, Napenda kuweka bayana kwamba, kwa kero zilizobakia za Muungano, mazungumzo yanaendelea vizuri hasa ya kisekta na yanatoa muelekeo mzuri wa kupatiwa muafaka. Kikao kijacho cha pamoja tunategemea mambo mengi yatapata ufumbuzi ili kuondoa manunguniko kutoka kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, Kuhusu mchakato wa mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mchakato huo unaendelea vizuri. Serikali zetu mbili zinashirikiana vizuri ili kuwa na utaratibu mzuri utakaosaidia mabadiliko hayo ya Katiba na kutoa haki kwa kila upande wa Muungano wetu. Hivyo, napenda kulihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba wakati ukifika wa kutoa maoni wananchi wote wa Unguja na Pemba watapata fursa ya kushiriki kutoa maoni yao kwa uhuru ili kuwezesha kufikia hatma ya kupata Katiba nzuri yenye kukidhi haja ya wananchi wetu.

Yapo mashirikiano makubwa na ya karibu baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia ya kuwatumikia vyema wananchi na kuimarisha muungano wetu. Nataka kulihakikishia Baraza lako Tukufu kuwa mashirikiano hayo yataendelezwa.

Hali ya Uchumi

Mhe. Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee ameeleza kwa kina hali ya uchumi wetu. Aidha, ameeleza kuwa ukuwaji wa uchumi wa Zanzibar ulifikia asilimia 6.5 mwaka 2010. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na Sekta ya huduma, ambayo mchango wake katika Pato la Taifa ulifikia asilimia 42.5 mwaka 2010. Pato la Mtu Binafsi kwa mwaka 2010 nalo limeongezeka na kufikia Dola za Kimarekani 561 sawa na Shs. 783,374. Hili ni ongezeko la asilimia 7.6 kutoka kiwango cha Pato la Mtu Binafsi la mwaka 2009, ambalo lilikuwa ni Dola za Kimarekani 558 sawa na Shs. 728,000. Nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kueleza kwa kina kuhusu hali ya uchumi wetu na kwa kuwasilisha vizuri Hotuba yake, niwashukuru wajumbe wote kwa kuchangia vizuri hatimae imekwisha.

Mhe. Spika, Mfumko wa bei kwa mwaka 2010 ulishuka na kufikia asilimia 6.1 ukilinganisha na mwaka 2009 ambao ulikuwa asilimia 8.9. Kushuka kwa mfumko wa bei kulichangiwa zaidi na kupungua kwa msukosuko wa fedha duniani na kushuka kwa wastani wa bei za vyakula na mafuta ya nishati.

Mhe. Spika, Kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuwapunguzia wananchi makali ya maisha, Serikali itaweka mkazo zaidi katika kuendeleza sekta za uchumi, ikiwemo miundombinu, nishati, sekta ya fedha na sekta za uzalishaji kwa kuleta mapinduzi ya kilimo, mifugo na uvuvi. Aidha, itaimarisha utoaji wa huduma za jamii, ikiwemo maji safi na salama, afya na elimu. Juhudi zaidi zitachukuliwa katika kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia mafunzo ya ujasiriamali na huduma za mikopo nafuu kwa mwananchi mmoja mmoja na vikundi vya ushirika.

Uwezeshaji wananchi kiuchumi
Mhe. Spika, Serikali katika mwaka 2011/2012 imejipanga katika kuandaa na kutekeleza miradi na programu mbalimbali za kuwawezesha wananchi kiuchumi hasa kwa makundi ya wanawake na vijana. Elimu zaidi ya ujasiriamali itatolewa ili kuwawezesha wananchi kubuni na kuandaa miradi bora ambayo itakuwa na tija na itakayowawezesha kupata mikopo kutoka asasi mbalimbali za kifedha na mifuko iliyopo nchini. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika itaendelea kuwashajiisha wananchi kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Akiba na Mikopo *(SACCOS).* Kupitia vyama hivi vya Akiba na Mikopo, wananchi walio wengi watawezа kupata fursa za mikopo na kuwa na mitaji ya kuanzisha na kuendeleza shughuli zao za kiuchumi na hivyo kuongeza fursa za ajira kwa wananchi na kupunguza umasikini. Taarifa kamili itatolewa na Mheshimiwa Waziri husika wakati wa kuwasilisha bajeti yao.

Uimarishaji wa Sekta Binafsi
Mhe. Spika, Kwa kutambua umuhimu wa Sekta Binafsi katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano ijayo itaendelea kusaidia Sekta Binafsi kwa kufanya mageuzi mbalimbali ya kitaasisi na kisera. Vilevile, Serikali itaimarisha Baraza la Biashara ili kupanua wigo wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi *(Public - Private Partnership).* Baraza la Biashara litaendelea kuwa chombo muhimu cha majadiliano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi yenye lengo la kuimarisha mazingira ya kuendesha biashara na kuibua fursa mpya za uwekezaji.

Sekta ya Viwanda na Biashara
Mhe. Spika, Serikali ya Awamu ya Saba imo katika maandalizi makubwa ya kufufua viwanda vilivyokufa na kuanzisha viwanda vidogo vidogo na vya kati. Hatua ya awali ni kuimarisha viwanda viliopo kwa kuvipatia vifaa na wataalamu kwa kuwashirikisha wawekezaji wa ndani na wa nje kujiunga katika ubia wa kuendesha viwanda hivyo. Serikali itafanya Utafiti wa kitaalamu kufikia azma ya kukuza Sekta ya Viwanda nchini ili kuwaondolea wananchi wetu umasikini.

Sekta ya Utalii
Mhe. Spika, kama tujuavyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua mbalimbali za kuimarisha uchumi wake pamoja na kutafuta njia nyengine za kuiingizia Serikali mapato ili kuiwezesha kuendesha shughuli zake ipasavyo na kuwaondolea wananchi umasikini. Sambamba na zao la karafuu, Serikali imechukua hatua za makusudi kukuza na kuimarisha Sekta ya Utalii kwa madhumuni ya kuongeza uwezo wa kiuchumi kwa nchi yetu. Hivyo, Serikali

itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mpango Mkuu wa Utalii. Serikali kupitia Kamisheni ya Utalii itaendeleza jitihada za kuitangaza Zanzibar katika masoko mapya hasa ya Asia ili kuongeza mapato ya Utalii na kuchukua hatua za kudhibiti mianya ya upoteaji wa mapato kutoka Sekta ya Utalii.

Mhe. Spika, Napenda kutoa wito kwa Kamisheni ya Utalii na wadau wengine katika nchi yetu kuendeleza na kuimarisha Utalii wa kumbukumbu za kihistoria, Utalii wa kiutamaduni na Utalii wa ndani wenye kutunza mazingira. Aidha, kuibua maeneo mapya ya vivutio vya Utalii yakiwemo Mapango, Michezo ya asili na Matamasha kwa lengo la kuongeza idadi kubwa ya Watalii na hatimae kuongeza mapato ya Serikali.

Uimarishaji wa Miundombinu na Mawasiliano

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba itaendelea kuweka mkazo katika sekta ya miundombinu ya kiuchumi kwa kusimamia ujenzi wa barabara zinazoendelea kujengwa, na kuanzisha ujenzi wa barabara zilizosalia ambapo mkazo mkubwa utawekwa kwa barabara zinazounganisha maeneo ya kilimo na barabara kuu ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo nchini. Aidha, juhudi zaidi zitafanywa za kutafuta ufadhili katika ujenzi wa Bandari mpya katika eneo la Mpigaduri kwa ushirikiano na wadau mbali mbali ikiwemo Jumuiya za Kikanda na Kimataifa na Taasisi binafsi.

Mhe. Spika, Sekta ya mawasiliano inatoa mchango mkubwa katika kuimarisha huduma za kiuchumi na kijamii, Sekta hii hapa nchini inajumuisha utoaji wa huduma za mawasiliano kwa njia za posta na simu na huduma za teknolojia ya habari. Maendeleo ya sekta hii yanashirikisha wadau mbali mbali wakiwemo taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na Makampuni binafsi.

Mhe. Spika, Kutokana na mabadiliko ya muundo wa Serikali na muundo mpya wa Wizara ambao una lengo la kuharakisha matumizi ya teknolojia ya habari katika sekta ya umma na binafsi na kuhakikisha kwamba jamii ya Zanzibar inanufaika na maendeleo ya tekenolojia ya habari yanayotokea ulimwenguni. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano itasimamia maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(TEKNOHAMA)* na kuratibu masuala ya taasisi za mawasiliano za Serikali ya Muungano ziliopo Zanzibar. Vilevile, Serikali itahakikisha inasimamia uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano iliyo bora zaidi ikiwa ni pamoja na uwekaji wa *MKONGA* wa Kimataifa *(Fibre Optic Cable)* na kuhakikisha unafanikiwa kufanya kazi vizuri. Aidha, Serikali itaendelea kukuza rasilimali watu na kujenga uwezo katika sekta ya teknolojia ya habari na mawasiliano, kushajiisha

matumizi ya teknolojia ya habari kwa sekta za kiuchumi na kijamii na kudhibiti matumizi na utoaji wa huduma za teknolojia ya habari *(IT).*

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba inadhamiria kuboresha mitambo ya TVZ na STZ ili iende sambamba na teknolojia ya digital ifikapo mwaka 2012 pamoja na kupanua wigo wa usikivu wa matangazo yao katika ukanda wa pwani wa Afrika Mashariki. Pia, ujenzi wa studio mpya za kisasa za kurikodia michezo na muziki, kutatoa fursa kwa wasanii wetu hasa vijana kuweza kuibua vipaji vyao katika fani ya sanaa ambayo ni sehemu ya ajira.

Mhe. Spika, katika kujenga nadharia ya utawala bora na kuwapatia habari wananchi juu ya maendeleo ya serikali yao. Serikali ya awamu ya saba imeanzisha mfumo mpya wa utoaji wa habari za kiserikali kwa vyombo mbalimbali vya habari vya ndani na nje ya nchi kupitia Msemaji Mkuu wa serikali katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Aidha, habari zinazohusu majukumu ya sekta (Wizara) pamoja na Taasisi zake zitatolewa na wizara husika kwa idhini ya Waziri mwenye dhamana. Katika kutimiza azma hii, Serikali inasisitiza kuwa kila Wizara iwe na Tovuti (*Website*) yake na Afisa wa Habari na Mawasiliano *(Information and Communication Officer)* wa kutoa habari za shughuli za Wizara kwa wananchi kupitia vyombo vya habari.

Sekta za Uzalishaji

Mhe. Spika, Sekta ya Kilimo inaendelea kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu. Mchango wa Sekta ya Kilimo katika uchumi umeongezeka kutoka asilimia 30.8 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 32.8 mwaka 2010. Sekta hii pia imekuwa kwa asilimia 4.6. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na ongezeko katika sekta ya mazao na ufugaji.

Aidha, ongezeko la uelewa mzuri wa wakulima juu ya matumizi bora ya pembejeo za kilimo, ikiwemo matumizi ya matrekta, utumiaji wa mbegu bora, upandaji kwa wakati, matumizi mazuri ya mbolea, uzuiaji wadudu waharibifu na maradhi ya mimea pamoja na utunzaji bora wa mashamba. Pia, ongezeko la uzalishaji wa zao la mwani na mpira nao umechangia ukuaji wa sekta ya kilimo.

Mhe. Spika, katika kuongeza kasi ya uzalishaji katika sekta ya kilimo serikali itaendelea kusisitiza matumizi ya mbegu bora za mazao ya kilimo, na mifugo. Utumiaji wa zana bora za kilimo ikiwemo matrekta makubwa na madogo, na matumizi ya mbolea na kuboresha huduma za utibabu wa mifugo na mimea.

Vilevile, wakulima watapatiwa elimu ya uhifadhi na usarifu wa mazao ya kilimo kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno na kuwaongezea wakulima na wafugaji fursa za upatikanaji wa masoko. Serikali pia itaendelea kushajiisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika usarifu wa mazao ya kilimo

Mhe. Spika, katika kuleta mageuzi ya kilimo, kilimo cha umwagiliaji maji kitapewa mkazo wa pekee ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo na kupunguza uagizaji wa vyakula kutoka nje ya nchi. Aidha, serikali itachukua juhudi zaidi ya kuimarisha upandaji wa mikarafuu Unguja na Pemba ili kulirudisha zao hilo katika haiba yake ya mwanzo katika nchi yetu. Serikali tayari imeshaongeza bei kwa wakulima wa zao hilo kwa azma ya kuwashajiisha kuendeleza kilimo cha mikarafuu ambacho ni msingi na uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika**,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imedhamiria kuleta mageuzi katika sekta ya uvuvi. Serikali itandelea na juhudi zake za kuwapatia wavuvi zana bora ili waweze kuvua kwa tija na kupata mapato makubwa zaidi.

Aidha, serikali itashajiisha wananchi kuingia katika kazi za ufugaji wa samaki na utunzaji wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani. Vilevile, serikali itaendeleza juhudi za kushajiisha wawekezaji kutoka ndani na nje kuekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya usarifu na kuhifadhia samaki na masoko.

Sekta za Jamii

Mhe. Spika**,** serikali itaendelea na juhudi zake za kuwapatia wananchi elimu bora na yenye manufaa kwa kuweka mazingira bora ya ufundishaji na kujifunza. Pia itaimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika ufundishaji. Hii ni pamoja na kuanza utekelezaji wa mradi unaojulikana kwa jina la "21 *Century Basic Education"* ambao utatoa mafunzo kwa walimu na wanafunzi wa madarasa ya 1 hadi la 4 kwa masomo ya Hesabati, Sayansi na Lugha kwa kutumia mtandao wa Kompyuta. Mradi huu utatekelezwa kwa kushirikiana na shirika la misaada la Marekani *USAID*.

Mhe. Spika, serikali katika kuimarisha huduma za Afya kwa wananchi, inakusudia kutekeleza azma yake ya kuifanya Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja kuwa ya Rufaa pamoja na kuzipandisha daraja Hospitali za Kivunge na Makunduchi kwa Unguja na Micheweni, Vitongoji, Wete na Abdalla Mzee kwa Pemba.

Aidha, serikali itasimamia utekelezaji wa mwongozo wa uchangiaji wa huduma za afya nchini kwa nia ya kuendeleza utoaji wa huduma zilizo bora. Vilevile, serikali itaendelea kushirikiana na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi katika kuimarisha huduma bora za afya.

Mhe. Spika, suala la kuwapatia wananchi maji safi na salama ni suala muhimu sana na kero inayowaathiri wananchi wetu wengi. Serikali itatilia mkazo zaidi sekta hii kwa kuijengea uwezo zaidi Mamlaka ya Maji, uhuishaji na upanuzi wa shughuli za maji mijini na vijijini.

Aidha, mradi wa usambazaji wa maji na usafi wa Mazingira utatekeleza mpango wa kukuza maendeleo ya rasilimali maji Zanzibar. Serikali inasisitiza zaidi wananchi kutunza miundombinu ya maji na kulinda vyanzo vya maji ili kuliondoa kabisa tatizo la maji nchini. Aidha, wananchi wanaopata huduma ya maji wanahimizwa kuchangia huduma hii ili kuifanya huduma hiyo kuwa endelevu.

Matumizi ya Ardhi

Mhe. Spika**,** ardhi ni rasilimali ya msingi kwa Maendeleo ya Taifa lolote duniani. Hapa Zanzibar wananchi waliowengi wanategemea ardhi kwa kuendesha maisha yao kwa kuitumia kwa shughuli za kilimo, ufugaji na makaazi. Hivi sasa Zanzibar inakabiliwa na migogoro ya ardhi ambayo chanzo chake kikubwa ni kutokuwa na usimamizi mzuri wa sera na sheria zinazohusiana na masuala ya ardhi.

Mhe. Spika, kutokana na changamoto hii, hatuna budi kuweka utaratibu mzuri wa matumizi ya ardhi ili kuondosha migogoro isiyo ya lazima. Viongozi katika ngazi zote tunawajibu wa kuhakikisha ardhi yetu inatumiwa vizuri ili iweze kuendelea kuwa rasilimali endelevu kwa maendeleo yetu ya sasa na ya vizazi vijavyo.

Serikali itahakikisha kuwa Sera ya Matumizi ya Ardhi inakamilika na sheria zinafanyiwa mapitio ili ziendane na wakati na mpango mpya wa matumizi ya ardhi *(land use plan)* utaandaliwa.

Aidha, Serikali inatoa wito kwa viongozi katika ngazi zote kuyashughulikia matatizo ya ardhi kwa haraka iwezekanavyo na viongozi kujiepusha kuwa chanzo cha migogoro hiyo. Hatua zitachukuliwa dhidi ya viongozi au watendaji watakaosababisha migogoro ya ardhi kwa kuwanyanganya wananchi ardhi zao na kusababisha migogoro hiyo.

Masuala Mtambuka

UKIMWI

Mhe. Spika, katika harakati za kupambana na janga la UKIMWI, serikali imeendelea kuandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kupunguza kasi ya maambukizi mapya hasa kwa rika la vijana ambalo limekuwa likiathirika kwa kiasi kikubwa. Kwa sasa kiwango cha maambukizi kwa jamii nzima ni asilimia 0.6 ambapo inakadiriwa watu 7,200 wanaishi na virusi.

Hata hivyo, katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba yapo makundi maalum ambayo viwango vya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI ni zaidi ya asilimia 0.6. Makundi hayo ni pamoja na wanaotumia dawa za kulevya kwa kujidunga sindano asilimia 10.8, wanawake wanaofanya biashara ya ukahaba ni asilimia 12.3 na wanaume wanaofanya mapenzi ya jinsia moja ni asilimia 16. Wilaya zilizoathirika zaidi ni Mjini, Magharibi na Kati kwa Unguja ambapo kwa Pemba ni Wilaya za Chake Chake na Micheweni.

Mhe. Spika, katika kufikia azma ya kupunguza maambukizi ya UKIMWI serikali itaendelea kutoa taaluma kwa wananchi wote juu ya athari na njia za kujikinga na janga hili. Aidha, serikali itaendelea kutekeleza mikakati ya kupambana na UKIMWI ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mkakati wa pili wa kupambana na UKIMWI. Napenda kuchukua fursa hii kuiomba jamii iachane na vitendo vyote vinavyochangia katika kusambaza maradhi ya UKIMWI lakini pia kuacha kuwanyanyapaa waliokwisha athirika na ugonjwa huu. Niseme tu bado chanjo wala dawa ya kutibu ugonjwa huu haijagundulika ingawa watu wamekuwa wakisafiria kikombe cha Babu kule Loliondo lakini, ithibati ya uhakika haijapatikana kama kweli watu hao wamepona kabisa. Ni bora tujikinge kuliko kuja kutegemea tiba.

Mazingira

Mhe. Spika, tatizo la uharibifu wa mazingira limeendelea kuwa ni tatizo sugu, kwani wananchi waliowengi wamekuwa wakishiriki katika uharibifu huo kwa njia moja ama nyengine. Uharibifu huu umekuwa ukisababisha athari nyingi zikiwemo zile za mabadiliko ya hali ya hewa. Usimamizi usioridhirisha wa sheria na kanuni zinazosimamia mazingira, ukosefu wa elimu ya umuhimu na utunzaji wa mazingira pamoja na ukosefu wa ajira na nishati mbadala vimekuwa kwa kiasi kikubwa vikichochea uharibifu wa mazingira, hasa katika uchimbaji miamba kwa ajili ya utengenezaji matofali katika maeneo ya ukanda wa mashariki wa Kisiwa cha Pemba na uchimbaji wa mchanga katika maeneo mbali ya Unguja na hasa Kaskazini.

Mhe. Spika, kufuatia matatizo hayo serikali itaendelea na juhudi zake katika kutoa elimu ya mazingira ili kuwafanya wananchi kuwa na uelewa mkubwa juu ya athari za uharibifu wa mazingira. Aidha, serikali itaendelea na mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa, kuimarisha mikakati ya kusimamia sheria na kanuni za mazingira, kufanyia tathmini za kimazingira miradi yote ya maendeleo pamoja na kubuni njia za ajira na nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa mazingira.

Wito wangu kwa wananchi na sekta binafsi, muendelee kuiunga mkono serikali hasa katika kutoa elimu na kubuni ajira zenye athari ndogo kwa mazingira. Nachukua fursa hii kumpongeza tena Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa jitihada zake katika kuhimiza na kufuatilia suala la hifadhi ya mazingira hapa nchini.

Madawa ya Kulevya

Mhe. Spika, kufuatia athari inayoendelea kujitokeza kutokana na matumizi ya madawa ya kulevya hasa kwa vijana ambao ndio tegemeo na nguvu kazi ya Taifa, serikali itaendelea kutekeleza mikakati ya kuzuia uingizwaji, usambazaji na utumiaji wa madawa ya kulevya. Katika hatua za kuwarudisha katika hali nzuri vijana ambao wameathirika na madawa haya, serikali itaendelea kutoa elimu na ushauri nasaha, pamoja na kuishajiisha jamii kuanzisha vituo vya huduma za marekebisho na za malazi kwa watumiaji wa dawa za kulevya *(Sober Houses)*. Aidha, Serikali itafanya taratibu za kuifanyia marekebisho Sheria ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevya pamoja na kuandaa Sera ya Madawa ya Kulevya ya Zanzibar.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa jumuiya ya ZAYEDESA pamoja na taasisi nyingine zisizo za kiserikali kwa juhudi zake za kupambana na tatizo hili na kuwasaidia vijana walioathirika. Aidha, napenda kurudia tena kuishukuru kwa dhati Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa juhudi zake za kuhamasisha wadau mbali mbali kuungana na Serikali katika kupambana na madawa ya kulevya.

Changamoto za Kitaifa na Mikakati ya Utekelezaji

Mhe. Spika**,** tuna matatizo makubwa katika uwajibikaji, utii na nidhamu ndani ya taasisi za serikali na katika utendaji kazi kwa jumla. Katika kukabiliana na tatizo hilo Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imo mbioni kukamilisha utaratibu bora wa ajira, kufanya mapitio ya sheria za kazi na utoaji wa taaluma kwa wafanyakazi ili kuongeza uwajibikaji na kuleta ufanisi kazini. Kadhalika, serikali itatoa elimu kwa viongozi wote wa serikali wa Wizara na Idara na Mashirika ya Umma kwa kuwafanyia semina elekezi.

Mhe. Spika, tuna changamoto ya kupambana na Rushwa. Katika suala la rushwa, serikali haitakuwa na huruma wala kumuonea haya mtu wa ngazi yoyote, tutahakikisha mkondo wa sheria unachukua nafasi yake. Sote tunaelewa kuwa sheria ni msumeno, serikali haitamuonea mtu ila itaendelea kufanya wajibu wake kwa uadilifu, na kwa misingi ya Sheria na Utawala Bora. Tutahakikisha kuwa tunaziba mianya yote ya ubadhirifu na kuwaondoa mara moja wale wote wanaojihusisha na vitendo vya hujma katika utumishi wa umma.

Mhe. Spika, nchi yetu inakabiliwa na changamoto kubwa ya udhalilishaji wa kijinsia, hasa watoto na wanawake. Katika azma ya kusimamia vizuri haki za watoto na wanawake na kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia, serikali itaendelea kuhakikisha uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika sera, mipango, programu na bajeti ili kuwajengea wanawake uwezo wa kiuchumi, kijamii na kisiasa na pia kuwapa fursa pana zaidi ya uwelewa wa Sheria ili waweze kutetea haki zao.

Aidha, serikali itazipitia upya Sheria kuhusu adhabu za ubakaji, kutelekeza wanawake na watoto, kupiga na kunyanyasa ili ziende sambamba na uzito wa makosa yenyewe. Hivi sasa serikali imeanzisha kituo maalum cha mkono kwa mkono *(one-stop centre)* kilichopo Hospitali kuu ya Mnazi mmoja ili kuhakikisha masuala yote ya aina hiyo yanashughulikiwa kwa pamoja katika kituo hiki kulingana na sheria zilizopo. Nia ya serikali ni kujenga vituo vya aina hii katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Tunawasihi wananchi wakitumie kituo hiki kila inapotokea haja ya kufanya hivyo.

Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo
kwa Mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, sasa kwa ruhusa yako naomba kueleza kwa muhtasari mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2011/2012. Bajeti hii imetayarishwa kwa misingi ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Pia Bajeti hii imezingatia utekelezaji wa malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2020, Malengo ya Milenia 2015 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA II).

Mhe. Spika, vipaumbele vya MKUZA II vimeainisha vipaumbele vya sekta na kuimarisha uratibu katika sekta hizo. Msisitizo utawekwa katika kutumia kwa ufanisi rasilimali za ndani na kuratibu misaada na mikopo kutoka nje. Mkazo umekuwa katika kuimarisha mashirikiano ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi pamoja na kuendeleza na kutekeleza mageuzi ya msingi *(Core Reforms).* Eneo jengine ni kuimarishwa kwa ufuatiliaji na tathmini kutokana na uzoefu ulio patikana baada ya mapitio ya MKUZA I.

Muundo wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
Mhe. Spika, Baada ya maelezo hayo ya jumla sasa naomba kutoa maelezo yanayohusiana na Ofisi yangu katika Bajeti hii ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika muundo wake inahusisha Idara/Taasisi zifuatazo:-

i) Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

ii) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

iii) Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

iv) Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali.

v) Idara ya Kukabiliana na Maafa.

vi) Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

vii) Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa.

viii) Ofisi Kuu Pemba.

ix) Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

x) Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
Mhe. Spika, jukumu kubwa la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni kusimamia na kuratibu masuala ya Kitaifa katika ngazi mbalimbami hapa Zanzibar. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni Kiungo na Mtendaji Mkuu wa shughuli zote za Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar. Majukumu Mahususi ya Ofisi hii ni kama ifuatavyo:-

i) Kuratibu Shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na za Muungano, ikiwemo Miradi ya Muungano ndani ya SMZ.

ii) Kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali.

iii) Kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. ya Chama Tawala 2010 - 2015.

iv) Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Utafiti.

v) Kusimamia shughuli za Kukabiliana na Maafa.

vi) Kusimamia Shughuli za Upigaji Chapa

vii) Kusimamia na Kuratibu Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa

viii) Kuratibu shughuli za Tume ya Uchaguzi

ix) Kuratibu Shughuli za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, Kikao cha Baraza lako Tukufu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi cha mwaka 2010/2011 kiliidhinisha matumizi ya Shs. 10,762,232,000 kwa kutekeleza malengo ya Ofisi yangu na Idara na Taasisi zake kwa matumizi ya kawaida, na hadi mwezi Machi 2011, Ofisi yangu imeingiziwa jumla ya Shs 8,323,202,575 sawa na asilimia 77 (Kiambatisho Na. 1).

Aidha, kwa upande wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Ofisi yangu iliidhinishiwa Shs. 8,351,461,038, hadi Machi 2011 imeingiziwa jumla Shs. 6,536,669,077, sawa na asilimia 78 (Kiambatisho Na. 2).

Mhe. Spika, Utekelezaji halisi wa majukumu ya Idara/Taasisi za Ofisi yangu kwa mwaka 2010/2011 na malengo ya mwaka 2011/2012 ni kama ifuatavyo:-

Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ni miongoni mwa Idara mpya yenye jukumu la kusimamia masuala ya uendeshaji wa shughuli za Ofisi pamoja na kusimamia kazi na maendeleo ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, katika Mwaka wa fedha 2011/2012 Idara inakusudia kutekeleza Malengo yafuatayo:-

(a) Kuwaendeleza wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. (Kiambatisho Na. 3).

(b) Kuongeza jengo la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hapo Vuga.

(c) Kuajiri watumishi 27 katika kada na fani mbali mbali kulingana na mahitaji.

(d) Kuanzisha mfumo wa tathmini ya utendaji kazi *(Staff performance appraisal).*

(e) Kuendeleza makaazi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kufanyia matengenezo nyumba za Dar-es-Salaam na Dodoma pamoja na kuweka samani mpya.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo hayo kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shs. 336,993,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida, kati ya hizo Shs. 130,000,000 zitatumika kwa matumizi mengineyo na Shs. 206,993,000 kwa ajili ya malipo ya Mishahara, Posho za wafanyakazi, na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF). Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shs. 75,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Spika, katika muundo mpya wa Serikali, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeongezewa jukumu la masuala ya utafiti. Idara hii kabla ilikuwa ikijulikana kama Idara ya Mipango na Sera, Majukumu makubwa ya Idara hii ni kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo, Miradi, Sera na Utafiti.

Mhe. Spika, katika mwaka wa 2010/2011, Idara hii iliidhinishiwa jumla ya Shs. 549,100,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida, malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2011 Idara imeingiziwa jumla ya Shs. 418,204,759 sawa na asilimia 76.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i) Kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria unaofadhiliwa kupitia mfuko wa *Global Fund.*

ii) Kuendeleza ukarabati wa jengo la ofisi, ya Makamu wa Pili wa Rais iliopo Vuga. Sehemu zilizofanyiwa ukarabati ni pamoja na vyoo na kupaka rangi nje na ndani ya jengo hilo.

iii) Jumla ya wafanyakazi watano (5) wamepatiwa fursa ya mafunzo ya muda mrefu katika fani za hesabu, Rasilimali watu, ufundi wa magari na ushauri nasaha katika vyuo mbali mbali Zanzibar na Tanzania Bara. Mafunzo hayo yako katika ngazi ya shahada ya kwanza, stashahada na cheti. Aidha, wafanyakazi wanne wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi (miezi 2) kwa msaada wa UNDP katika Chuo cha Mawasiliano ya Habari na Teknolojia Dar es Salaam.

iv) Idara imenunua vifaa mbali mbali kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango, Miradi ya Maendeleo na bajeti katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

b) Kuratibu matayarisho ya Sera ya Habari, Mawasilano ya Teknolojia (ICT) na Sera ya Utafiti.

c) Kwa kushirikiana na taasisi husika kuzifanyia mapitio Sheria ya Maafa na Sheria ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa.

d) Kuimarisha Sekreterieti ya Mfuko wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (ZGFCCM) ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

e) Kuimarisha Kitengo cha Habari na Teknologia (ITC) na Huduma za Tovuti (*website*) ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

f) Kuratibu maandalizi ya kuweka vipaumbele vya utafiti Zanzibar.

g) Kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia (SMT) itasimamia ufunguaji wa ofisi za Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) na Tume ya Mionzi.

h) Kwa kushirikiana na *COSTECH*, idara itaandaa semina kwa watendaji wakuu wa serikali juu ya sera na sheria za utafiti na mionzi na kuijengea uwezo kamati ya utafiti ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo hayo kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shs. 140,163,000, kati ya hizo Shs. 100,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida, Shs. 40,163,000 kwa kulipia mishahara, maposho ya wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha ina jukumu la kutoa huduma kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa Ofisi Kuu Zanzibar na Ofisi zilizopo Dar es Saalam na Dodoma.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2010/2011 Ofisi ya Faragha iliidhinishiwa Shs. 345, 699,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2011 Ofisi imeingiziwa jumla ya Shs. 240,420,590, sawa na asilimia 70. Ofisi ilitekeleza mambo yafuatayo:-

i) Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amefanya jumla ya ziara tatu (3) za nchi za nje. Nchi hizo ni Seychelles, Iran na Abudhabi. Katika ziara hizo, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alifanya mazungumzo rasmi ya Kiserikali na Viongozi wa nchi hizo. Katika mazungumzo hayo, mambo yafuatayo yalijadiliwa na kuagizwa utekelezaji wake.

Ziara ya *Seychelles*

(a) Kuanzisha usafiri wa anga na baharini kati ya Seychelles na Tanzania kwa lengo la kukuza shughuli za utalii.

(b)Ushirikiano wa kibiashara, ambapo Zanzibar itauza Seychelles matunda, mboga mboga na viungo, na Seychelles itauza mafuta Tanzania.

(c) Kushirikiana katika kupiga vita uharamia wa baharini *(piracy).*

Ziara ya Abudhabi

(d)Ujenzi wa bandari katika eneo la Mpigaduri na kiwanda cha kusindika samaki.

(e)Huduma za meli za mizigo, uchukuzi na uhifadhi wa mafuta.

(f) Uzalishaji wa umeme kwa kutumia nguvu za upepo.

(g) Uanzishwaji wa Shirika la Ndege la Zanzibar na.

(h) Masuala ya kilimo na usarifu wa mazao ya chakula.

Ziara ya Iran

(i) Kuunda kikosi cha wataalamu wa SMZ kufuatilia makubaliano yaliyofikiwa baina ya Zanzibar na Iran.

(j) Kuwashajihisha wawekezaji kutoka Iran kuja kuwekeza Zanzibar katika sekta ya Viwanda.

(k)Upanuzi wa Hospitali Kuu ya Mnazi mmoja.

(l) Ujenzi wa Kiwanda cha Boti za Uvuvi *(fibre boats)* na kusaidia wavuvi wadogo wadogo.

(m) Kujenga maabara na kusaidia madawati katika shule za Sekondari za Wilaya, Zanzibar.

(n) Iran kuisaidia Zanzibar nafasi kumi za masomo, hasa katika nyanja za Afya.

(o) Iran kuanzisha Ofisi yake ya Ubalozi mdogo hapa Zanzibar.

ii) Kupitia Ofisi ya Faragha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeratibu mazungumzo ya Makamu wa Pili wa Rais na viongozi wa nchi na Mashirika ya Kimataifa, mazungumzo ambayo tayari matokeo yake yameshaanza kuleta muelekeo wa mafanikio. Viongozi alioonana nao ni Mabalozi 27 wa nchi mbali mbali waliofika kusalimiana nae na Viongozi 5 wa Mashirika ya Kimataifa, ambayo ni *UNDP, JICA, UNESCO, USAID* na Benki ya Dunia.

iii) Jumla ya wafanyakazi watano (5) wamepatiwa mafunzo katika fani mbali mbali na viwango tofauti, kati yao wafanyakazi wawili wamemaliza mafunzo ya Cheti na Diploma katika fani ya uhudumu wa vyakula na utunzaji nyumba Katika Chuo cha Utalii Maruhubi, Wafanyakazi wawili wanaendelea na Mafunzo ya Cheti katika fani ya Vyakula na Vinywaji Katika Chuo cha Utalii Maruhubi. Aidha, mfanyakazi mmoja anaendelea na masomo ya Shahada ya kwanza katika fani ya Utawala wa Umma katika Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi ya Faragha imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuratibu ziara za kikazi za ndani na nje ya nchi za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.
b) Kufuatilia utekelezaji wa ahadi na ahadi zinazotolewa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.
c) Kukiendeleza Kitengo cha Habari cha Ofisi ya Faragha kwa kukipatia nyenzo na teknolojia ya kisasa ili kuwa na Studio kamili ya kutoa habari za Kitaifa.

Mhe. Spika, ili idara iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shs. 285,404,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shs. 130,000,000 zitatumika kwa matumizi ya kazi nyenginezo na Shs. 155,404,000 zitatumika kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ina jukumu la kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Taasisi za Muungano ziliopo Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, idara ilipangiwa kutumia jumla ya Shs. 340,448,000, na hadi kufikia Machi 2011, idara iliingiziwa Shs. 308,274,975 sawa na asilimia 91. Aidha, idara iliidhinishiwa Shs. 100,000,000 (mchango wa Serikali) kwa matumizi ya kazi za maendeleo ambazo zimeingizwa kwa asilimia 100, Vile vile kwa upande wa wahisani iliidhinishiwa Shs. 1,515,726,128 na hadi mwezi Machi, 2011 fedha zilizoingizwa ni Shs. 1,515,726,128 sawa na asilimia 100.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali imeweza kutekeleza yafuatayo:-

a) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 - 2010.

b) Kuratibu Vikao vya Makatibu Wakuu na Mawaziri wa SMT na SMZ vilivyojadili utekelezaji wa changamoto za Muungano.

c) Kuratibu kikao cha mashirikiano kwa Taasisi za Muungano ziliopo Zanzibar kilichofanyika Disemba, 2010 katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Tayari muongozo wa kuratibu vikao hivyo umeshaandaliwa.

d) Idara imeshiriki vikao kumi (10) vya sekta mbali mbali za SMT na SMZ ikiwa ni hatua za kuzipatia ufumbuzi changamoto za Muungano.

e) Jumla ya vibali vya utafiti 51 vilitolewa, kati ya hivyo vibali 30 vya masuala ya elimu, 15 mambo ya bahari na 6 mambo ya afya.

f) Jumla ya malalamiko 39 yamepokelewa, yakiwemo Ardhi 27, Ajira 1, Fidia 4, Makaazi 4, Kazi 2 na Kisheria 1. Malalamiko hayo yanaendelea kufanyiwa kazi.

g) Idara imeshiriki vikao vitatu vya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

h) Idara imesimamia utekelezaji wa jumla ya miradi 104 Unguja na Pemba **(Kiambatisho No. 4A na 4B).**

Mhe. Spika, katika mwaka wa 2011/2012 Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuratibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015.

b) Kufuatilia ziara za Makamu wa Pili wa Rais.

c) Kufuatilia utekelezaji wa ahadi za viongozi wa kitaifa.

d) Kuratibu malalamiko ya wananchi.

e) Kuandaa utaratibu wa kukusanya na kutayarisha taaarifa za utekelezaji wa kila wizara.

f) Kuratibu vikao vya pamoja vya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

g) Kuratibu vikao vya Mashirikiano kati ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

h) Kuratibu na kufuatilia shughuli za maendeleo ya miradi ya Muungano.

i) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wane (4) wa idara pamoja na vitendea kazi.

j) Kushiriki katika mikutano ya Afrika Mashariki na Kikanda.

k) Kuratibu miradi ya *TASAF III* na miradi midogo midogo ya wananchi.

Mhe. Spika, ili Idara iweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shs. 202,080,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shs. 110,000,000 zitatumika kwa matumizi mengineyo na Shs. 92,080,000 zitatumika kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Miradi ya Maendeleo ya Jamii

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, Serikali inaendelea na hatua za kuanzisha Mradi wa TASAF Awamu ya Tatu *(TASAF III)* kwa miradi inayohusu na huduma za jamii (afya, elimu, maji), pamoja na miradi ya mazingira na kiuchumi. Hatua zinaendelea za kufanya Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya *TASAF II* ili kupima mchango wake kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi wetu. Aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuanzia mwaka wa fedha wa 2011/2012 itaratibu utoaji wa fedha za miradi midogo midogo ya wananchi katika majimbo yote 50 ya uchanguzi, ikiwa pamoja na kutayarisha Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(CDF).*

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shs. 590,000,000 kwa kazi za maendeleo, ikiwa ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi kwa Programu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* na miradi midogo midogo ya wananchi. Mchango wa wahisani kwa sasa haujajulikana mpaka itakapoanza *TASAF* awamu ya III.

IDARA YA KUKABILIANA NA MAAFA

Mhe. Spika, Idara ya Kukabiliana na Maafa ilianzishwa mwaka 2006 ikiwa na jukumu kuu la Kuratibu Masuala ya Maafa hapa Zanzibar. Kama ilivyoelezwa katika Sheria namba 2 ya mwaka 2003 ya Kusimamia Maafa.

Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Idara hii iliidhinishiwa Shs. 198,586,000. Hadi kufikia Machi, 2011 Idara imeiingiziwa jumla ya Shs. 85,196,863 sawa na asilimia 43.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, Idara ya Kukabiliana na Maafa imetekeleza malengo yafuatayo:

a) Kutoa Mafunzo ya Kukabiliana na Maafa kwa Wananchi.

Idara imetoa mafunzo ya kukabiliana na maafa kwa Shehia 50 (30 Unguja, 20 Pemba) na jumla ya wananchi 1,500 (wanawake 845, wanaume 655) walishiriki katika mafunzo hayo. **(Kiambatisho Na. 5).** Katika kuadhimisha siku ya Maafa Duniani pia mafunzo yametolewa kwa wanafunzi 100 wa Vyuo vya Elimu ya Juu hapa Zanzibar. Aidha, elimu ya kukabiliana na maafa ilitolewa kupitia vyombo vya habari. Idara imeanzisha vikao vya Kitaifa vya majadiliano *(National Platform for Disaster Risk Reduction)* kwa kuwashirikisha wadau mbali mbali kujadili masuala ya kukabiliana na maafa.

b) Uandaaji wa Sera ya Kukabiliana na Maafa.

Rasimu ya Sera ya Kukabiliana na Maafa imeandaliwa, na kujadiliwa na Kamati ya Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na hivi karibuni Rasimu ya sera hiyo itawasilishwa katika Kikao cha Baraza la Mapinduzi. Aidha, Idara imeendelea na mchakato wa kukamilisha uundaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa pamoja na Mkakati wa

Mawasiliano wakati wa Maafa ambayo itasaidia utekelezaji wa Sera hiyo

c) Kutoa Mafunzo kwa Wafanyakazi .

Idara imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wawili. mfanyakazi mmoja tayari amemaliza mafunzo ya stashahada ya usimamizi wa raslimali watu na mfanyakazi mwengine anaendelea na masomo ya Shahada ya Kwanza ya Sheria. Vile vile Idara imetoa mafunzo mafupi kwa wafanyakazi wake juu ya matumizi ya*"radio calls"* wakati wa dharura, mipango ya dharura *(contingency planning)* na elimu ya Afya na Mazingira

d) Kuanzisha Kitengo cha Kuratibu Hali ya Dharura.

Idara imeunda Kitengo cha Kuratibu Hali ya Dharura nchini katika kufanya kazi zake za kupokea taarifa kuhusiana na matokeo ya maafa kutoka sehemu husika. Kitengo kimepatiwa vifaa vya aina mbali mbali ikiwemo, mitambo ya mawasiliano ya simu za masafa marefu na mafupi *(VHF na HF),* ambayo imefungwa katika Ofisi za Wilaya ya Kaskazini A, Kusini Unguja, Micheweni Pemba na Ofisi za Idara ya kukabiliana na maafa Migombani na Chake Chake Pemba.

e) Kuratibu Shughuli za Maafa.

Idara imeweza kuratibu matukio ya majanga mbali mbali ikiwemo kufanya tathmini ya athari ya upepo mkali uliotokea mwezi Febuari 2011 katika Wilaya za Mjini, Magharibi na Wilaya ya Kati Unguja, kufanya tathmini pamoja na kusaidia wahanga wa janga la Moto lililotokea katika Kijiji cha Pwani Mchangani Unguja.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012, Idara imepanga kutekeleza malengo kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

 Kujikinga na Maafa

- Idara itaendelea kushirikiana na sekta nyengine muhimu katika kukabiliana na maafa. Hii itajumuisha sekta za kiserikali, Taasisi za kiraia pamoja na mashirika ya ndani na nje ya nchi.

- Kuifanyia mapitio Sheria Nam. 2 ya mwaka 2003 ya kukabiliana na maafa.

- Kuendelea kutoa mafunzo ya kukabiliana na maafa kwa Shehia 50 za Unguja na Pemba.

- Kuandaa mipango ya kukabiliana na maafa kwa Wilaya 5 *(District Emergency Preparedness Plans)* Unguja na Pemba.

- Kutoa elimu ya kukabiliana na maafa kupitia vyombo vya habari.

- Kuandaa mfumo wa kuweka takwimu *(Database)* unaoonesha aina ya vifaa vya kukabiliana na maafa vilivyopo katika taasisi mbalimbali nchini.

Kukabiliana na Maafa

- Kutafuta vifaa vya kutumika wakati wa kukabiliana na maafa katika makaazi ya dharura.

- Kuandaa taratibu za kuanzisha na kusimamia Mfuko wa Taifa wa Kukabiliana na Maafa.

Kurudisha Hali Baada ya Maafa

- Idara itasimamia uundwaji wa kikosi kazi cha kufanya tathmini baada ya maafa kutokea kwa mujibu wa Sera na Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Maafa.

Mhe. Spika, ili Idara ya Kukabiliana na Maafa iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2011/2012 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shs. 148,413,000 kwa ajili matumizi ya kawaida. Kati ya hizo Shs. 100,000,000 kwa matumizi ya kazi nyenginezo na Shs. 48,413,000 kwa ajili ya malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

IDARA YA MPIGA CHAPA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, kufuatia mabadiliko ya muundo wa Serikali baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ilihamishiwa rasmi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kama tujuavyo Kiwanda cha Upigaji Chapa kwa muda mrefu kipo pahala ambapo panajaa maji na kinashindwa kufanya kazi zake ipasavyo. Aidha, mitambo ya Kiwanda hicho ni michakavu na haipo katika viwango vinavyokubalika katika mfumo wa sasa.

Hivyo, Serikali imekusudia kukihamishia kiwanda hicho katika majengo ya kilichokuwa Kiwanda cha Sigara Maruhubi. Sambamba na juhudi hizo, Serikali pia itaendelea kutafuta Washirika wa Maendeleo katika kusaidia upatikanaji wa mitambo ya kisasa kwa ajili ya Kiwanda hicho. Pia, Serikali kupitia Idara ya Mpiga Chapa Mkuu inaandaa mkakati wa ufufuaji wa Bohari yake Kuu ya vifaa mbali mbali vya matumizi ya maofisini. Hivyo, Serikali inaagiza taasisi zake kuitumia bohari hiyo kwa ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa matumizi ya wizara wakati itakapokuwa tayari.

Mhe. Spika, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011 iliidhinishiwa Jumla ya Shs. 381,847,000 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2011 Idara imeingiziwa jumla ya Shs. 273,494,332 sawa na asilimia 72. Vile vile Idara iliidhinishiwa jumla ya Shs. 220,000,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2011 Idara imeingiziwa Shs. 90,000,000 sawa na asilimia 41. Aidha, Idara ilipangiwa kuchangia Shs. 136,604,000 katika Mfuko Mkuu wa Serikali na hadi kufikia Machi, 2011 Idara imechangia Shs. 14,509,700 sawa na asilimia 10 ya makadirio.

Mhe. Spika, Idara hii kwa mwaka 2010/2011 imeweza kutekeleza malengo yafuatayo:

a) Jumla ya Wafanyakazi 16 wamepatiwa nafasi za mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika ngazi ya cheti na elimu ya juu.

b) Idara inaendelea kutoa huduma ya machapisho mbali mbali yakiwemo, Sheria, Katiba, Vyeti vya kuzaliwa, kazi za Uchaguzi, Hotuba za Rais, Magazeti Rasmi, Kalenda, Madaftari ya Mishahara *(Salary registers)* na kazi nyenginezo za watu binafsi.

c) Idara imeufanyia matengenezo mtambo mkubwa wa Zirkon 66 kwa ajili ya kazi za uchapishaji.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara imejipangia malengo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi na kutoa mafunzo ya vitendo.

(ii) Kuendelea kuzifanyia matengenezo *machine* zilizopo ili zifanye kazi katika hali bora zaidi.

(iii)Kuendelea kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

(iv) Kurejesha huduma za Bohari kuu ya Serikali.

(v)Kukihamisha kiwanda kutoka Saateni na kufungwa katika majengo ya kilichokuwa kiwanda cha Sigara, Maruhubi.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali iweze kutekeleza majukumu yake iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shs. 391,753,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo Shs. 180,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shs. 211,753,000 kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA

Mhe. Spika, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ni mpya, ambayo imeanzishwa tarehe 24 Januari 2011 chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Idara hii haikua na bajeti na mipango ya kutekeleza kwa mwaka 2010/11. Kabla ya kuanzishwa kwa Idara hii, masuala ya Sherehe na Maadhimisho yalikuwa yanasimamiwa na Halmashauri ya Sherehe na Mapambo kwa kupitia Kamati zake mbali mbali chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Mhe. Spika, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ina jukumu la Kusimamia na Kuratibu Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, na kusimamia shughuli za Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, ikiwemo kushughulikia mazishi, hitma pamoja na kutunza kumbukumbu za viongozi hao.

Mhe. Spika, Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa yatakayosimamiwa na Idara hii ni pamoja na Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar, Sherehe za Muungano wa

Tanganyika na Zanzibar, (kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu) Siku ya Mashujaa/Karume.

Mhe. Spika, katika kipindi kifupi tokea kuanzishwa Idara hii imeweza kuratibu shughuli zifuatazo:

(a)Maadhimisho ya Siku ya Karume yaliyofanyika tarehe 7 Aprili 2011.

(b) Sherehe za miaka 47 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zilizofanyika Kitaifa hapa Zanzibar tarehe 26 Aprili 2011 kwa kushirikiana na Waziri Mkuu.

Mhe. Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Taasisi na wote wale walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha maadhimisho ya Sherehe hizo. Aidha, nachukua nafasi hii pia kuipongeza Kamati ya Sherehe na Mapambo kwa kazi nzuri ya kufanikisha sherehe za miaka 47 ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizofanyika tarehe 12 Januari 2011.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa imepanga malengo yafuatayo:-

(a) Kuandaa mazingira mazuri ya kiofisi na utendaji kazi kwa kununua vitendea kazi na kuandaa ziara za mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Kusimamia na Kuratibu Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kwa:

i) Kuandaa Kalenda za Sherehe na Maadhimisho.

ii) Kusimamia na kuratibu Sherehe za Mapinduzi, Siku ya Karume na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

iii) Kununua vifaa vipya vya sherehe.

iv) Kuandaa miongozo ya utekelezaji wa Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa.

(c) Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa kwa:

(i) Kufanya mapitio ya Sheria namba 10 ya 2002 ya Kuwaenzi Viongozi pamoja na mambo yanayohusiana na hayo

(ii) Kuanza mchakato wa kukusanya na kutunza kumbukumbu za Muasisi wa Taifa (Marehemu Mzee Abeid Amani Karume).

Mhe. Spika, kwa sasa Idara imo katika hatua ya kukamilisha Muundo wa Kamati zake za Sherehe na Maadhimisho.

Mhe. Spika, ili Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 20011/2012, tunaomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shs. 838,210,000 kwa matumizi ya kawaida, ikiwa Shs. 830,000,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shs. 8,210,000 kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi Kuu ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba inajukumu la kuratibu shughuli za Idara zote zilizochini ya Ofisi hii kwa upande wa Pemba.
Mhe. Spika, katika Kutekeleza malengo ya mwaka 2010/2011 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya Shs. 305,552,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2011 Ofisi iliingiziwa jumla ya Shs. 259,094,620 sawa na asilimia 85.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Ofisi Kuu Pemba imeweza kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuratibu na kufuatilia utendaji wa shughuli za Serikali kwa upande wa Pemba.

(ii) Kuratibu na kusimamia utoaji wa mafunzo ya kukabiliana na maafa kwa wadau walioko Pemba.

(iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya TASAF iliyoanzishwa Pemba.

(iv) Kuwaendeleza wafanyakazi tisa (9) kwa kuwapatia mafunzo katika fani mbalimbali.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

a) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali Kisiwani Pemba.

b) Kuendelea kutoa mafunzo na kusimamia shughuli za kukabiliana na maafa kwa kushirikiana na Idara ya Maafa.

c) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya *TASAF* Kisiwani Pemba.

d) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wanane (8) katika kada mbali mbali.

e) Kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi, vikiwemo vespa na *computer*.

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo hayo kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shs. 267,984,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shs. 160,000,000 ni kwa matumizi mengineyo na Shs. 107,984,000 kwa ajili ya malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

TUME YA UCHAGUZI

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ni chombo kilichoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 119(1) na Sheria Nam. 9, 1992 ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar ili kuendeleza Demokrasia kwa njia ya Uchaguzi. Tume ina majukumu yafuatayo:-

a) Usimamizi mzima wa mienendo ya jumla katika uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

b) Kukuza na kuendeleza elimu ya wapiga kura.

c) Kusimamia ukataji wa mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi Zanzibar.

d) Kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na

e) Kusimamia Kura ya Maoni

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya Shs. 695,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2011, Tume ya Uchaguzi Zanzibar iliingiziwa jumla ya Shs. 556,236,250 sawa na asilimia 80 ya makadirio.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Tume ya Uchaguzi Zanzibar ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

a) Kutoa elimu ya Wapiga Kura kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.

b) Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe na watendaji wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

c) Kukamilisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 na.

d) Kuendesha Kura ya Maoni kuhusu kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Tume ya Uchaguzi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kuwaandikisha Wazanzibari waliofikia umri wa miaka 18 na kuendelea na ambao hawamo katika daftari

b) Kuendelea kutoa elimu ya Wapiga Kura kupitia Vyombo vya Habari, Semina, Makongamano na vielelezo vyengine.

c) Kuimarisha majengo ya Ofisi za Tume ya Uchaguzi za Wilaya

d) Kutoa mafunzo kwa Makamishna na Watendaji wa Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Spika, ili Tume ya Uchaguzi iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shs. 761,000,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shs. 220,000,000 zitatumika kwa matumizi mengineyo na Shs. 541,000,000 kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

OFISI YA BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi Zanzibar limeundwa kwa maelekezo ya kifungu cha 63 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 na Majukumu yake ya msingi yanatajwa kwenye Kifungu cha 88 (1) cha Katiba kuwa ni:- Kutunga Sheria; Kujadili Shughuli za wizara wakati wa Mkutano wa Bajeti; Kuiuliza Maswali Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na Kuidhinisha na Kusimamia Mipango ya Serikali.

Mhe. Spika, ili kuyatekeleza malengo ya mwaka 2010/2011, Baraza liliomba kuidhinishiwa jumla ya Shs. 7,946,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2011, Jumla ya Shs. 6,182,280,186 zilikuwa zimeingizwa sawa na asilimia 78. Aidha, Baraza liliidhinishiwa jumla ya Shs. 50 milioni ikiwa ni mchango wa SMZ kwa ajili ya kazi za maendeleo na zimeingizwa kwa asilimia 100 ya makadirio. Vile vile Baraza liliidhinishiwa jumla ya Shs. 525,796,910 mchango wa wahisani na hadi kufikia Machi, 2011 jumla ya shs. 405, 813,000 zimeinginzwa sawa na asilimia 77 ya makadirio.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i) Kutunga sheria.

ii) Kufuatilia Utendaji wa Shughuli za Serikali.

iii) Kujadili Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2010/2011.

iv) Kuwapatia Mafunzo Wajumbe na Wafanyakazi wa Ofisi ya Baraza.

v) Kusimamia ujenzi wa nyumba ya Makaazi Rasmi ya Spika na

vi) Kuimarisha Kitengo cha Hansard.

Mhe. Spika, katika mwaka wa 2010/2011, Baraza lilitekeleza malengo yake kama ifuatavyo: Jumla ya Miswada Kumi (10) ya Sheria ilipitishwa kama inavyoonekana kwenye **(Kiambatisho Na. 6)** Vilevile, Baraza lilijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na kuidhinisha matumizi ya Shs. 444,634,206,000.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Baraza liliendelea kufuatilia utendaji wa shughuli za Serikali kwa kuzitumia Kamati zake za Kudumu na kupitia maswali ya Wajumbe. Kamati za Baraza zilifanya kazi za kuchunguza utendaji kazi wa Taasisi za Serikali kwa utaratibu wa kawaida na kuwasilisha Ripoti za Kazi zao kwenye Mkutano wa Tatu wa Baraza la nane, uliofanyika kuanzia tarehe 23 Machi mpaka tarehe 1 Aprili 2011.

Mhe. Spika, jumla ya maswali 241 yaliulizwa na Wajumbe na kujibiwa na Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndani ya Baraza.

Mhe. Spika, pamoja na kazi hizo, Baraza lilitekeleza kazi mbali mbali zikiwemo:

- Kupokea Hotuba ya Rais ya kuvunja Baraza la Saba.
- Kupokea Hotuba ya Rais ya Uzinduzi wa Baraza Jipya (Baraza la Nane).
- Kujadili Hotuba ya Uzinduzi wa Baraza.
- Kufanya Uchaguzi wa Spika.
- Kufanya Uchaguzi wa Wajumbe watano (5) wa Baraza wa kuingia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Kufanya Uchaguzi wa Naibu Spika, Uchaguzi wa Wenyeviti wa Baraza na Uchaguzi wa Wajumbe watatu (3) wa Tume ya Bajeti.

  Kupokea na kujadili ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2008/2009 na kujadili Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza lilijiwekea lengo la kuwapatia mafunzo Wajumbe pamoja na watendaji wake kwa kusaidiana na washirika wa Maendeleo, Wajumbe. Wajumbe wa Baraza walipatiwa mafunzo ya awali, baada ya uzinduzi wa Baraza jipya uliofanyika tarehe 10 Novemba 2010, Mafunzo hayo yalifanyika kwa njia ya semina na yalidhaminiwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*United Nations Development Ptogramme – UNDP)*. Kwa upande mwengine Baraza liliendelea na mpango wake wa kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake ili kukuza uwezo wao wa kazi na kuongeza ufanisi. Jumla ya wafanyakazi (5) walipatia udhamini wa mafunzo ya muda mrefu7 katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 katika taasisi mbali mbali za elimu ndani na nje ya nchi. Idadi hiyo inafanya jumla ya wafanyakazi 14 walioko masomoni, kwa kujumuisha na wafanyakazi tisa (9) ambao walikuwa wanaendelea na masomo yao.

Mhe. Spika, vile vile katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Ofisi ya Baraza iliendelea kusimamia Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Baraza la Wawakilishi) Chukwani na Nyumba ya Makaazi Rasmi ya Spika wa Baraza. Ujenzi wa Jengo la Baraza umekamilika na jengo hilo lilihamiwa rasmi tarehe 5 Agosti, 2010. Kwa niaba ya serikali tunawashukuru wote waliofanikisha ujenzi huo, hasa Mfadhili wa Ujenzi huo Sheikh Abdallah Mohammed Al-Youseif na

Taasisi yake ya *Al-Youseif Charritable Society* ya Saudi Arabia. Aidha, tunauthamini mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) kwa kufanikisha ujenzi huo, pamoja na Taasisi za Serikali na zisizo za serikali tulizoshirikiana nazo katika kazi hiyo. Ujenzi wa nyumba ya Makaazi Rasmi ya Spika unakaribia kukamilika.

Mhe. Spika, **k**atika kuimarisha Kitengo cha Hansard. Ofisi inagharamia masomo ya watumishi sita (6) wa kitengo hicho ambao wanaendelea na masomo ndani na nje ya nchi. Vile vile, Ofisi ya Baraza imenunua Mtambo wa kukatia karatasi kwa msaada wa *UNDP*, kwa madhumuni ya kurahisisha utoaji wa vitabu vya Taarifa Rasmi za Baraza (*Hansard*). Mtambo huo ulinunuliwa kwa fedha za Mradi wa Kukuza Demokrasia Tanzania *(DDTP)* ambao ulimalizika rasmi mwezi Disemba, 2010.

Mhe. Spika, **b**aada ya kumalizika mradi huo, Ofisi ya Baraza ilitarajiwa kutekeleza Mradi mpya wa Kukuza Uwezo wa Mabunge Tanzania *(Parliamentary Support Program of Tanzania - PSPT)* kwa msaada wa *UNDP* kuanzia Februari, 2010. Lakini mradi huo haukuanza kutokana na sababu za kiutawala za wafadhili wenyewe. Hata hivyo, katika mwezi wa Novemba, 2010, *UNDP* na SMZ zilitoa fedha kwa ajili ya mafunzo ya awali kwa Wajumbe wa Baraza Jipya ambalo liliingia baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010. Mafunzo hayo yalilenga Wajumbe wa Baraza Jipya kukabiliana na shughuli za Baraza. Jumla ya shilingi 72,223,000 zilitolewa na *UNDP* kugharamia mafunzo hayo. Utekelezaji wa Mradi wa *PST* unatarajiwa kutekelezwa kuanzia Julai, 2011.

Mhe. Spika, katika kuimarisha uhusiano wa kimataifa, Baraza liliendelea kushiriki kwenye mikutano ya Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Wajumbe wawili (2) walishiriki Mkutano wa Ulimwengu wa Jumuiya hiyo uliofanyika Kenya Julai 2010, Wajumbe watatu walihudhuria Mkutano wa Kanda ya Afrika ya Jumuiya hiyo uliofanyika Mpumalanga nchini Afrika ya Kusini Agosti, 2010 na Watendaji watatu (3) wa Baraza walihudhuria Mkutano wa Jumuiya ya Makatibu Mezani uliofanyika Accra Ghana mwezi wa Aprili, 2011. Vile vile, Wajumbe wanne (4) walihudhuria mafunzo kwa njia ya semina zilizoandaliwa na Mabunge ya *CPA* yaliyofanyika Canada na Uingereza.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza lilipata heshima ya kutembelewa na wageni mbali mbali wakiwemo:- Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Ujumbe wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Sweden wanaosaidia Tanzania *(Uniform Tanzania)*, Wabunge watatu (3) wa Bunge la Africa, Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Ulaya, Mwakilishi wa Jumuiya ya Ulaya Tanzania, Wabunge wa Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika, Msajili wa

Vyama vya Siasa Tanzania, Wajumbe wa Kamati Tendaji ya *CPA* Kanda ya Afrika. Ujumbe wa Tume ya Utumishi ya Bunge la Uganda, na Wanafunzi wa Mataifa mbali mbali kwa ajili ya mafunzo ya Unadhimu na Ukamanda kutoka Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi, Arusha.

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Baraza la Wawakilishi linakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

i) Kutunga sheria kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

ii) Kufuatilia utendaji wa Taasisi za Serikali.
iii) Kujadili Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012.

iv) Kuendeleza Ushirikiano na Mabunge ya Jumuiya ya Madola na Mabunge Mengine.

v) Kuwapatia Wajumbe mafunzo kuhusu shughuli zao za kibunge
vi) Kuimarisha Utoaji wa Taarifa za Baraza kwa Umma na kuzifanya huduma za Baraza kuwa bora zaidi.

Tunakusudia Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti kuwapatia majoho kama ilivyo katika Bunge.

Mhe. Spika, ili kuyatimiza malengo hayo kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 9,129,925,000 kwa matumizi ya kawaida, kati ya hizo shilingi 4,500,000,000 kwa matumizi mengineyo na shilingi 4,629,925,000 kwa malipo ya mishahara, posho kwa wafanyakazi na stahiki za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kabla sijamalizia hotuba yangu, napenda nikushukuru tena wewe binafsi kwa namna ulivyosimamia uwasilishaji wa taarifa ya ofisi yangu. Aidha, pia nawashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa utulivu wao mkubwa katika kuisikiliza taarifa ya utekelezaji wa malengo ya mwaka 2010/2011 pamoja na mipango ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitowashukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Mhe. Mohammed Aboud). Pia niwashukuru na kuwapongeza watendaji wangu wote, akiwemo Katibu Mkuu, (Dkt. Gharib Salum Moh'd); Naibu Katibu Mkuu, (Ndugu Said Shaaban); Afisa Mdhamini, (Ndugu Amran) na Wakurugenzi wa idara mbali mbali na

Watumishi wote kwa mashirikiano yao makubwa wanayonipa ambayo yamekuwa chachu ya mafanikio ya ofisi yetu na pia kuwa kunisaidia kuiandaa hotuba hii, nawaambia nawashukuru sana.

Mhe. Spika, pia nashukuru sana kwa mashirikiano na michango ya Kamati za Baraza lako Tukufu iliyopelekea utayarishaji wa hotuba hii. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Washirika wa Maendeleo *(Development Partners)* na Nchi Marafiki kwa misaada yao katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya ofisi yangu katika kipindi cha mwaka 2010/2011, miongoni mwao ni: *AL-Yousef Foundation*, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *BADEA*, *Clinton Foundation*, China, Denmark, *FAO*, Finland, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, India, Japan, Marekani, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu, Malaria na UKIMWI, Oman, *UNAIDS*, *USAID*, *UNDP*, *UNICEF*, *UNFPA*, *WHO*, *WFP*, na *WIPO*. Vilevile, nawashukuru sana Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mashirikiano ya karibu sana na ofisi yangu. Pia nazishukuru taasisi zisizo za kiserikali kama *ZAYEDESA*, Jumuiya ya Wafanya biashara, Wenye Viwanda na Wakulima kwa kuendelea kuisaidia serikali katika kutoa huduma za jamii na kuiletea maendeleo nchi yetu. Nawashukuru wananchi wote ambao wamefuatilia na kusikiliza hotuba yangu hii.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba sana Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 12,501,925,000 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake ikiwemu Tume ya Uchaguzi na Baraza la Wawakilishi. Kati ya fedha hizo, shilingi 6,460,000,000 kwa matumizi mengineyo na shilingi 6,041,925,000 kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii **(Kiambatisho Na. 7).**

Aidha, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 715,000,000 kwa Kazi za Maendeleo ikiwa ni fedha kutoka serikalini **(Kiambatisho Na. 8).** Mchanganuo halisi ni kama ifuatavyo:-

- Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - 3,326,000,000
- Ofisi ya Baraza la Wawakilishi - 9,129,925,000
- Tume ya Uchaguzi - 761,000,000

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kuwasilisha vyema Hotuba ya Bajeti ya Ofisi yako pamoja na taasisi zake. Umetumia muda wa saa mona na nusu barabara nakushukuru sana na wajumbe wamesimama kuashiria kuunga mkono hoja hii ambayo ni kwamba sasa hivi

inaweza kujadiliwa. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kuwashukuru tena hasa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wote wa ofisi yako na taasisi zilizo chini ya ofisi yako kwa kazi nzuri ya kukusaidia kutayarisha hotuba hii.

Waheshimiwa Wajumbe sasa hoja ijadiliwe na kwa maana hiyo basi, nimkaribishe kwa nafasi ya kwanza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ali Salum Haji (Kny: Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Shughuli za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kabla sijasoma taarifa hii kwa ruhusa yako naomba nitoe neno dogo la shukurani. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na uhai kwa kuweza kusimama hapa, lakini pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa umahiri na utendaji wako bora katika kusimamia Baraza hili tukufu.

Pia Mhe. Spika, naomba niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani kwa mashirikiano wanayonipa katika utendaji wangu wa kazi za kila siku.
Mhe. Spika, sasa kwa ruhusa yako naomba kusoma taarifa ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa kwa mara nyengine kujadili masuala muhimu ya Bajeti ya Serikali kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, ikumbukwe kwamba, hii ni mara ya kwanza tangu kumalizika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, tunakutana hapa kuijadili Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu saba. Hivyo ni vyema kwa Wajumbe wenzangu wa Baraza kuijadili bajeti hii kwa kina kwa maslahi ya wananchi wetu na kuacha utashi wa kisiasa.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii na kwa niaba ya kamati kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, maoni ya kamati ya kusumamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. kwa bajet ilyosomwa na waziri ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipomshukuru Mhe. Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kutuwasilishia mbele ya Baraza lako tukufu bajeti ya wizara yake kwa mwaka 2011/2012 kwa umahiri mkubwa bila ya hofu.

Mhe. Spika, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaiafa kwa ushirikano na umakini wao wakati wakuchambua na kuijadili Bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Naomba niwatambulishe kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
4. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mjumbe
5. Mhe. Mohammed Haji Khalid	Mjumbe
6. Mhe. Salma Mohammed Ali	Mjumbe
7. Mhe. Ussi Jecha Simai	Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni	Katibu
9. Ndg. Ramadhan Kh. Masoud	Katibu

Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Mhe Waziri katika kitabu chake cha bajeti ya mwaka uliopita na malengo ya utekelezaji wa bejeti ya mwaka 2010/2011 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2011/2012 ambapo imeelezea muundo wa wizara pamoja na vitengo vilivyomo chini yake kama hivi ifuatavyo :-

1. Idara ya Uendeshaji
2. Idara ya Mipango na Sera
3. Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali
4. Idara ya Kukabiliana na Maafa
5. Idara ya Upigaji Chapa
6. Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa
7. Ofisi ya Faragha ya Mhe Makamo wa Pili wa Rais
8. Ofisi Kuu Pemba
9. Tume ya Uchaguzi
10. Baraza la Wawakilishi la Zanzibar

Tume ya Uchaguzi

Mhe Spika, ukurasa wa 5 , kifungu cha 5 wa kitabu cha bajeti Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ameelezea jinsi Tume ya Uchaguzi ilivyofanya kazi nzuri kwa kuandaa na kusimamia kwa wakati mmoja daftari la kudumu la kupigia kura,

kuandaa kura ya maoni na pia kusimamia uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 kwa mafanikio makubwa, kwani kwa mara ya kwanza tangu kuanza mfumo wa vyama vingi hapa Zanzibar wameendesha zoezi hilo bila fujo ya aina yeyote hapa. Mhe Spika, tunawapongeza sana Tume ya Uchaguzi kwa kazi hiyo nzuri kwa hiyo, tunawaomba wananchi wote wa Zanzibar kuunga mkono jitihada za serikali kuishi kwa amani na utulivu ili ipate nafasi ya kuwaletea maendeleo.

Mhe Spika, pamoja na kazi kubwa na nzito waliyofanya Tume ya Uchaguzi, lakini bado maslahi yao ni madogo. Kwa hiyo, tunaiomba serikali inapoongeza mishahara kwa watumishi wa serikali basi wao waangaliwe kutokana na uzito wa kazi yao, ili kuendelea kulinda haki zetu wakati wa uchaguzi ujao. Pia tunaiomba serikali kwa kipindi hichi ambapo tunasubiri uchaguzi wa mwaka 2015 basi kuwapatia taaluma zaidi ili kuweza kuifanya kazi yao vizuri zaidi huko mbele tuendako.

Mhe Spika, kifungu 13.0 cha hotuba ya Mhe Makamo wa Pili kimeelezea jinsi ya serikali hii ya awamu saba kuwa imeweka mkazo wa uwajibikaji na usimamizi wa mapato, na utumiaji mzuri wa rasilimali za wananchi na nidhamu ya kazi serikalini, hili tunaliunga mkono na tunalipongeza sana, lakini bado tunahisi serikali bado inawalinda watendaji wake kutokana na muhali na kuogopa kuwajibika kwa uzembe wa watendaji wake.

Mfano mdogo tu Mhe. Spika, hivi karibuni wajumbe walipotoa maoni yao jinsi taratibu za usimamizi wa mapato na kufuata taratibu za kisheria, basi serikali ilikinga kifua hapa inaonyesha bado serikali haijakuwa tayari kusaidiwa hiyo kazi ambayo wenyewe serikali tunahisi hawaiwezi, lakini tunakuhakikishia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuko tayari kuisaidia serikali kufichua maovu yote, kwani tunajua mambo mengi kwani humu ndani mna watu wa aina mbali mbali wenye taaluma na uzoefu wa fani mbali mbali na sisi tutatumia uzoefu wetu wote kusaidia serikali kwa kila hali.

Mhe. Spika, tunaunga mkono kauli ya serikali kuwataka watendaji wake kuwajibika na kujitolea kwa moyo wao wote ili kujenga nchi yetu.

Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali

Mhe Spika, Ukurasa wa 8, kifungu 18.0 Mhe. Makamo, umeelezea nia ya Serikali ya Zanzibar kuulinda na kuudumisha Muungano wetu, hilo tunaliunga mkono kwa nguvu zetu zote mia jua ya mia, lakini hatutokuwa tayari kuona mambo ya msingi ya maslahi ya nchi yetu yakikwamishwa kwa makusudi na baadhi ya watendaji wasiotaka kutekeleza matakwa ya Muungano na sisi tukanyamaza kimya. Kwa hilo, hatuna mzaha hata kidogo, kwani wananchi

wetu ni maskini sana hali ya maisha kila siku inazidi kuwa ngumu wakati nchi yetu inazo rasilimali za kutosha kuwakomboa kwenye umaskini huo, na wametuteua sisi kuja kuwatetea maslahi yao.

Mheshimiwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunakuhakikishia tunaupenda sana Muungano wetu na yeyote atakae taka kuuvuruga basi hatutokuwa pamoja naye.

Idara ya Kubaliana na Maafa

Mhe. Spika, kamati yetu inathamini sana jitihada zinazochukuliwa na serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupitia idara hii pamoja na taasisi nyenginezo za serikali, katika kukabiliana na maafa yanayotokea katika nchi yetu. Aidha, kamati inaipongeza ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kuendelea na mchakato wa sera ya kukabiliana na maafa pamoja na mpango wa dharura wa kukabiliana na maafa na mkakati wa mawasiliano wakati wa maafa.

Mhe. Spika, kamati yetu inaamini kwamba kukamilika na kutimizwa kwa sera hii umoja na kuwepo kwa mpango wa dharura wa kukabiliana na maafa na mkakati wa mawasiliano wakati wa maafa kutaiwezesha Zanzibar kukabiliana vyema na maafa ambapo ndani ya mpango huo utaelekeza kuanzisha mfuko wa maafa ambao utakuwa ndio mfuko pekee utakaoweza kuwasaidia pale yatakapotokea maafa. Vile vile, suala la idara hii kuipatia vifaa vya kisasa vya kujikinga na kukabiliana na maafa.

Mhe. Spika, kamati kwa upande mwengine inaipongeza kwa dhati Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Maafa kwa kuweza kuzipatia shehia 135 mafunzo mbali mbali yanayohusiana na maafa. Kamati inaomba ofisi hii kuendeleza zaidi na mafunzo hayo ili suala la maafa lifahamike kila pembe ya nchi yetu. Kamati itakuwa na wizi wa fadhila isipoishukuru Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Maafa kwa kuwapatia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Mafunzo ya Mpango wa Dharura wa Kukabiliana na Maafa na Mkakati wa Mawasiliano wakati wa maafa. Kamati inaamini kwamba mafunzo tuliyoyapata yamesaidia kuwapa uelewa mkubwa na wao kuwaelimisha wananchi majimboni.

Aidha, kamati inafarajishwa na ofisi hii kuwa na lengo la kuendelea kutoa elimu ya maafa kwa umma katika ngazi mbali mbali za uongozi. Hata hivyo, kamati inaona kuna haja kwa ofisi hii kuendelea kutoa elimu hii kwa kuwaangalia wadau mbali mbali wakiwemo akinamama na watoto hususan wanafunzi wa skuli mbali mbali, ambao ndio huathiriwa zaidi pale maafa yanapotokea.

Idara ya Sherehe na Mapambo
Mhe. Spika, kamati inaipongeza Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kuweza kuratibu na kusimamia kwa mafanikio sherehe mbali mbali za kitaifa zilizofanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011. Hata hivyo, kamati yetu inaendelea kukumbushia kupunguzwa kwa gharama za kuzigharamia sherehe hizi ili kuepuka matumizi yasiyo na ulazima. Aidha, kamati inashauri serikali kutengeneza kiwanja mbadala badala ya Uwanja wa Amani kwa ajili ya kufanya sherehe hizo ili kuuwezesha uwanja huo utumike kama vile ulivyokusudiwa.

Idara ya Upigaji Chapa
Mhe Spika, kwanza tunaipongeza sana serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kuanza taratibu za kukihamisha Kiwanda cha Upigaji Chapa kwenda Maruhubi, hili linatupa faraja sana kwani wameshateseka muda mrefu kuingiliwa na maji kila siku, lakini tunaamini kwa sasa hapo walipo watafanya kazi kwa bidii zote. Lakini bado kuna Taasisi nyingi za Serikali zinadaiwa na idara hii kwa muda mrefu. Hapa tunatoa indhari kwa mawaziri wote kila wizara inayodaiwa na Kiwanda cha Upigaji Chapa basi hatutapitisha bajeti zao mpaka watuhakikishie kwamba watalipa ndani ya mwaka huu. Na hili tunaomba Waheshimiwa tuwe pamoja nalo.

Mhe. Spika, kamati vile vile katika hatua za kukithamini na kukiwezesha kiwanda hiki kufanyakazi zake, tunazitaka Taasisi zote za Serikali kupeleka kazi zao katika kiwanda hiki ili kuongeza mapato ya serikali na kuacha tabia ya kuchapa kazi za serikali nje ambapo sio jambo zuri, kwani kunaweza kuvujisha siri za serikali na kudhibiti upoteaji wa fedha za umma.

Mhe. Spika, kamati kwa upande mwengine inafurahishwa na hatua zilizochukuliwa na serikali za kuanzisha utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizokubaliwa kati ya viongozi wetu wakuu wa kitaifa na wenyeji wao huko ughaibuni. Hata hivyo, kamati inaikumbusha serikali kuifuatilia na kuifanyia kazi ahadi ya serikali ya India ya uanzishwaji wa mradi mkubwa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*ICT*) hapa Zanzibar. Suala hili lilizungumzwa wakati wa ziara wa aliyekuwa Mhe. Waziri Kiongozi wa Zanzibar, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, nchini India.

Mhe. Spika, kwa upande wa shughuli za *TASAF*, kamati inapongeza kwa dhati na jitihada zinazochukuliwa na serikali katika kuwawezesha wananchi wanaoibua miradi yao katika jamii ili wajiajiri na wapambane na umaskini. Hata hivyo, kamati imebaini kwamba miradi mingi iliyofadhiliwa na *TASAF* imeshindwa kuendelea kutokana na ukosefu wa utaalamu ndani ya vikundi kwa

ajili ya kuviendeleza vikundi hivyo mfano mzuri ni mradi wa pembejeo za kilimo, Bumbwi Sudi ulioanzishwa mwaka 2006 kwa gharama ya shilingi 10,343,000. Kamati kwa ujumla haikuridhishwa na uchanganuzi wa mapato na matumizi ya mradi ambao unaonekana kutekelezwa kwa hasara. Aidha, kamati haikuridhishwa na kiwango cha mapato yanayopatikana katika mradi huo.

Hivyo, kamati inaingiza Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kukipatia wataalamu kikundi hiki pamoja na vyenginevyo mfano wa hichi ili waweze kuchanganua shughuli zao kitaalamu, lakini pia waiendeshe miradi yao kwa faida.

Mhe. Spika, hata hivyo, kuna miradi inayofadhiliwa na *TASAF* imeonekana kuwa na mwelekeo mzuri mfano ni mradi wa ufugaji kuku wa kienyeji Bumbwisudi wenye wanachama 10 ambao kila mmoja anafuga kuku katika banda lake. Hata hivyo, kamati inatoa ushauri kwa kikundi hiki na vyenginevyo kufungua *account* ya pamoja katika Benki ya Watu wa Zanzibar kwa lengo la kujiwekea akiba lakini pia kuwawezesha kupata mikopo ya kuuendeleza mradi wao na inayofanana na hiyo.

Mbali na ufugaji wa kuku wa kienyeji, pia waangalie uwezekano wakufuga kuku wa kisasa ili kutanua biashara na kuongeza mapato.

Kamati pia inaishauri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuupatia mradi huu utaalamu wa kuendesha shughuli zao pamoja na utaalamu wa utunzaji kuku hao kuepusha hasara inayoweza kutokea. Aidha, kamati inasisitiza uanzishwaji wa polisi jamii katika shehia hiyo ili kupunguza wimbi la wizi wa kuku wa mradi huo, lililoenea na kupelekea kuwavunja moyo wanaushirika.

Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Spika, kamati inapongeza kazi zinazotekelezwa na ofisi hii katika kuratibu kwa ufanisi ziara za Makamo wa Pili wa Rais ndani na nje ya nchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, kamati inajenga matumaini juu ya ziara zinazofanywa na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais pamoja na viongozi wengine wakuu wa kitaifa kwamba zitaleta matunda yaliyokusudiwa ya kuinua ustawi wa jamii na uchumi wa Zanzibar. Aidha, kamati inafurahishwa na utaratibu wa serikali wa kuhakikisha kwamba kila kiongozi kutakiwa kuandaa ripoti baada ya kurejea safari za kikazi nchi za nje. Utaratibu huu utaisaidia serikali kuyafanyia kazi masuala yaliyojadiliwa katika ziara hizo.

Baraza la Wawakilishi

Mhe. Spika, kamati haina budi kuipongeza ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuweza kufanikisha kwa ufanisi mkubwa shughuli zake mbali mbali zikiwemo za uendeshaji wa kikao na shughuli za kamati.

Kamati inashauri kwamba, kuharakisha mchakato wa kuanzishwa kwa Mfuko wa Baraza ili Baraza lifanye kazi zake kwa ufanisi mkubwa, lakini kufikia uanzishwaji wa Mfuko huo, kuna haja kwa sheria itakayoanzisha Mfuko huo kuhakikisha kwamba utapatiwa fedha kupitia pasenteji ya makusanyo ya serikali. Na hili sio jambo jipya kwani hata jirani zetu Tanzania Bara wanafanya hivyo.

Mhe. Spika, kamati pia inaikumbusha serikali kuwashirikisha wadau mbali mbali wakiwemo wawakilishi katika maandalizi ya bajeti ya nchi. Ni vyema serikali kwanza ikaandaa mapendekezo ya serikali baadae wadau mbali mbali wakiwemo wawakilishi wa wananchi wakaipitia katika vikao vyao vya Baraza vya mwezi wa Januari ya kila mwaka. Baadae mapendekezo hayo baada ya kuchangiwa kiutaratibu yarudishwe serikalini kwa kuzingatiwa na baadae ndipo serikali iwasilishe bajeti hiyo rasmi katika Kamati za Baraza na baadae katika Mkutano wa Bajeti wa Baraza wa kila mwaka.

Mhe. Spika, utaratibu huu nao sio jambo jipya katika baadhi ya Mabunge ya Afrika. Bunge la Zambia kwa muda sasa limo katika mchakato wa kutaka kuutekeleza utaratibu huu wa kuhakikisha kwamba matayarisho ya bajeti yanawahusisha Wabunge na hata Wilaya.

Mhe. Spika, bajeti ni mali ya wananchi, hivyo ni vyema wakashirikishwa kikamilifu katika maandalizi yake**.**

Kamati kwa upande mwengine haina budi kuishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mfadhili na mjenzi wa jengo jipya la Baraza la Wawakilishi liliopo Chukwani kwa kuiwezesha Ofisi ya Baraza kuwa na jengo ambalo linaendana na shughuli za Baraza. Hata hivyo, kwa kuwa jengo hili limekabiliwa na kasoro zinazopelekea kuvuja, kamati inaona kuna haja kwa ofisi kupata ushauri wa kitaalamu ili jengo hilo lifanyiwe marekebisho kwa umakini na uhakika.

Mhe. Spika, kamati inaipongeza ofisi kwa kufanikisha uondoshwaji wa mwangi (*echo*) katika ukumbi. Hata hivyo, Ofisi ya Baraza kwa kushirikiana na serikali inahitaji kuharakisha upatikanaji wa jenereta yenye uwezo wa kutoa huduma za umeme pale unapokatika, vyenginevyo vikao vya Baraza hususan kipindi hiki cha mkutano wa Bajeti, vinaweza kuathiriwa pindi umeme ukikatika, hali ambayo inaweza ikaligharimu Baraza pamoja na serikali.

HITIMISHO:
Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichukue fursa hii tena kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya kamati naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha ahsante.

Mhe. Spika: Nashukuru Mhe. Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Waheshimiwa Wajumbe shughuli ya kujadili bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais tunategemea imalizike kesho kipindi cha jioni, hivyo niwaombe wote wale ambao wana nia ya kuchangia watume majina yao mapema, wapange *point* zao vizuri ili tuweze kufahamu namna ya kuugawa muda kuwawezesha wajumbe hao wakapata nafasi ya kuchangia. Lakini pia kutoa nafasi kwa Makamo wa Pili wa Rais na baadhi ya mawaziri ambao watapenda kumsaidia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais katika kutoa majibu kwa hoja mbali mbali.

Basi baada ya maelezo hayo sasa twende kwenye uchangiaji wa jumla.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo kuchangia asubuhi hii ya leo. Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa jitihada zako na kwa uongozi wa Baraza lako tukufu. Pili nimshukuru Mhe. Rais Dk. Ali Moh'd Shein kwa kutuchagulia Mheshimiwa wetu Makamo wa Pili, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Mhe. Rais hakukosea hata kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, dalili nzuri inaonesha leo katika hotuba yake Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ambapo ameamua kwa makusudi kusema yeye mwenyewe kutokana na hali ambayo imejawa na mambo mazuri sana ya kuwaeleza wananchi na wakayakubali. Mhe. Spika, natoa shukrani.

Mhe. Spika, niende ukurasa wa 10 kuhusu suala la malalamiko ya wafanyabiashara. Mhe. Spika, kwa kweli suala hili Waheshimiwa wetu wote wawili Makamo wa Pili wa Rais na Mhe. Waziri wamelieleza kwa fasaha nzuri sana lakini kimazingira ya utendaji mpaka leo ni magumu.

Mhe. Spika, juzi katika matembezi yangu nilitembea sehemu ya *TRA* basi niliwakuta wafanyabiashara wengi tu wamejikusanya. Mimi nikawauliza jamani mbona leo mmejikusanya hapa, wakasema leo tunakutana nao hawa watu wa *TRA*, mheshimiwa hali bado ngumu. Mmoja akaonesha risiti ambayo kalipia kule Bara, akaonesha na risiti ambayo haina tofauti na ile iliyolipiwa gari ile ile kule kule Bara . Mhe. Spika, kwa kweli hili suala nimefanya haraka tu lakini ilikuwa leo nije navyo vile vitu kwa sababu mara nyingi sana sipendi kusema bila ya *document.*

Mhe. Spika, hili suala linatisha na linasikitisha sana. Lakini mimi niseme tu hatuoni kwamba hii ni moja katika *sabotage* ambayo tunafanyiwa kuwa Zanzibar tusiwe na biashara, Zanzibar tusiinuke kiuchumi kwa kupitia wafanyabiashara. Mhe. Spika, namuomba tena Mhe. Makamo wa Pili na Mhe. Waziri hili suala tulifuatilie kwa kina kabisa tusiseme kwenye *paper*, tumeshachoka nalo kulizungumza kwenye *paper*, tuvuke maji tukaangalie.
Mhe. Spika, wafanyabiashara wanasema kheri ya hivyo bora tukafanye biashara kule kule na wakiamua hivyo hatuna uchumi tutajidanganya kwenye vitabu hivi bure. Kila siku tunasema tunaokoa uchumi tutakuwa waongo. Kwa hiyo, naomba hilo kwa kuwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ni mfuatiliaji najua atalifuatilia haraka sana.

Mhe. Spika, ukurasa wa 12 hapa namsifu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kujitahidi sana katika kujadili kuuinua uchumi kwa upande wa Zanzibar. Hili nasema nampa pongezi na kumshukuru sana.

Lakini tukija katika ukurasa wa 13 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mhe. Spika, viongozi wa fedha wanajitahidi lakini kuna mambo mengine tunayasahau katika haya mabenki. Kwa sababu mabenki wana sera zao hatuwezi kuwaingilia lakini kuna mambo ambayo tunaweza tukakubaliana nao kimsingi. Mhe. Spika, leo wanajikusanya wananchi wetu kwa njia ya kutaka kuinua uchumi, wanataka kwenda kukopa benki lakini benki sharti lao la mwanzo wanakwambia lete kitu kilichokuwa kikubwa kinachofanana na pesa yako.

Lakini tunatafuta mbinu jinsi gani ya kuweza kuwasaidia wale. Labda tungezungumza na wale mabenki kuwa waangalie katika sera zao au kama sisi tunasema wakati mwengine kanuni zimewekwa kando. Sasa na wao zile sera zao waziweke kando kuweza kuwasaidia hawa ndipo tutakapoweza kuinua uchumi. Mhe. Spika, kutakuwa adha hii ya umaskini hakuna hapa Zanzibar kama tutakwenda katika njia hizo.

Sasa na hili mimi naomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aliangalie kwa kina ili kuwawezesha hawa wananchi wetu na kuweza kujiondolea ukali wa maisha uliotuandamana kila leo. Tutafanya bajeti chungu nzima lakini bado tutaendelea pale pale.
Mhe. Spika, uimarishaji katika sekta binafsi. Mhe. Spika, hii tunaizungumza tu lakini tukiendeleza kuimarisha sekta binafsi sidhani kama tutaambiwa mshahara mdogo, hospitali hakuna dawa, kilimo hatuna matrekta, hiyo itaondoka. Ndio maana tukenda katika nchi za wenzetu wana sekta hizi za binafsi wamezipa kipaumbele.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri jana alisema kuwa sekta hizi tutazipa *power* kwa sababu fedha zao zinakuwemo ndani, lakini isiwe kwenye *paper* tu tunataka na utekelezaji. Mhe. Spika, naomba kumnukuu alisema kuwa "Sasa wawakilishi tuwaandame mawaziri katika utekelezaji". Mimi wa mwanzo nitaanza kuwaandama mawaziri sitowaachia. Alisema kwa nia nzuri tu kwa sababu kaona kasoro zilizokuwepo tunapopitisha bajeti utekelezaji wake unakuwa mdogo tunawaachia watendaji waamue wao wenyewe wanavyotaka tunakosa fedha hizi.

Mhe. Spika, nilizungumzia suala lile la mwekezaji binafsi na mengine yapo lakini hili limenikaa rohoni kwa sababu lina *mass* kubwa ya wafanyakazi ambao wananchi wetu watakwenda pale kufanya kazi si chini ya 250 serikali imeshajivua katika suala la ajira.

Mhe. Spika, lakini Mhe. Waziri amesema kuwa atalichukulia hatua na mimi naomba si vibaya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kuwa nae ni mpenzi wa kuleta maendeleo katika nchi ya Zanzibar. Kwa sababu yeye ni mwanadiplomasia katembea nchi nyingi anajua jinsi gani wenzetu wanavyoendelea. Katusifia nchi chungu nzima ameshakwenda hapa, hakwenda kuuza uzuri kule kenda kuyachukua ya kule kuyaleta hapa yafanyiwe kazi ndio maana yake. Mhe. Spika, namsifu sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tena tuko pamoja na wewe usiomuonee haya mtu tutashirikiana na wewe.

Mhe. Spika, suala la viwanda bado hatujawa tayari Zanzibar tukubaliane. Kwa sababu tuna kiwanda chetu kizuri cha sukari kile pale mpaka leo hii tukiuliza serikali imepata nini *minus zero*. Tunacheza nini joka la mdimu sisi tunakosa na wenyewe kwa wenyewe hali ngumu ndio yale sasa yanayotukuta.

Lakini Mhe. Spika, nifurahi na niisifu tume ambayo ameiunda mwenyewe Dk. Ali Moh'd Shein ikiongozwa na Mwenyekiti Kamandoo kabisa, Mheshimiwa wetu, mpendwa wetu si mwengine isipokuwa mwenyewe Mhe. Waziri wa

Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ndio Mwenyekiti wa kushughulikia kero ya kiwanda kile.

Mhe. Spika, mpaka leo hatujapata ripoti ile kiwanda kinaanza kuteketea wananchi hawana ajira. Lakini wenzetu kule Dar es Salaam wana shirika linaitwa *SIDO* ambalo linatengeneza vile viwanda vidogo vidogo. Mhe. Spika, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko hebu nendeni mkachukue *contract* nao wale watutengenezee mashine zitakazoweza kutusaidia. Kuna mashine nzuri tu za kukamua *juice* sisi tuna mapera mengi sana hapa, tuna miembe, tuna kila kitu. Mhe. Spika, hili suala tunalizungumza katika kitabu lakini uamuzi wake unakuwa ni mdogo sana.

Kwa kweli Mhe. Spika, hili suala linasikitisha sana naomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alichukulie kwa nguvu suala hili tukutane na watu wa *SIDO*. Nimeona kwenye kitabu hapa wewe mwenyewe shuhuda umekwenda kuangalia kinamama jinsi gani mafuta wanayafanya kwa njia ya mwani. Hii hapa wala haitaki tochi, hii ni mashine *local* inatumia *energy power*, namuona mama na ujiti wake sijui anatwanga twanga hapa. Sasa mashine kama hizi kama zitaletwa kwa wingi ndani ya nchi yetu hii basi Zanzibar umaskini utaondoka kwa njia ya viwanda. Si lazima mtuletee viwanda vikubwa vikubwa ni vidogo vidogo tu vitatuondolea umaskini. Sasa bado hili naomba Mhe. Spika, liangaliwe.

Mhe. Spika, nije sekta ya utalii na naomba tukubali kwamba kwa dhana ya juu juu tumeona pale tumefanikiwa kwa dhana ya ndani huko tumefeli hatuna hoteli zilizokuwa *five stars,* tuna hoteli ni vilabu tu na ndio maana zinatupa matatizo mara leo zinakufa.

Kwa mfano Mheshimiwa wewe mwenyewe umeunda Tume ya Uchunguzi wa *Venta Club* leo limebakia janga wananchi wetu wanalia pale hawajalipwa mafao yao yaani mshahara, wale waliopeleka tenda za vyakula, majengo yanateketea. Kwa kweli sekta hii tusiseme kwamba tumepata mafanikio mimi nasema hatufanikiwi jamani.

Kwa sababu hebu tuiangalie sheria yetu kama ina mapungufu basi tuirekebishe tutafute zile zenye wawekezaji ambao wana sifa za *five star*. Hazifi kwa mfano kama vile Kempinski ile hoteli inaondoka jina lile litakuja jina jengine lakini bado inafanya kazi kwa sababu ile ni ya kimataifa. Lakini ukija hizi Vera zile ni klabu lakini sisi tunaona kama hoteli zenyewe, huko kwao hazina *condition* za kuonesha kwamba ni hoteli hasa. Ndio maana utakuta wale watu wao

wanawachukua kabisa kwa sababu ni memba, wanarejesha kule kabisa hapa wanakuja na idadi yao tu na kila kitu wameshalipa kule kwao.

Mhe. Spika, halafu isitoshe sekta hii sasa hivi imekuwa Zanzibar tuna-*fight* nao hususan wale watu wa ukanda ule wa wananchi. Mhe. Spika, kuna malalamiko mengi ya wananchi wetu. Tuangalie sheria jinsi gani hawa ma-*PO*. *PO* inakwenda na wazalendo ninavyofahamu mimi, lakini ukiangalia kimandhari ya hoteli nyengine unakuta *PO* ni Mkenya unatarajia nini hapo wewe Mzanzibari.

Mhe. Spika, tumefungua vyuo tunawasomesha Wazanzibari wameshafika mpaka diploma lakini hatimaye diploma zile zinakwenda kuishia kwenye miembe. Sasa hii ningeomba tuangalie zile sheria zetu zikoje.

Mhe. Spika, mimi siku zote ninachoumia ndani ya roho kuwa najisikia kelele zangu zinaishia ndani ya ukumbi tu lakini wizara husika haifanyii kazi haiendi kuangalia kule. Nimezungumza na sehemu ya Idara ya Wafanyakazi nimekwenda nao siku moja kufanya *study* yenyewe kuangalia jinsi gani keo zinavyofanyika katika mahoteli kudhalilisha wananchi. Tulipokwenda kule tumegundua kuwa ni kweli, tukagundua mpaka Wakenya wengine hata ile *permit* yake ya kukaa imekwisha. Tumekwenda ziara hiyo mara moja tu mara ya pili naona wameingia mitini sikuwaona tena.

Leo Mhe. Spika, hoteli ya *Blue Bay* na nyenginezo unawakuta hao wameja tele, wale wenyewe wenye matunda hayo ya Mapinduzi walioukaribisha utalii hakuna nafasi hata moja. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aunde tume kwa makusudi ili awasaidie Wazanzibari kwa sababu wananyanyaswa vibaya sana. Anaye waziri wake mzuri sana tu Mhe. Moh'd Aboud Moh'd hana tatizo lolote. Mhe. Spika, Mhe. Makamo ana timu nzuri tu katika wizara yake hiyo niseme ukweli. Jamaa wananiambia ninamsifu kwa kuwa Mbunge wangu, ndio ni lazima niseme kwa nini mbunge wangu nimponde.

Mhe. Spika, naomba tukubaliane si vibaya ukasema sisi Zanzibar, sisi Bara, asilimia iliyobakia ndogo tukawapa Wakenya au wasipewe kabisa wapambe wamenambia huko. Lakini sasa hiyo hali Mhe. Spika, kama tutainyamaza kimya ile maana ya dhana ya kusema uchumi wetu kwa utalii kuwa wananchi wa Zanzibar wanufaike itakuwa haina maana.
Mhe. Spika, niingie ukurasa wa 19 sekta ya uzalishaji wa kilimo hapa wewe shahidi tuna mabonde kule yako wazi kabisa Kirombero, Pangeni hayaguswi na si kama hawataki kulima wananchi. Lakini sasa kipindi cha wakati wa kutaka

kulima ule mpunga wetu uliokuwa unatumia kwa ajili ya mvua wanaukosa kipindi kile kwa sababu hawana zile zana.

Lakini Mhe. Waziri wangu hapa alisema kwamba zana zile zitaletwa na limezungumzwa kwenye *document* hiyo sasa tunangojea utekelezaji. Mhe. Spika, tusifanye mchezo kilimo Zanzibar tunakiweza ten asana na tukiweka ghala la akiba kwa wananchi wote sasa hivi limeni mpunga halafu serikali ikenda ikanunua ikaweka ghalani utaona faida yake na utasema kweli.

Mhe. Spika, ulimaji wa mboga mboga njoo ukatazame pale Upenja. Mhe. Spika, Mhe. Rais Amani Abeid Karume alishangaa alisema kumbe Zanzibar tunaweza kutoa biringani kama kichwa changu. Akasema kwamba hawa watu lazima wawezeshwe na shahidi alikuwepo Katibu mwenyewe wa wizara hii hii yupo ataniunga mkono hivi ninavyosema na yeye mwenyewe akawa mstari wa mbele katika kuwasaidia hawa vijana kuwapelekea water pump ili wanufaike na yale maji. Lakini niseme kwa bahati mbaya wakati ule akaondoshwa maskini Katibu huyu mpaka katika ukatibu wake wewe mwenyewe namna gani suala hili atalichukulia kwa jitihada zote kwa sababu na yeye aliona vijana walivyonufaika katika miradi ile ya mboga mboga.

Mhe. Spika, suala hili linasikitisha sana na naomba kwa makusudi wajitahidi sana katika kilimo hasa katika jimbo la Mhe. Makamo wa Pili wa Rais mabonde tunayo mengi sana. Ulimaji wa mfumo wa kumwagilia maji unafaa. Mhe. Spika, Mkorea tayari sasa kilichobakia tuwanufaishe wananchi.

Mhe. Spika, ukurasa wa 21 sehemu ya uvuvi. Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Waziri, waziri mpya lakini ana mambo mapya. Hongera sana mheshimiwa. Mhe. Spika, Dk. Ali Moh'd Shein akichagua kiongozi hafumbi macho anachagua kwa uhakika akikaa na Makamo wake wote wawili. Mhe. Spika, miezi sita sijui kama imefika vizuri ameshaandaa vitu vizuri sana anawapeleka wananchi wetu China kwenda kusomea masuala ya uvuvi wa juu. Mhe. Waziri hongera sana jitahidi hivyo hivyo.

Maana yake kuna uvuvi wa baharini na uvuvi wa juu. Kwa sababu huwezi kwenda kuvua tu moja kwa moja baharini kama huna uvuvi wa juu, uvuvi wa juu ni kufuga samaki.

Mheshimiwa kaliona hili nimekaa nae mara nyingi sana, tutakufa maskini kwa uvuvi kwa sababu kule baharini kunachafuka, hebu tutafute mbinu hizi za uvuvi wa juu. Mhe. Spika,

Mhe. Spika, tatizo kubwa kwa sasa hivi linalotuandama ni suala la uvuvi haramu. Kule Kiwengwa uko mwingi sana nakuomba Mhe. Waziri ufanye ziara kwa makusudi uende kule.

Mhe. Spika, nimalizie suala la ardhi nimsifu sana Mhe. Ali Juma Shamuhuna ameshaanza kulichukulia utaratibu mzuri na shahidi mimi mwenyewe nilikuwepo nilishuhudia jinsi wananchi wenye matatizo ya ardhi alikaa nao kwa pamoja na akaamua sasa anajipanga na katika bajeti hii kanihakikishia kwamba matatizo haya yataondoka kwa awamu hadi awamu.

Mhe. Spika, la mwisho nilifikiria mimi katika hotuba hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kutakuwepo na ripoti japo ndogo ya kuhusiana na tatizo la manispaa, nimejaribu kupekua lakini halimo humu. Mhe. Spika, juzi tulisikia kwenye vyombo vya habari kuwa madiwani wameunda tume ya uchunguzi katika manispaa yao, ripoti imepelekwa wapi siwezi kujua. Sasa hili tunamuomba Mhe. Makamo japo siku ile tulimpinga lakini tunaomba radhi kwa sababu unajua wakati mwengine ile jazba ikitokezea unampinga hata mzee wako lakini baadae unasema astaghfirullah kwa Mungu wako baba nisamehe.

Lakini tulitegemea angalau rasharasha ile angetudokolea kidogo lakini humu hamna, hili nalo tusilizungimzie kwa sababu si pahala pake lipo kwenye wizara yake. Hapo kwenye wizara yake mimi nina shilingi yangu ndani ya koti, hapa sasa hivi nalipitisha kama transit tu.

Mhe. Spika, la mwisho ili niweze kuunga mkono ni suala la polisi jamii. Mhe. Spika, polisi jamii naomba tuwasifu sana. Mhe. Spika, jana nilipita sehemu moja hapa kati kati Mbarali nilikuta vijana wamejitolea na marungu yao. Mhe. Spika, nikapigwa mkono mimi nikasimamishwa, toka kwenye gari nikatoka. Kwa kweli kitendo kile kilinifurahisha lakini nikajieleza tulikuwa na kikao cha harusi sehemu ya jirani sasa nikakubaliana nae. Kwa hili naomba kwa makusudi Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ampongeze Kamishna wa Polisi kwa jitihada zake za polisi jamii.

Mhe. Spika, juzi nilitoa maajabu niliunga mkono kwa Mhe. Waziri asilimia 120 lakini leo namuunga mkono Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa asilimia mia mbili.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nianze kwa kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kwake kushika nafasi hii muhimu ya kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi mbali ya yale majukumu ya pamoja ya kuwa ni mmojawapo wa wasaidizi na washauri wakuu wa Mhe. Rais. Naamini

chini ya busara, hekima na uzoefu wake atamsaidia Mhe. Rais yeye na Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad ili kuipeleka nchi yetu kule ambako tunakusudia tufike kwenye maendeleo na ustawi.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kuungana na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kupongeza hali hii ya maridhiano ambayo imefikiwa katika nchi yetu. Leo tunajadili kwa amani na utulivu na tukiwa tunaongozwa na maslahi ya taifa kwa sababu ya hatua hii kubwa ambayo ilifikiwa na haijapata kuonekana katika historia zaidi ya miaka 50 ya misukosuko ya kisiasa katika visiwa vyetu vya Zanzibar.

Mhe. Spika, katika hilo naomba niwatambue sana wenzetu wawili Rais Mstaafu Mhe. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad kwa mchango mkubwa sana waliochukua kwa uamuzi uliofikiwa tarehe 5 Novemba pale Ikulu ambao hatimaye umetufikisha hapa tulipo.

Lakini pia Mhe. Spika, kuna kamati haijulikani imetoa mchango mkubwa sana katika kuyafanikisha maridhiano hayo. Hii ni tofauti na vyama vyengine ambavyo vilikuwa shughuli zake hadharani viliteuliwa na waheshimiwa hawa wawili waliofanya kazi kubwa sana ya kuwasaidia. Bila shaka iko siku watatajwa watakumbukwa lakini naomba nimtambue tu aliyekuwa kiongozi wetu mzee wetu Mhe. Hassan Nassor Moyo kwa kazi kubwa ambayo aliifanya na hatimaye kufikisha nchi yetu leo ikafika hapa.

Mhe. Spika, kwa dhana hiyo hiyo ya kujenga maridhiano nadhani mzee wangu Balozi Seif Ali Iddi katika ukurasa wa 33 pale kidogo pengine wachapaji walikosea walipozungumzia kuwepo kwa chama tawala. Nadhani hivi sasa Zanzibar tuna muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na hatuna tena chama tawala na chama cha upinzani bali tuna vyama viwili vinavyoshirikiana kuiendesha Serikali ya Umoja wa Kitaifa bila shaka ikiongozwa na Rais kutoka upande wa chama cha CCM.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, mimi naomba nizungumzie masuala matatu. La kwanza ni hili la migogoro ya ardhi ambalo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais amelitaja. Ukisikiliza maelezo yake na hasa hotuba zilizokuwa zikitolewa mara kwa mara na marais wetu inaonekana viongozi wanachangia sana katika migogoro ya ardhi hapa Zanzibar. Sasa kwa sababu Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ndio inayosimamia Uratibu wa Viwanja vya Serikali inategemea iwasimamie viongozi hawa kwa sababu hili limekuwa ni donda ndugu katika Zanzibar.

Mhe. Spika, kuanzia chini huko kwa masheha, madiwani, ukija pengine mpaka kwa baadhi yetu wawakilishi humu, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa kila mmoja kajitumbukiza tele katika migogoro ya ardhi. Pia inakuwa kazi kubwa sana ya wananchi wetu wanyonge wanapoona kwamba wanapambana na viongozi ambao wanavamia maeneo ya wazi, wengine wanavamia mashamba ya watu, maeneo ya baharini ndio yamemalizwa kabisa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, hili linawanyong'onyesha sana wananchi wetu na tuliona kasi kubwa ya Balozi Seif Ali Iddi pale mwanzo lakini tunaona kama vile imefifia fifia. Basi tuko tayari hapa kwamba tunataka kuona matokeo ya kazi ile ambayo alikuwa ameianza ifanywe kwa haki na uadilifu si kwa lengo la kumuonea mtu yeyote wala si lengo la kuwaachisha pengine wawekezaji kuja kuwekeza katika nchi yetu lakini izingatie haki za wananchi wetu tukitambua kwamba nchi yetu ni ya visiwa na eneo letu la ardhi ni dogo sana.

Lakini hapo hapo niungane na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk rafiki yangu. Mhe. Spika, Mhe. Mshimba alizungumzia kwamba tulitegemea katika hotuba hii tupewe maelezo kuhusu sakata la matumizi mabaya katika Baraza la Manispaa. Kwa sababu katika kikao kilichopita tunakumbuka sote palikuwa na mapambano makubwa baina ya *front benchers* na *back benchers* katika suala zima la kutaka kuundwa kamati teule ya kwenda kuchunguza masuala ya mikataba yenye utatanishi katika Baraza la Manispaa. Hatimaye *front benchers* walishinda na ndio *spirit* ya demokrasi katika Baraza. Lakini nikafurahi kwamba kile ambacho kilisemwa na *back benchers* kilikwenda kikathibitishwa na madiwani wenyewe katika Baraza lao la Manispaa.

Kama alivyosema Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba imeripotiwa katika gazeti la serikali la Zanzibar Leo likinukuu baadhi ya mambo ambayo waliyaona Kamati ile ya Baraza la Manispaa. Sasa tunakumbuka wakati Makamo wa Pili wa Rais alipokuwa akituomba tuiridhie serikali na hakuna haja ya kuunda kamati teule alisema tumuachie yeye kwa sababu ndio kwanza analisikia pale na angetupa taarifa Barazani. Sasa tunategemea basi atakapokuja ku-*wind up* atupe taarifa Barazani na tuone wale waliohusika na matumizi mabaya ya madaraka hata ikiwa ni Mkurugenzi, basi achukuliwe hatua ili tuweze kujenga uwajibikaji katika nchi yetu na hapo ndipo tutakapoweza kutunza kweli vyanzo vyetu vya mapato. Hii itasaidia sana kuona kwamba wananchi wanapotozwa kodi au mapato yanapoingia serikalini yanakusanywa kwa ajili ya kunufaisha wananchi wetu na kuipeleka nchi yetu mbele.

Mhe. Spika, la mwisho ambalo nataka kulizungumza lakini kwa upana wake hasa na naamini *inshaallah* dakika zinanitosha ni suala zima la Muungano lililokuwepo katika Idara ya Uratibu. Mhe. Spika, Mhe. Makamo wa Pili wa

Rais katika hotuba yake alisema kwamba idara hii inaratibu shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini pia shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nakubaliana nae kabisa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwamba tunao wajibu wa kuulinda Muungano na kuuenzi, lakini mimi nataka niongezee ikiwa nao Muungano utatulinda na kutuenzi Wazanzibari.
Mhe. Spika, tumejadili kwa urefu sana suala la mafuta hapa na lilitolewa ufafanuzi, naamini yale aliyoyazungumza Mhe. Ali Juma Shamuhuna na yale mengine upande wetu tutakuja kuyatolea maoni zaidi katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Tunategemea kwamba zitachukuliwa hatua kuona Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haionekani kama ni joka la mdimu la kuwazuia Wazanzibari wasitumie fursa zetu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu na watu wake.

Mhe. Spika, Ofisi hii ya Makamo wa Pili wa Rais inayotuwakilisha katika vikao vya mazungumzo baina ya serikali mbili katika kuzungumza zile tunazoziita Kero za Muungano. Napenda niipe changamoto kwamba katika hili tunapaswa kufikiria nje ya *box* kwa sababu inaonekana kiini hasa cha matatizo haya yaliyokuwa hayamaliziki ni muundo wa Muungano wenyewe.

Mhe. Spika, mimi ni mmoja kati ya watu wanaopenda sana kujisomea vitabu vya historia maandishi mbali mbali, katika nyaraka za kihistoria ukizitazama akiwemo mtu mmoja muhimu sana katika historia ya nchi hii bwana mmoja wa Kichina anaitwa *Thomas Frank* alikuwa ni Mshauri wa Kisheria wa chama cha *Afro Shirazi.*

Huyu amenukuliwa katika kitabu cha *Background Revolution* kinachohusu Zanzibar akisema kwamba tatizo moja la Muungano huu umefanywa kwa misingi ya mahusiano ya Ireland ya Kaskazini na Uingereza. Sasa hapa ndio penye tatizo Mhe. Spika, kwa sababu Ireland ya Kaskazini ni koloni la Uingireza. Zanzibar haijapata kutekwa na Tanganyika, hapa ndipo kwenye matatizo baada ya kuona hawa wenzetu wanaona kwamba sisi ni koloni lao. Kwa hivyo, nadhani hili katika kuzingatia misingi ya usawa hasa tunapaswa kudai marekebisho katika msingi huu wa mwanzo kabisa wa mahusiano ya pande hizi mbili, tukijua kwamba Muungano huu wa nchi mbili zilizo huru na zilizo sawa zilizoamua kwa hiari yake kuungana.

Mhe. Spika, tulipoungana aliyekuwa Rais wa Tanganyika Mwalimu Julius Kambarage Nyerere hakuja hapa kama Askofu, wala Mzee Abeid Amani Karume hakutuwakilisha sisi kama Sheikh, walikuwa wote wawili ni wanasiasa na viongozi wa nchi mbili zinazoungana Tanganyika na Zanzibar. Kwa hivyo,

msingi wa mahusiano yetu lazima uzingatie misingi ile ya nchi mbili zilizoungana kisiasa, sio kama vile kuna masuala ya kidini hapo kati kati kwamba yakiguswa inakuwa ni matatizo. Katika hilo nalileta katika masuala haya ya kero.

Mhe. Spika, tumeambiwa hapa kwamba kodi za kutozwa mara mbili zimeondoka. Mhe. Spika, hili suala tunapewa taarifa katika makaratasi tu katika hali halisi halijaondoka, bado wafanyabiashara wetu wanalalamika sana na Zanzibar ni nchi inayotegemea biashara. Kwa hivyo, ukikwamisha suala la utozaji kodi mara mbili unakwamisha biashara Zanzibar na unakwamisha uchumi wa watu wa Zanzibar na maisha ya watu ambao wanategemea kupata riziki zao kutokana na mzunguko wa biashara kutoka Zanzibar. Kwa hivyo, hili tunaomba tupewe maelezo hasa linakwama wapi kwa sababu tumekuwa tukiahidiwa miaka nenda miaka rudi lakini bado utekelezaji wake unakuwa na vikwazo. Itakuwa ni lile lile lengo alilosema mwanzo kama Muungano haukusudii kuienzi Zanzibar ambalo utekelezaji wake unakuwa na vikwazo. Lakini Zanzibar tunatakiwa kuenzi Muungano basi kweli Mhe. Spika, hatutofika.

Hapo hapo nizungumzie hili la mgawanyo wa misaada kupitia *GBS*. Mhe. Spika, jana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katuhakikishia hapa kwamba tunapata shida katika kupata na takriban tunapoteza karibuni bilioni 131 hazikugawiwa hizi kwa sababu zinapitishiwa katika mifumo ya kisekta. Sasa mimi hapa nina rai wenzetu wamekuwa wakitumia jina la Tanzania kuomba na kuchukua misaada kwa mambo ambayo sio ya Muungano lakini sisi Zanzibar hatunufaiki. Hii wanaipata kupitia ule utaratibu wa mkutano baina ya nchi washirika wa maendeleo na ile Jamhuri ya Muungano.

Mimi hili nimelifanyia utafiti Mhe. Spika, nimezungumza na mabalozi kadhaa na wametuthibitishia kwamba ikiwa Zanzibar itaamua kuanzisha *consultation grouping meeting* kwa ajili yake kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano, Jumuiya ya Kimataifa iko tayari kuasisi kwa kupitia serikali hii na Zanzibar iweze kuanzisha programu zake wenyewe kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano. Natoa changamoto hiyo kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais tuone kwamba sura ile inaanzishwa kuanzia mwaka huu wa fedha. Ili huu ujanja wa kutupitishia misaada hii katika sekta ambazo sisi tunakosa kuzipata irudi Zanzibar na fursa kama hiyo tuweze kuipata kama ambayo Tanganyika wanayo kupitia kwa kutumia vibaya jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hapo hapo Mhe. Spika, nije katika suala la Tume ya Pamoja ya Fedha limezungumzwa hilo. Tume ya Pamoja ya Fedha imetajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 133, hapa ndipo tungetegemea kujua uhalisia kwa wazi kabisa juu ya nani anachangia nini na anapata nini katika Muungano huu. Vyanzo vya mapato kweli vinatosheleza au havitoshelezi, tunapaswa kuchangia na tunapaswa kupata faida kutokana na vyanzo vya mapato vya Muungano.

Mhe. Spika, ripoti iliyotajwa ni ya mwezi Agosti, 2006 iliyofanywa na wataalam waliopewa kazi hii na Tume ya Pamoja ya Fedha. Mimi nimebahatika kuiona walichanganua mle vyanzo vya mapato vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania halafu wakavigawa katika mafungu matatu, vile vinavyohusu matumizi ya Muungano, vinavyohusu matumizi ya Zanzibar visivyokuwa vya Muungano na vinavyohusu Tanganyika visivyokuwa vya Muungano. Wakagundua kwamba Tanganyika na Zanzibar hazitapaswa kuchangia chochote katika Serikali ya Muungano kwa sababu vyanzo vyake vya mapato vinatosheleza kabisa kuendesha na bakaa ikabakia ikagawiwa kwa Tanganyika na Zanzibar. Hicho ndio kisa mpaka leo ripoti ile inakaliwa haitaki kutolewa tusidanganyane. Kwa hivyo, tunaomba pia ile tuambiwe badala ya kuahidiwa kila siku kwamba linafanyiwa kazi, tunaomba sasa tupate matokeo ya kazi hiyo sio kuambiwa tu linafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, hapo hapo nimalizie kwa suala la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Hili sikulisikia kabisa katika hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais wakiwa wao ndio waratibu wa shughuli za Muungano kwa upande wa Zanzibar hata kutuwakilisha sisi ofisi inayohusika. Nilikuwa naomba niseme katika hili na naomba nitumie kanuni zetu kifungu cha 96 (b) na (c) kwamba nitazuia shilingi ikiwa sikupata maelezo ya kutosheleza juu ya hatma ya Zanzibar katika Afrika ya Mashariki.

Kwa sababu gani Mhe. Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki ukipitia mkataba wake una mambo 17 ambayo yanasimamiwa na jumuiya ile, katika mambo haya 17 kwa upande wa Jamhuri ya Muungano ni mambo manne tu ndio mambo ya Muungano, lakini mambo 13 sio ya Muungano kwa upande wa Tanzania. Ndio kusema Zanzibar ina haki ya kusimamia wenyewe mambo haya na hili limo katika mkataba wa Muungano wa mwaka 1964. Tulisemwa wazi mle kwamba Serikali ya Zanzibar itakuwa na mamlaka kamili kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano, hilo linatambuliwa na Katiba ya Muungano hata hivi sasa pamoja na maelezo yake yote lakini wanatambua. Ukisoma kifungu cha 102 kifungu cha kwanza kinasema.

> “Kutakuwa na Serikali ya Zanzibar itakayojulikana kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo itakuwa na mamlaka katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo ya Muungano kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.”

Lakini nataka kulinganisha hilo na Katiba yetu ya Zanzibar katika kifungu kinachozungumzia Baraza la Wawakilishi. Kifungu cha 78 kinasema:

> “Nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano katika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi”.

Sasa Mhe. Spika, hoja yangu ni kwamba Serikali ya Muungano inapokwenda kutuwakilisha kwa mambo haya 13 haina haki hiyo wala haina mamlaka hayo, haya ni madaraka na mamlaka pekee ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa tunapoambiwa kwamba Zanzibar haiwezi kuwa mwanachama wa Afrika ya Mashariki hili sio sahihi kwa sababu huyo anayekwenda kutuwakilisha hana mamlaka na mambo haya. Ndio maana nikasema kwamba kwa hili kama sikupewa maelezo ya kutosha nitazuia kifungu cha Idara ya Uratibu mpaka nihakikishiwe hatua gani zitachukuliwa ili Zanzibar iweze kupata haki zake katika Afrika ya Mashariki.

Mhe. Spika, katika hili tusidanganywe kwamba haiwezekani hakuna jambo ambalo katika dunia haliwezekani hasa haya mambo ya sheria. Mhe. Spika, Jumuiya ya Ulaya imeweka vifungu maalum kwa baadhi ya nchi ambazo zina masharti maalum, sasa nasema na Zanzibar inawezekana kufanyika hivyo. Nilikuwa naomba tupewe maelezo katika hilo tuone vipi Zanzibar itawakilisha pendekezo rasmi katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kama nilivyosema nitaunga mkono hoja baada ya kupatiwa maelezo niliyoyaomba. Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Ismail Jussa Ladhu umezitumia vizuri dakika kumi na tano kuwasilisha michango na hoja ulizokuwa nazo. Waheshimiwa Wajumbe jioni naomba waheshimiwa hawa wawe tayari kusijekuwa hakuna wachangiaji. Nao ni Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Shawana Bukheti Hassan, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Abdulla Juma Abdulla, Mhe. Rashid Seif Suleiman na Mhe. Saleh Nassor Juma, wajitahidi pamoja na waheshimiwa wengine wote kufika mapema ili tuendelee na mjadala wetu.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(majadiliano yanaendelea)

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa dhati kwa jioni hii ya leo kunipatia nafasi hii ya kuweza kuichangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.
Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye aliyetuwezesha siku hii ya leo tukawa tuko katika hali ya uzima. Mhe. Spika, nichukue fursa hii adhimu kwanza nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na watendaji wake wote ambao wamempangia kitabu hiki mwanana, chenye kufahamika na kueleza maelekezo ambayo yatakuwa ndio dira ya kuweza kufanya kazi.

Kabla sijaendelea Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nimechukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais jinsi anavyofuatilia mambo na kutupa dira ya kufuata nyayo zake.

Mhe. Spika, Mhe. Rais ni kipindi kifupi tu baada ya kuchukua madaraka ya urais, basi aliita wizara zote kwa siku maalum ili kuhakikisha anauliza matatizo ili apate kujibiwa na kuwajua watendaji wake. Si hilo tu Mhe. Spika, Mhe. Rais alitembelea mikoa yote mitano, kwa upande wa serikali kuuliza matatizo jinsi alivyojionea mwenyewe katika matembezi yake ya ziara yake. Pia nimpongeze sana alitembelea katika chama chake cha Mapinduzi. *(Makofi).*

Mhe. Spika, huu ni mwelekeo ambao ni wa kutuonesha sisi kuwa tufuate nyayo zake. Naomba sana Mhe. Spika, niwaambie wajumbe wenzangu kuwa na sisi tukubali na tubadilike ili kusimamia vyema dhamana tulizopewa na kuaminiwa na wananchi wa taifa hili la Zanzibar.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii nimpongeze tena Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa jitihada zake ambazo anachukua na kuhakikisha kwamba anasimamia vyema, kwa sababu yeye ndiye dhamana na ndiye mkuu wa serikali, kuhakikisha kwamba yale yote ambayo anaelekeza yanafanyiwa maamuzi. (*Makofi).*

Pia nipongeze na namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Mhe. Rais wa Zanzibar, tuwashukuru sana Mama Shein kwa jitihada zake ambazo

anazifanya. Vile vile nimpongeze Mama Asha Seif Ali Iddi, jinsi na yeye alivyofunga mkaja kuhakikisha anasaidia katika nyanja mbali mbali. *(Makofi).*

Vile vile nichukue nafasi hii nimpongeze kwa dhati Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Hamad, kwa jinsi anavyofuatilia kwa karibu sana majukumu yake na hasa kutilia mkazo katika masuala ya ukimwi, mazingira na pia kutafuta wafadhili ili kuweza kusaidia taifa letu.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye mchango wangu. Mimi nitaanza na suala la rushwa. Mhe. Spika, sisi suala la rushwa tunaliona kama ni mzaa mzaa tu, lakini rushwa ipo Mhe. Spika, naomba sana kwa kupitia kwa Makamu wa Pili wa Rais, suala hili liangaliwe kwa uangalifu. Kuna baadhi ya sehemu unapokwenda kama hukutoa senti basi huwezi kufanikiwa yale ambayo unayahitaji.

Kwa hivyo, natoa indhari Mhe. Spika, suala hili lichunguzwe kwa makini ili tuepukane na kashfa ambayo kwa Zanzibar haijaenea vilivyo. Niseme tu kwamba tujitahidi ili kuhakikisha suala hili lisije likatuharibi taifa letu hili.

Mhe. Spika, nizungumzie jambo jengine ambalo ni suala la utalii. Suala la utalii wenzangu wameligusa, sitaki nirejee na mimi nitilie mkazo tu kama nilivyochangia huko nyuma katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Nadhani ni vyema tukajipanga upya ili kutathmini mahoteli yetu ya aina mbali mbali. Mfano, hii ni hoteli ya aina gani, iko *class* gani inatakiwa ifanye nini pamoja na kuhakikisha wafanyakazi ambao wamo mahotelini.

Mhe. Spika, ukenda mahotelini utasikitika jinsi wafanyakazi wanavyonyanyaswa na wenye mahoteli. Kwa hivyo, naomba sana kupitia kwa Makamu wa Pili wa Rais, suala hili lizingatiwe na lifanyiwe utafiti kama nilivyosema, ili kuhakikisha tunapokuwa na utalii tujue utalii wetu utatuletea tija na sio kutuharibia.

Mhe. Spika, nije kwenye Idara ya Upigaji Chapa. Kwanza nichukue nafasi hii kwa kuwapongeza sana wafanyakazi wa idara hii ya Upigaji Chapa, kwa kweli wanafanyakazi katika mazingira magumu. Mhe. Spika, sijui niseme idara hii imekaa kama yatima au kama iliyoapizwa, kwa sababu ni miaka mingi sana toka mimi ni Naibu Waziri wa Habari, idara hii kwa kweli ina misukosuko ya sehemu ya kuweka mitambo yake.

Mhe. Spika, nakumbuka kwenye miaka ya 1979 au 1978 iliagizishiwa mitambo basi ilioza haikuweza kufungwa. Kwa hivyo, kupitia kwa Mhe. Makamu wa

Pili wa Rais nimefurahi kuonekana kwamba humu matarajio yake ambayo ameyazungumza basi naomba sana kutilia mkazo kuhusu suala hili la Idara ya Upigaji Chapa.

Mhe. Spika, nichukue tena nafasi hii niwapongeze sana kwa sababu wanatumia uzalendo na kama sio uzalendo wao basi kwa kweli hivi vitabu visingechapwa na baadhi ya mambo yasingechapwa, lakini ni kutokana na uzalendo.

Mhe. Spika, nije katika suala ambalo mjumbe mwenzangu aliligusia hapa, kwenye hiki kitabu halimo, lakini naomba nizungumze kidogo. Mhe. Spika, kwa kweli tutaikaba Manispaa. Manispaa hivi karibu baada ya kumaliza ziara ya kamati yangu, ile kamati ilikaa kama iliyokwenda kuwashtua Manispaa, Meya mwenyewe akaunda tume ili kuchunguza ubadhirifu wa fedha ambazo zinatumika vibaya.

Mhe. Spika, kupitia kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba sana kwamba suala hili tusilifanyie mzaha, suala hili lichunguzwe kwa makini ili tuhakikishe wale ambao hawawezi kuitumikia Zanzibar basi wapishe wenzao.

Mhe. Spika, nilisema nitadokoa tu kidogo kidogo, nije katika watendaji wetu. Naomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na ni imani yangu na hasa ulivyopata waziri ambaye kwa kweli ki mtizamo waziri huyu na anavyotuonesha hapa katika Baraza hili tukufu kwamba atakusaidia sana pamoja na watendaji wako. Naomba sana watendaji wetu wabadilike, kuna watendaji wengine mtu saa 3:00 hajafika afisini, mfanyakazi wa chini yake atafika saa ngapi, naomba wabadilike.

Jengine kubwa, mtanisamehe wajumbe wenzangu na kama wakinisikia wenyewe watanisamehe. Watendaji wanaingia kwenye madaraka hata hautimii mwaka mmoja au miwili basi mtendaji ana nyumba tatu, gari saba, maduka na kadhalika. Kwa kweli mimi naomba ile sheria Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo mutuletee haraka ili itupe miongozo kuhakikisha kwamba watendaji wanajua dhamana zao na hawafanyi ubadhirifu wa fedha.

Ninashangaa Mhe. Spika, nasema hili kwa udhati wa moyo wangu na kwa uchungu wa nchi yangu, kwa kweli tubadilike tena tubadilike tuache mambo ambayo hayatotuletea tija katika nchi yetu. Naomba sana kwa kupitia Baraza lako hili tukufu kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tuhakikishe tunakwenda na wakati.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia *fil* mia, ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Asha Bakar Makame amenikumbusha jambo moja la baadhi ya watendaji kufika maofisini wakiwa wamechelewa. Hapa tuko kwenye kikao cha Baraza la Wawakilishi tukizungumzia habari ya bajeti, viti hivi hapa vya wajumbe na hivi vyengine hapa vya mawaziri, nina taarifa za dharura za mawaziri wawili tu. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Wengine wote sina taarifa nao. Namshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu anaingi hivi sasa. *(Makofi).*

Kwa hivyo, kama Mhe. Asha Bakar anawaambia watendaji basi na tujiambie na sisi wenyewe ili wananchi wanapoona kwenye televisheni zao na wakati huo pengine ndio Mhe. Asha Bakar alikuwa anasema na kulaumu watendaji, basi wenyewe kule watendaji wanaweza kusema aah! mbona anasahau wao wenyewe hawapo. *Chief Government Whip* yupo nadhani atafanyakazi yake inayomuhusu. Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana.

Baada ya maneno hayo mbayo pengine hayafurahishi, lakini ni wajibu kuyasema. Sasa tumsikilize Mhe. Shawana Bukheti Hassan, baada ya hapo tumsikilize Mhe. Omar Ali Shehe.

Mhe. Shawana Bukheti Hassan: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi kwa jioni hii ya leo kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Spika, hotuba ni nzuri, inayoleta matumaini kwa wananchi na inayotegemewa sana kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, pamoja na nitakayoyazungumza lakini nitamke mapema kuwa hotuba hii mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Dole tunaikubali kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, katika mengi yaliyoelezwa katika kitabu hiki, yaliyonifurahisha mimi hasa ni masuala mazima yanayoelezea ziara ya Mhe Makamo wa Pili wa Rais alipokwenda nchi za nje.

Kwa kweli ziara za viongozi wetu zinaleta tija kubwa nchini mwetu. Mhe. Spika, ziara kama hizi ndizo tunazozitegemea na ziara kama hizi hatukereki nazo ambazo wanakwenda wenzetu na wanakuja na kitu ambacho kitawasaidia wananchi, kitaongeza uchumi wa nchi yetu na kitawaondoshea umaskini wananchi wetu. Hongera sana Mhe. Makamo wa Rais kwa ziara zako hizi ambazo zina mustakabali mzuri wa nchi yetu. *(Makofi).*

Mhe. Spika, moja ya ziara ambazo zimenikosha ni hii ziara ya Abudhabi. Ziara hii Mhe. Spika, katika mengi yaliyoelezwa naomba kunukuu, inaelezea ujenzi wa bandari katika eneo la Mpigaduri na Kiwanda cha Kusindika Samaki. Mhe.

Spika, hayo ni maendeleo makubwa. Katika suala moja kubwa katika nchi yetu mpaka sasa hivi ambalo linawaletea shida wananchi wetu ni bandari.

Bandari iliopo sasa hivi Mhe. Spika, haitoshi, hivi sasa katika mazingira tuliyokuwanayo, abiria katika eneo wanalopanda meli na kushukia, kwa kweli hali ni ngumu sana pale. Kitishari kile ni kidogo na kinateleza teleza pale, hata hali ya amani katika upandaji na ushukaji wa meli pale linaleta mashaka.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama tutamudu kweli na hawa wenzetu kama watatukubalia kutujengea hii bandari kweli tutafika kwenye hatua kubwa na nchi yetu itaweza kunufaika kiuchumi. Kwa sababu katika maeneo ambayo yanayoongezea uchumi wetu au mapato yetu ya ndani, moja ni Shirika la Bandari. Kwa hivyo, mimi napongeza sana na Mwenyezi Mungu amjaalie aendelee na ziara nzuri ambazo zitaendelea kutuletea matunda katika nchi yetu.

Mhe. Spika, niendelee na ziara nyengine ambayo alikwenda Iran. Katika ukurasa wa 42(k), kuhusu upanuzi wa hospitali ya Mnazi Mmoja. Suala hili pia nataka nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Makamo wa Rais kwa ziara yake hii pamoja na hawa walioahidi kututanulia hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.
Mhe. Spika, Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja pamoja na jitihada ya kuwa kutakuwepo na jitihada ya kuwa kutakuwepo na hospitali za Kiwilaya, lakini hospitali ile inataka itanuliwe na kufanyiwa marekebisho ya hapa na pale katika huduma za mule hospitali ili iweze kuwa kweli hospitali ya rufaa. Hili pia namshukuru Mhe. Makamo kwa ziara hii, tunaamini kuwa haya yote tukifanikiwa yaliyoelezwa humu katika wizara yake basi mambo yatakuwa mazuri. Ukiacha masuala ya mboga mboga ya kusafirisha na kupeleka Seychelles, kuna masuala ya kilimo na usarifu wa mazao ya chakula na kuna mambo mengi ambayo Mhe. Makamo ameyasema, kwa kweli tunapongeza na Mwenyezi Mungu ajaalie haya yote yaliyoandikwa humu tuweze kufanikiwa. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, la pili nataka nije kwenye suala zima la madawa ya kulevya. Mhe. Spika, suala la madawa ya kulevya sasa hivi limeshatutosha ndani ya nchi yetu. Suala hili kila tunavyojitahidi kulitafutia dawa naona haijapatikana. Ninachomuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, hetu tusaidiane hasa kwa udhati kabisa katika haya maeneo yanayopitishwa haya madawa ya kulevya tunaambiwa kuwa njia kuu ni bandari na *airport*, lakini *airport* nafuu kuliko bandarini.

Mhe. Spika, mimi nataka kukubaliana na hili kuwa inawezekana sana bandarini ikawa ni kituo kikubwa cha kupitisha madawa haya ya kulevya, kwa sababu pale hakuna mashine za kuonesha inapopitishwa ile mizigo ikaweza kuonekana

na kujulikana upi una madawa ya kulevya na upi uko salama. Kitu cha kuchekesha pale Mhe. Spika, abiria wanapoteremka basi hukaa mtu mmoja akawa anapunga mkono tu, anamwambia mmoja nenda pale. Sasa huku anamwambia mmoja nenda pale na huku kumi na sita wameshampita mizigo haijaenda kupekuliwa. Kwa hivyo, jambo hilo naliona sio sahihi na halitufanyi tukaweza kugundua nani ana madawa ya kulevya na nani hana. Kwa sababu mmoja unamwambia aende kule na wale kumi na sita waliokupita pengine ndio wanayo hayo madawa.

Kwa hivyo, nadhani tutafute njia madhubuti ya kuona pale kuwa kweli ndio njia ya kupitisha yale madawa, hebu tutafuteni dhana ambazo tutaziweka pale bandarini ili hawa wanaopitisha haya madawa ya kulevya basi waweze kugundulika. Hilo lilikuwa la pili.

Suala jengine la tatu Mhe. Spika, nije katika suala zima la mradi wetu huu wa TASAF. Mhe. Spika, mradi wa TASAF ni mradi mzuri, unawasaidia wananchi katika kuwaondoshea shida na kero zao katika maeneo yetu ambayo tunakuwa na shida mbali mbali, vituo vya afya, maji, barabara na mambo mengine.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba hebu safari hii, nafikiri itakuwa TASAF III iangalie vizuri zile shida hasa za wananchi. Mhe. Spika, katika jimbo langu mpaka hivi ninakuambia mradi hasa ule unaowagusa wananchi katika shida zao kama hizo nilizozieleza skuli, maji, vituo vya afya na kadhalika hatujafaidika. Wananchi wanaibua mradi mwengine lakini TASAF wanakuja na hisia nyengine.

Kwa mfano Bumbwisudi pale wameibua mradi wa maji, lakini matokeo yake wamekuja kuletewa mradi wa ukimwi na miradi ya ukimwi hiyo iko kila Shehia. Tatizo la ukimwi lipo na linataka kushughulikiwa na watu wapewe elimu, lakini kuna mambo ambayo ni mazito zaidi, maji Mhe. Spika, hayana mbadala. Mradi ule ulikuwa na milioni 19 na milioni 19 zingeweza kupatikana kwa mujibu ya miradi hii inavyopangwa. Lakini matokeo yake hawakupatiwa mpaka hii leo. Tumehangaika sisi wenyewe kwenda *ZANTEL* na kwengine ndio tumeweza kukamilisha kidogo.

Sasa Mhe. Spika, mimi naomba kama wanahisi mradi huu wanaoupitisha wananchi hawawezi kuumudu kuukamilisha, basi ni vizuri warudi kwa wananchi wakawaambie, kuliko tu wakaamua mradi huu hawaupeleki wanaamua kupeleka mradi mwengine, hiyo haipendezi na tunaomba jambo hili lifanyiwe masahihisho.

Jengine Mhe. Spika, ijapokuwa tunaambiwa mswada utakuja lakini mimi ningeomba nilizungumzie tu kidogo kwa sababu naona hata utakapokuja huo mswada kwa upande wangu nitakuwa nimeshapata mitihani mikubwa kidogo. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa vile yeye ndiye msimamizi mkuu wa serikali au wa shughuli za serikali, hebu ajaribu sana kusaidiana na mawaziri husika, ikiwa na makatibu wakuu au na watendaji wengine katika suala zima la mikataba inayotiwa hapa nchini kwetu katika shughuli zetu za kutuletea maendeleo.

Mhe. Spika, kwa nini nikasema hivi. Sasa hivi tunajengewa barabara, ni vizuri, tunafurahi na tunashukuru sana, kwa sababu tatizo la barabara linatupa dhiki na linatupa shida na tukijengewa barabara ni asilimia moja kati ya mambo ambayo yanatupunguzia umaskini. Lakini nashangaa Mhe. Spika, mikataba inavyofungwa, barabara zile hazina viwango hasa vinavyotakiwa, viwango vyao ni kwa pale inapopita gari tu. Katika sehemu zile za pembeni mwa barabara hakuna umaliziaji mzuri, barabara unapojenga lazima iwe na misingi, barabara zetu hazina misingi kwa hivyo zinatuletea maafa.

Mimi Mhe. Spika, jimboni kwangu nimeshapata maafa na nitaendelea kuyapata, kwa sababu sasa hivi barabara inayojengwa ni ya Amani/Dunga, nategemea maafa hayo yanaweza yakatokea, maana yake sasa hivi nyumba ziko mabondeni na barabara ziko juu. Kwa hivyo, mimi ningewaomba hao wahisani wetu wanapokuja kujaza mikataba, hao makandarasi wetu basi tukubaliane katika suala la barabara iwe ni ya aina gani.

Sasa hivi pale maafa yatatokezea wakati wowote tusiyoyategemea, maana yake kuna maafa ambayo yanatengenezwa na Mwenyezi Mungu na maafa wakati mwengine sisi wanadamu tunayatengeneza, sasa moja ni kama lile. Kweli ni suala zuri la kutengenezewa barabara lakini maafa wakati wowote yanaweza yakatokezea. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba sana katika suala hili liangaliwe. Kwa hapa tulipofikia wao wenyewe watatizama ni jinsi gani ya kurekebisha, lakini huko usoni tunako kwenda kuna haja ya kuonekana suala hili linafanyiwa kazi vizuri, ili hao wakandarasi watakaokuja, basi tukubaliane barabara ikijengwa ijengwe na misingi vyenginevyo maafa yatakuwa yanatokezea kila siku na wala hayeshi.

Mhe. Spika, nimalizie kwako wewe. Naomba nichukue nafasi hii kukupongeza kwa dhati kabisa kwa jinsi unavyosimamia Baraza hili, umri wako katika Baraza hili na mimi umri wangu katika uwakilishi ndani ya Baraza hili unalingana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tokea umeingia nafasi yako ya Uspika mimi kura yangu unayo mpaka hii leo. Kwa kweli kura zetu hazikupotea, yaani tulichagua mtu ndiye ambaye ni makini, muadilifu, mwenye kutambua mambo pamoja na kupenda maendeleo. Kwa kweli hongera sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tulikuwa tukiondoka kwenye mabao yale tukikuandikia memo kwamba sote tunaumia migongo na hivi sasa tunakwenda kiajabu ajabu wewe mwenyewe unajua Mhe. Spika tuliko tokea, yaani ilikuwa hali ngumu, lakini leo *Alhamdulillah*. *(Makofi)*

Pamoja na jitihada za muhisani, lakini bila ya juhudi zako pamoja na kushirikiana na serikali yetu basi muhisani huyo asingeweza kupatikana. Kwa hivyo, tunakushukuru kwamba leo tupo hapa tunakushukuru *Alhamdulillah* kwa hilo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninachokiomba au kushauri kwa kuwa jengo letu zuri na kwamba tunao utamaduni mzuri sana kama vile Rais aliyemaliza muda wake wa Awamu ya Sita na hili alilisema kwamba tunao utamaduni wa kujenda majengo mazuri, lakini kuyatunza, kuyafanyia usafi pamoja na kuyafanyia ukarabati tunakuwa wazito.

Kwa hivyo, jengo letu hili ni zuri na tunachokiomba Mhe. Spika, kuwa jengo hili tulitunze na wala tusiogope gharama kwa sababu vizuri vina gharama na kama hutaki gharama basi vizuri huwezi kuwa navyo. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, tufanye vyovyote na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na yeye anatusikia hapa pamoja na hali tuliyonayo kwenye bajeti yetu atutafutie utaratibu maalum na jengo letu tutafute watu wenye uzalendo, kwa ajili ya kutufanyia usafi wa *high dusting* na wala sio hii ya kufuta vumbi tu, kwa sababu jengo baada ya miaka mitano litakuwa si jengo, yaani tayari limeshachakaa. Kwa mfano, watu wanatakiwa wasafishe mpaka vioo vya nje. Kwa hiyo, mimi naomba sana Mhe. Spika na suala hilo lichukuliwe kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Mwisho kabisa Mhe. Spika, naomba sana kwa sababu humu kimetajwa Kitengo cha *Hansard* wamepatiwa mafunzo mambo gani. Kwa hivyo, ninachoomba hawa vijana wetu wa *Hansard* pamoja na yote wanayofanyiwa ya jumla jumla wao wafikiriwe na utaratibu maalum, yaani hapa wanakaa watu wote wanaondoka wanafika mpaka saa 6:00 vijana wetu wa *Hansard* bado hawajaondoka. Kutokana na hali hiyo, nao tuwafikirie na wao katika hali hiyo waliyonayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimalizie kwa kumpongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa mara ya pili na Mwenyezi Mungu amjaalie *spirit* aliyoanza nayo aende nayo hiyo hiyo na sisi tuko pamoja na yeye, naunga mkono hoja kwa asilimia 150. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Sheha: Mhe. Spika, kwanza na mimi napenda niitumie fursa hii nikushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii, ili niwe mchangiaji katika Hotuba hii muhimu ya Makamu wa Pili wa Rais.

Kwanza na mimi naomba nianze kwa kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi, kwa kuchaguliwa kwake kuikamata nafasi hii. Kwa kweli Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein hakukosea, yaani alifanya kazi kubwa ambayo ni ya ziada na hatimaye akatupatia chombo kama hiki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ni mtu makini sana, sifa ya pili ni mtu mwenye uwezo, tatu ni mtu mwenye utashi na nne ni mtu mwenye uzalendo. Kwa kweli mambo haya manne aliyonayo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ndiyo yanayonifanya niamue kuchukua nafasi hii maalum kutoa pongezi zangu kwake yeye. *(Makofi)*

Naamini kwamba ataendelea na kazi na wala hatomuangusha Mhe. Rais na atafanya kile ambacho Wazanzibari tunakitegemea ndani ya kipindi cha miaka hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mnasaba wa sifa hizo nataka nianze kwamba tunayo matatizo mengi Zanzibar, yaani mengi sana kuanzia kiuchumi, kijamii pamoja na mengine. Lakini msingi wake mkubwa ni tatizo la nidhamu katika utendaji wa serikali umeshuka. Kwa kweli kama tutakaa na kutafakari, kwa sababu sisi tunakwenda katika mawizara pamoja na idada, tutaona kwamba kuna tatizo la nidhamu ya kiutendaji, nadhani kwanza tunanze kazi hii ya kulirekebisha hili.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, asimamie utendaji serikalini. Sasa wapi ataanzia ni vyema kwanza aanze na mawaziri wake, kwa kweli haipendezi na tena ni aibu kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi yupo kwenye kiti na mawaziri hivi sasa hawaoni wako wapi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sisi Wawakilishi hali hii inatupa tabu na ninaamini na wananchi nao inawapa tabu hiyo. Sasa hali hiyo haitoi picha nzuri na wala haioneshi umakini wa mawaziri katika hili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi kama Wawakilishi kwa kweli tunataka kuona mawaziri wetu wanawajibika, kwa sababu wao ndio serikali, kwani tutakapokuwa na mawaziri goigoi maana yake usitegeme Makatibu Wakuu watafanyakazi, pia tusiwategemee Wakurugenzi kama watawajibika na wala usiwategemee wafanyakazi kama watawajibika. Kwa maana hiyo, nadhani Mhe. Makamu wa Pili wa Rais uanze na mawaziri wako. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika hilo niungane na hoja ya kuliomba Baraza la Wawakilishi kurudisha Kanuni inayotaka Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ajibu Maswali ya Papo kwa Papo. Kwa kweli hoja ile inao umuhimu wake, kwa sababu tunataka Makamu wa Pili wa Rais ajue kila kinachoendelea katika nchi kwa kila siku na pia tunataka Mhe. Makamu wa Pili wa Rais maana yake kila siku apate taarifa za mawaziri wake, yaani wawe karibu. *(Makofi)*

Sasa hoja ile itamfanya kwanza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais awe karibu na mawaziri wake kwa kila wakati, pia itamfanya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ajue kila kinachotokea na kinachoendelea katika nchi kwa siku, yaani ikiwa hivyo basi naye atakuwa na nafasi nzuri ya kumshauri vizuri Mhe. Rais wa Zanzibar.

Kwa mfano, leo ukienda katika serikali unaweza kumuuliza waziri hebu tupe taarifa kwamba leo umefanyakazi gani, andaa utaratibu huo, yaani waulize mawaziri, wiki na hata mwezi huu, lazima twende huko. Vile vile watendaji hata wa chini na wao waulizwe. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, leo unaweza kwenda na kumkuta mfanyakazi ndani ya wiki nzima ukimuuliza umefanyakazi gani hakuelezi na hiyo ndio Zanzibar tuliyonayo hivi sasa, yaani mtu anaingia na kutoka wakati anaotaka kazini na wala hatuwezi twenda katika hali kama hiyoi. Kwa kweli hivi sasa umefika wakati lazima tubadilike kama tunataka maendeleo ya kweli ndani ya kipindi cha miaka mitano. Naomba nimalizie hapo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi ni muhimili wa Dola na moja miongoni mwa kazi iliyopewa na Katiba ni kuisimamia serikali. Tatizo langu ambalo ninalolipata ni juu ya suala ya namna ya kuisimamia serikali. Kwa mfano, tunaweza kuisimamia serikali kupitia utendaji wa Kamati zetu, lakini muda wa utendaji wa kamati zetu ni mdogo. *(Makofi)*

Kwa kweli hapa naomba nizungumzie hasa nizungumzie Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*). Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu. Kwa mfano, hivi sasa tumo kwenye bajeti wizara 16 zitakuja kuomba fedha hapa na zitakapopewa fedha mwaka mzima zitakwenda

kwenye matumizi. Kwa hivyo, lazima kiutaratibu fedha zinazotolewa hapa tufike pahala ziwe *accounted for* na Kamati hii. *(Makofi)*

Utamaduni na utaratibu unatuonesha kwamba kufuata ripoti tu ya Mdhibiti ni wizara nyingi tunaidhinisha fedha, lakini ndani ya mwaka kuna wizara ambayo hazipitiwi hata mara moja kukaguliwa katika hili na Mhe. Spika, hilo lipo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tukiwa na wizara 16, kuna Mashirika ya Umma na ndipo hoja ilipokuja na wenzetu hatimaye Bara kawafikia uamuzi wa kuigawa Kamati, ili kuzipa nafasi kamati nyengine ziweze kusimamia, kwa sababu tunasimamia wizara 16, mashiriki, halmashauri zote kwa muda wa wiki mbili. Kwa mfano, tukiangalia ripoti iliomo mikononi Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi basi peke yake ichukue wiki moja, yaani wizara moja, tunazo wiki ngapi ndani ya mwaka.

Mhe. Spika, ninachotaka kukizungumzia hapa ni kwamba tunangalie upya utendaji wa kazi za Kamati zetu na muda wake, nasema kwa kamati zote, lakini kila mwenye kulia, basi naomba Kamati ya *PAC*, ili tuone vizuri kwamba fedha tutakazoziidhinisha hapa mwisho wa siku tunakuja kupata majibu yake ya Kamati ya *PAC*, basi tunaomba muda wa Kamati ya *PAC*. *(Makofi)*

Kwa kweli hili si geni Mhe. Spika, kuna mabunge kadhaa kamati hii inafanyakazi kwa muda wa mwaka mzima. Kwa mfano, tumekwenda Malaysia walitueleza hivi na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni shahidi, pia wenzetu nchi za Afrika Magharibi nao ni hivyo kwa umuhimu wa kazi hii.

Mhe. Spika, katika hilo la Baraza la Wawakilishi kuna mradi mkubwa sana na tunashukuru na tunawapongeza wahisani pamoja na serikali kwa kutupatia jengo zuri kama hili. Lakini jengo bado halijakamilika kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe wako watakapoondoka hapa wengine sijui wanapanda kwenye daladala wanakwenda Kanyeni, wengine Hanyegwamchana. *(Makofi)*

Kwa kweli hatuwezi kuwa na chombo kama hiki na Waheshimiwa Wajumbe wakitawanyika nyakati za usiku ni hatari hata kwa usalama wao. Kwa hivyo, jengo zuri hili lingelipendeza zaidi Mhe. Spika, Waheshimiwa Wawakilishi wakawa na *hostel*. Mhe. Spika, ni mradi mzuri sana ambao unaweza kuliingizia Baraza pamoja na serikali fedha nyingi sana.

Kwa maana hiyo, tunacho kiwanja kizuri sana hapa, kwa nini serikali na Baraza la Wawakilishi halijengi jengo moja ambalo Waheshimiwa Wawakilishi wote, ikawa ni utamaduni kila baada ya kipindi cha miaka mitano Wajumbe wapya wanapokuja wanakabidhiwa funguo, basi makato yao unayakata moja kwa moja. Nadhani hilo litalisaidia sana chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mara hii hatuwezi kutalipigia buti hili wala kulizuia. Lakini naamini kwamba hatua zitachukuliwa na pengine katika bajeti inayokuja, basi itakuwa ni mmoja katika ya miradi ya Baraza la Wawakilishi au serikali na fedha zipo.

Kwa mfano, jana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alitueleza kwamba fedha zipo, kwamba ipo mifuko mingi tu, yaani unaweza kwenda kuchukua fedha na kujenga na baadaye ukarejesha fedha kwa muda ambao mtakubaliana. Kwa hivyo, hilo ni suala ambalo linahitaji utekelezaji tu na wala halina tatizo lolote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikimalizia suala la Baraza la Wawakilishi sasa nataka niingie suala nyeti kuhusu Muungano. Kwa kweli kidonda chetu kinachotuuma ni hiki. Mhe. Spika, kama alivyosema mtaalamu wa Kambi hii ya *Backbenchers* kuna wataalamu wa ngazi mbali mbali. Kwa mfano, tunaye mtaalamu wa masuala ya Katiba na mambo ya nje Mhe. Ismail Jussa Ladhu ndiye anayechukua dhana hiyo na wengine wapo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, alizungumza asuhubi na mimi naomba niungane naye kwamba tatizo letu tuachane na kudondoa hizi vijikero na pachi ndogo ndogo. Tatizo la msingi la muungano wetu ni mfumo wa muungano wetu, yaani huu mfumo wa muungano wetu ndio tatizo na tufike pahala tujadili tatizo na wala tusijadili mambo madogo madogo. *(Makofi)*

Katika hili Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwenye kitabu chake cha bajeti ukusara wa 39 ametuelezwa na naomba kunukuu Mhe. Spika.

Ukurasa wa 39 kifungu (g) kinasema hivi:-

"(g) Kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia (*SMT*) itasimamia ufunguwaji wa Ofisi za Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) na Tume ya Mionzi".

Mhe. Spika, suala hili sisi tunalipinga kwa sababu mambo haya tumeshachoka nayo na haya ambayo tunayo tuendelee kuwa nayo na yaliyokuwa yako huko

kupiganie tuyapate wenyewe na wala tusichukuwe mapya na kwenda kuyasokomeza huko, yaani tusiyapeleke tena huko. *(Makofi)*

Hivi sasa Zanzibar mambo ya Sayansi na Teknolojia si mambo ya Muungano na ikiwa si mambo ya Muungano kwa nini tusifanye sisi wenyewe hapa. Kwa maana hiyo, hivi sasa tunayo kila sababu ya mambo haya kujifanyia wenyewe na wala tusichukue tena na kwenda kuyapeleka huko na kuja kutuletea matatizo na kutatua mambo ya makero.

Mhe. Spika, tatizo la *General Budget Support (GBS)*. Mhe. Spika, niungane na Mhe. Ismail Jussa Ladhu wakati alipoeleza kwamba lazima tufike pahala katika mambo haya ya kuzungumza na wafadhili Zanzibar wenyewe ifanye kazi hiyo.

Kwa kweli ifanyekazi hiyo, kwa sababu laitani kama tutapitia mgongo huu wa Muungano, yaani Serikali ya Jamhuri Muungano kuzungumza na wafadhili, basi mara nyingi watu hawa wanakuwa na masharti yao. Sasa iwapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano haito-*meet conditions* watakazopewa na wafadhili maana yake kusema kuwa 4.5 yetu tutaikosa.

Mhe. Spika, hivi sasa sisi Zanzibar inaelekewa kwamba mambo ya rushwa pamoja na ufisadi tunapambana nayo, lakini wenzetu huko wanayo mashaka yao. Kwa hivyo, isijekuwa mashaka yao wakatuambukiza na sisi na kutuathri. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, naunga mkono hoja kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hivi sasa iandae utaratibu wa kuwasiliana na wafadhili moja kwa moja katika kuipata hii *General Budget Support* ya kila mwaka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna tatizo ambalo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amelizungumza kuhusu ushuru. Kwa kweli sijui mambo yanakwenda vipi, kwa sababu ukija serikalini unaambiwa suala hili tayari tumeshalikamilisha, lakini ukenda katika hali halisi bado tatizo lipo na hili lipo pahala gani. *(Makofi)*

Tatizo la wafanyabiashara wetu kutozwa ushuru mara mbili bado lipo. Mhe. Spika, katika hili Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na viongozi wengine msidanganywe na wala wewe usidanganywe kwani wewe si mtu wa kudanganywa. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Makamu wa Pili wa Rais suala hili lichukulie hatua mwenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika kulipatia ufumbuzi suala hili Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nadhani ni vyema awaite watu na awasikilize na wala tusikae tu maofisini na kuletewa habari, kwa sababu habari nyengine ni za kupotosha na wala sisi

hatutaki wakubwa wetu wapotoshwe. Kwa hivyo, ni vizuri kusimima mambo haya. Sasa tunachokizungumza ni tatizo la wafanyabiashara wetu kutozwa ushuru mara mbili bado lipo. Kutokana na hali hiyo, tunaomba lichukuliwe hatua. *(Makofi)*

Suala jengine ni kuhusu Zanzibar na kujiunga na Jumuia za Kimataifa. Mhe. Spika, Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*) alikwenda Lome hivi karibuni, yaani ni Togo. Kwa kweli Togo ni nchi ambayo waislamu hawafiki hata mia moja na wala sikupata kuwahesabu, lakini kwa taarifa nilizopewa hawafiki mia moja.

Kwa hivyo, zaidi ya asilimia 50 ya Watogo ni watu wanaoabudu milima, majabali na maji na asilimia ndogo sana ndio Wakiristo. Pamoja na hali hiyo Mhe. Spika, Togo ni mwanachama wa Jumuia ya *OIC*. *(Makofi)*

Sasa ikiwa wao wanafanikiwa na hilo na mifano iko mingi tu wenye sifa kama hizo, kwa nini Zanzibar tusiwe mwanachama wa *OIC*, tatizo liko wapi. Mhe. Spika, Wazanzibari pamoja na Wawakilishi wa Wazanzibari tunataka Zanzibar ijiunge na Jumuia ya *OIC* na wala hakuna sababu ya sisi kutokujiunga na Jumuia ya *OIC*. *(Makofi)*

Kwa kweli sijui mnataka tufanye tuitishe maandamano, ili muone kweli Wazanzibari wanataka hivyo au tufanye nini maana yake ili muamini kwamba Wazanzibari wanataka kujiunga na *OIC*. Hivi ni kitu gani ambacho kinatuzuia kujiunga na jumuia kama hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi sasa tunataka kauli rasmi ya serikali juu ya Zanzibar na kujiunga na *OIC*, kwa sababu hatuna sababu yoyote ya kutokujiunga na Jumuia ya *OIC*. *(Makofi)*

Suala jengine ni kwamba tunaelekea kwenye Jumuia ya Afrika ya Mashariki. Kwa kweli ni vyema maana yake tunalo tatizo na tunataka kujitia tena kwenye tatizo jengine, kwa sababu hili bado halijamaliza tunataka kujitia kwenye matatizo mengine. Mhe. Spika, kwa bahati mbaya sana tukeshajitia huko basi ile nafasi ya kuzungumza sisi kama sisi itakuwa haipo tena, tutazungumza na nani wakati ndugu yetu hakutusikiliza, hivi ndugu wa mwenzetu atatusikiliza vipi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunataka Zanzibar ijiunge katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki na Mhe. Ismail Jussa Ladhu amezungumza hapa kwamba mambo mengi yaliopo si mambo ya Muungano, isipokuwa ni ya Zanzibar na nani atatuwakilisha kule, mbona tunataka kuvunja Katiba mchana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunatoa rai kwamba tumalize matatizo yetu kabla hatujajiingiza kwenye tatizo hili. Kwa hivyo, tunaomba sana tumalize matatizo yetu kabla hatujajiunga, yaani kabla hatujajiingiza kule na itakuwa hatuwezi kutoka tena. Kwa maana hiyo, lazima tujiunge Zanzibar kama Zanzibar katika Jumuia hii ya Afrika ya Mashariki. *(Makofi)*

Kwa kweli wenzetu au ndugu zetu hawana nia njema katika hili. Mhe. Spika, kwenye mkutano ule wakati tulipokwenda kule Mdhibiti Mkuu na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali alilalamika kwamba Zanzibar tunayo Bendera, Katiba, Serikali, Baraza letu la Wawakilishi, Mahakama Kuu, yaani Zanzibar tunavyo vigezo vyote vya kuweza kujiunga na Jumuia hizi za Kikanda.

Mhe. Spika, yule Rais wa *AFROSAI* ambaye ni Mdhibiti Mkuu na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ya Afrika ya Kusini, akapita pembeni na kusema msiseme hivyo ni wenzenu wenyewe ndio hawalitaki hilo. Kwa kweli sisi tupo tayari kuwapokea katika Jumuia hii, lakini wenzenu hawataki na wakati huo huo na sisi tukachomeka pale, tukamwambia Katibu Mkuu wake ambaye ni Mzambia na sisi *PAC* tunataka tuiunge na *SADCOPAC*.

Mhe. Spika, alituambia tusijekusema kwa sababu Raymam akawasikia, kwa sababu hawataki. Kwa hivyo, jambo la msingi andikeni barua na wala hiyo barua msiwaandikie wao, isipokuwa muniandikie mimi na wao muwatilie nakla tu. Mhe. Spika, hiyo ndio Zanzibar na huo ndio Muungano ulivyofikia.

Kwa kweli wenzetu wa damu hawa ndio ambao hawataki na wala wenzetu wengine ambao si ndugu zetu wao wako tayari kutupokea. Lakini wenzetu kadri tunavyojipapatua hawataki Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaomba Serikali ya Awamu ya Saba chini ya Jemedari Shupavu Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein pamoja na Majemedari wasaidizi Masarahangi hawa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad pamoja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi hili tatizo tulimalize. *(Makofi)*

Kwa hivyo, linalowezekana leo limalizwe leo. Kwa kweli haya matatizo yako pahala gani, maana yake kila siku sisi tunazungumza matatizo na makero, yaani miaka nenda rudi na wengine wazee tunakufa hatumalizi inakuwaje. Mhe. Spika, watu tunazungumza lugha moja, chama kimoja, itikadi moja pamoja na sera ni moja, hivi kwa nini hatuelewani na kuweza kumaliza mambo na kuendelea mbele na tatizo nini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaomba sana haya mambo yamelizike, ili Zanzibar ifadike. Kwa kweli tunachokihitaji hasa ni kuona ndani ya kipindi cha miaka mitano hii kile kitu kinabadilika. Kwa maana hiyo, miaka mitano hii tunataka tuone kipimo sahihi ya kubadilisha mambo ndani ya Zanzibar yetu, linalowezekana leo, basi lazima lifanywe leo. *(Makofi)*

Mwisho kabisa Mhe. Spika, naomba kumalizia kwa kuuliza tu, kwamba Muungano wetu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alitueleza hapa kuwa ipo Idara inayoratibu Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Moja ya kazi inayofanya ni hizi Sherehe za Muungano.

Mhe. Spika, Muungano huu ni nani na nani walioungana, mbona siku ya Sherehe za Muungano wanaoingia katika Sherehe pale kwa mbwembwe ni Rais wa Jamhuri ya Muungano na Mkuu wa Majeshi, hivyo kweli Muungano huu ulifanywa na Mhe. Rais wa Jamhuri na Mkuu wa Majeshi. Kwa kweli tungeona fahari kubwa ya Muungano wetu laitani kama Rais wa Jamhuri ya Muungano angeliingia na Rais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, na mimi kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai na kuwa wazima na kuweza kufika katika Baraza hili, kwa ajili ya kuwatumikia wananchi kwa miguu yetu bila ya kukamatwa mikono. Kwa kweli hii ni dalili ya uzima na hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa hili.

Pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kusema machache katika Hotuba hii ya Bajeti ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kumteua Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Vile vile akamteua Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Spika, tukiwakusanya wote watatu pamoja na wewe Mhe. Spika, utaona wote nywele na ndevu zao tayari zimeanza kubadilika, yaani zimekuwa nyeupe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ishara hii wale wazee wenye hekima unapomkuta mtu anaanza kubadilika nywele basi hiyo ni dalili ya busara. Kwa hivyo, serikali yetu inao watu watatu ambao wenye busara nyingi. Kwa maana hiyo, tunatarajia basi huenda mambo yetu yakawa mazuri sana katika Awamu hii ya Saba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninayo mambo mengi kidogo lakini nitajaribu kwenda haraka ili nisichukue muda mkubwa sana. Nikianza mchango wangu kwenye ukurasa wa 8 Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ametuhadithia kuhusu habari ya kuimarisha Muungano, naomba nimnukuu kidogo Mhe. Spika.

Ukurasa wa 8 kifungu cha 18 kinasema hivi:-

> "Mhe. Spika, Muungano wa Tanzania na Zanzibar ni urithi wa taifa letu, hivyo, hatuna budi kuuenzi, kuulinda na kuuimarisha kwa maslahi ya pande zote mbili za Muungano".

Mhe. Spika, sasa hii kwa maslahi ya pande zote mbili za Muungano *underline*.

Kwa kweli hatuwezi kuepuka Muungano kama alivyosema Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwamba ni urith wetu wa siku nyingi, tayari tumeshachanganyika sana, *tumeshastakim* katika maeneo yote ya Muungano wetu, yaani watu wa pande zote. Kwa hivyo, hatuwezi kusema tuuepuke Muungano, lakini kwa sharti kwamba lazima uwe unaleta maslahi kwa pande zote mbili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hata ndoa ya mtu mmoja na mkewe nyumbani, ikiwa itatawaliwa na kero nyingi basi ndoa hiyo kuna hatari siku moja kuvunjika. Sasa Mhe. Spika, kero zimekuwa nyingi katika Muungano wetu na hii ni nyimbo ya kila siku. Kwa mfano, tumeseme sana na hivi sasa ni mwaka wa kumi tunazungumza kero, kweli zipo kero ambazo zinapatiwa ufumbuzi lakini kuna kero nyengine ni sugu na hizo si kero tena. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama sikosei nakumbuka Mhe. Mohammed Ali Salim alisema siku moja kwamba kero ikeshakuwa sugu si kero tena na hilo ni tatizo, hivyo Mhe. Spika tatizo hutatuliwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ninayo mambo mawili matatu ambayo nataka niyataje na juzi nilisema hapa Mhe. Spika. Kwanza tatizo la wafanyabiashara wetu kutozwa kodi mara mbili hili ni tatizo na wala sio kero tena. Kwa kweli tumelizungumza mara nyingi viongozi wetu wamekutana mara nyingi katika kulitatua hili lakini pamoja na taarifa ya balozi kutwambia kwamba hili jambo limepata ufumbuzi nimeona pahali humu ukurasa wa 10 kwenye *paragraph (b)* kaeleza namna hili kero limeshatibiwa.

Mhe. Spika, hili suala bado lipo wakubwa wakikutana huko wanakubaliana mambo lakini wanakubaliana hapa kwenye ulimi hayamo ndani ya nafsi zao. Juzi nilikutana na mfanya biashara mmoja akanihadithia kwamba ana wiki tatu sasa hivi anasota mzigo wake upo pale bandarini Dar es Salaam wala hakuna

sababu yoyote ya kufanya hivyo, sina haja ya kuirudia lakini ni kielelezo wakubwa wengine hurudi kwa watendaji wakaja wakawaambia msimamo ni ule ule, na kwa msingi huo Mhe. Spika, hili halifiki mwisho.

Sasa mimi nilikuwa naomba ndio nikasema hata ndoa ikitawaliwa na kero nyingi siku nyengine inaweza kuvunjika, mimi nilikuwa naona Mhe. Balozi wakati umeshafika sasa ZRB hapa ipo, katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini haikuweka *formula* kufanya jambo litoke ndani ya muungano kwa sababu ili jambo liingie kwenye Muungano kule bungeni linahitaji *two third majority* wabunge wa kule Tanzania Bara wakasema labda mafuta yasiwe ya Muungano hawasemi kwa sababu kwao ni hasara.

Sasa ni changamoto ambayo imo katika katiba yetu na mimi nilikuwa nadhani fursa tunayo sasa hivi kwa sababu kuna mdahalo huu wa kufanya mapitio ya katiba na kuiandika upya. Hili lazima Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe,. Spika waliangalie vizuri tuwe na *formula,* kwa sababu mambo ambayo yako katika muungano ukiangalia yote haya yanatudhalilisha sisi Wazanzibari. Sasa tufike pahali tukiona hili halifai tuwe na *formula* itakayowezesha kulitoa.

Kuna jambo jengine hili la *OIC* wenzangu wamelizungumza na mimi naomba nilizungumze kidogo tukumbuka kule nyuma kuna wakati Zanzibar walijiunga na *OIC* lakini tukapigiwa makelele kweli kweli tukaambiwa tumevunja katiba zogo na balaa mpaka tafrani ikaingia hapa nchini, hatimae kimya kimya Zanzibar ikajiondoa kwa sharti kwamba Tanzania sasa itajiunga na tutapata faida sote. Sjui kwa misingi ipi lakini mpaka leo huu ni mwaka wa kumi na tano kama sikosei bado Tanzania haijajiunga na *OIC* na huku wametuwekea mguu tusijiunge. Shirika la *OIC* ni shirika kubwa duniani na shirika ambalo linasaidia nchi masikini sana kama sisi waafrika wenzetu wameshafaidika sana kwa *OIC*. Lakini sisi bado mpaka leo linawekwa katika kero za Muungano.

Wenzangu wamesema hapa mimi nafikiri sasa wakati umefika wa kuyaangalia mambo haya katika mtizamo maalum, mimi nadhani Mhe. Spika, nimshauri Mhe. Makamo wa Pili wa Rais afanye mazungumzo sasa na *OIC* na tujiunge. Kwanza kujiunga kwetu kule ni kwa faida za kiuchumi ambazo sio jambo la muungano kwa nini tusijiunge.

Jambo la tatu katika kuimarisha Muungano ni kuondoa hizi kero za Muungano Mhe. Spika, mimi juzi nilisikitika na leo ninasikitika tena, Baraza lako tukufu lilikaa tena kwa umakini mkubwa sana likaamua na kuyatoa rasmi kwa niaba ya Wazanzibari mafuta katika muungano, na siku ile tulipofikia maamuzi yale hatukuamua kwamba hili lipelekwe kwenye kero za Muungano. Sasa huko pembeni pembeni nimesikia kwamba hili limo kwenye kero za Muungano,

hapa tafsiri yangu nini. Tafsiri yangu kwamba maamuzi ya Baraza hayakusikilizwa au Mhe. Balozi atwambie kwamba hizi tetezi zilizokuwepo sio za kweli halimo katika kero, Mhe. Spika, si sahihi suala la mafuta ambalo limeshaamuliwa na chombo kama hichi halafu likawekwa tena kwenye mjadala. Mimi nilikuwa nadhani katika kujinasua hali yetu ya kiuchumi ni mbaya na kwa kweli tumenasa na pakutokea hatuna. Nafikiri njia ya mkato ni kuchimba mafuta yetu mafuta tunayo tusiyakalie alisema juzi Waziri wa Fedha hapa mafuta yetu tunayo na tusiyakalie, sasa tuondoke pale tulipokaa na tuyafanyie kazi.

Katika ukurasa wa 40, 41 na 42 Mhe. Makamo wa Rais katuhadithia au katupa mafanikio aliyoyapata katika ziara zake zile za nje, mimi nilikuwa namuomba sana ajiandae kufanya ziara tena kwenda kutafuta makampuni na kufanya nayo mazungumzo kuja kuchimba mafuta ndio lililobakia Mhe. Spika, sidhani kama tukiendelea kuchelewa tutaumia sana.

Mhe. Spika, niende ukurasa wa 13 pale kuna maelezo kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi, hili ni jambo muhimu sana kwa sababu wananchi wetu hali zao ni duni sana na serikali imejaribu kulizingatia hili katika upeo mzuri, lakini katika utafiti wangu mdogo niliofanya ni changamoto kwa huu uwezeshaji na namuomba sana Mhe. Waziri wa uwezeshaji ayazingatie vizuri, kwanza watu wetu hawana taaluma kwa kile ambacho wanakusudia kukifanya na kwa sababu hawana taaluma nacho hakiendelei.

Lakini la pili mitaji wanayopatiwa kama kwa njia ya mikopo au misaada na vyenginevyo lakini huwa ni midogo sana, sasa ukiyachan'ganya yote mawili kwanza mtu hana taaluma lakini halafu ukampa mtaji mdogo Mhe. Spika, haendelei na ndio pale inapokuja watu wanakopa lakini uwezo wa kurudisha mikopo hiyo haupo. Tumeelezwa hapa juzi mfuko wa JK na AK karibu asilimia 50 watu hawajarudisha ile mikopo waliyochukua, sasa yanayotuathiri ni haya, mimi nafikiri taaluma ni kitu muhimu kweli kweli Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Kiuchumi afanye kazi kubwa kweli kweli ya kuwawezesha wajasiliamali ili kile watakachokifanya wakifanye kwa uhakika ili ziwaletee tija.

Jambo jengine naomba niende kwenye miundo mbinu ukurasa wa 16, miundo mbinu ni jambo muhimu sana katika kukuza uchumi, hapa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais katueleza vizuri sana wanalenga kutengeneza barabara hata zile zinazounganisha watu katika maeneo ya uzalishaji, sasa naomba nikumbushe jambo moja tu Mhe. Spika, kuna kijijji kimoja kinaitwa Ngomeni si maarufu sana hicho kijiji. Lakini nataka niseme kule Pemba kama utafanya utafiti basi mikarafuu iliyopo imara na inayotoa matunda mengi basi ni iliyopo huko katika

kijiji cha Ngomeni, nathubutu kusema karibu asilimia thalathini ya karafuu zinazozalishwa Pemba sasa hivi zinatoka Ngomeni wana kipande cha barabara kutoka pale Kuyuni mpaka kufikia hapa Ngomeni, kuna kipande cha barabara kama kilomita mbili mpaka tatu hivi ni kibaya sana ikinyesha mvua ndogo huwezi kwenda hata kwa miguu. Nilikuwa naiomba sana serikali waangalie kule hasa kwa kuwa kuna uzalishaji mkubwa wa karafuu na sio karafuu tu hata ndizi naomba hili walichukue.
Mhe. Spika: Mheshimiwa bado dakika tano.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, naomba niende ukurasa wa kumi na tatu haraka haraka kabla sijaunga mkono hoja pale kuna matumizi ya ardhi, ardhi yetu ni ndogo sana kiasi ambacho wataalam wanasema ukiigawa sasa hivi kumpa kila mtu hawezi kupata mita saba, sasa kama haikutumika vizuri na humu tuna mpango wa kuzalisha tuna mpango wa kujitosheleza kwa chakula lakini maeneo ambayo ni ya kuzalisha chakula ndio maeneo ambayo watu wanafanya makaazi ya kuishi, kuna ukanda wa Makaani ambao kwa chakula sio mzuri lakini kule hakutumiki kwa nyumba za kuishi sasa nilikuwa naomba sana serikali iangalije japo kama ni mtizamo wa muda mrefu. Lakini kuweza kufikia pahali tukaishi kule ambako hatuwezi kuzalisha tukaacha ardhi hii ambayo tunaweza kuzalisha ili tuitumie kwa kuzalisha.

Mhe. Spika, kuhusu madawa ya kulevya ukurasa wa 27 hii ni hatari sana na ni jambo ambalo linatumalizia rasilimali watu kwa nguvu kubwa sana vijana wanateketea kwa madawa ya kulevya. Nataka nitoe pongezi kidogo kwa serikali kupitia jeshi la polisi kule jimboni kwangu kuna kijiji kinaitwa Pujini na ndiko ninakokaa mimi, Pujini siku hizi imekuwa maarufu sana kwa bangi Mhe. Spika, vijana wanavuta bangi sana na matokeo yake uhalifu umekuwa mkubwa kupindukia. Watu wa Pujini sasa hivi hawana hamu ya kufuga kuku, mbuzi wala ng'ombe wala hawana hamu ya kulima kutokana na vijana hawa. Sasa hivi karibuni nimeona polisi wamekurupuka kidogo naomba uwekwe mkazo watu wa Pujini wanasema hawataki bangi iingie tena kule.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nataka nizungumze kuhusu miradi ya maendeleo ya jamii na hii nigusie TASAF kidogo, TASAF imesaidia sana katika kufikisha maendeleo kwa jamii zetu hasa kule ndani ndani ambako macho ya serikali hayaoni kwa wepesi, nilikuwa naomba hii miradi iendelee na iwe na uratibu wa karibu zaidi. Nina wasi wasi Mhe. Makamo wa Pili wa Rais lile fungu la pesa linalotolewa kwa ajili ya mradi fulani ukienda kuangalia na kile kilichofanyika unaweza kupata wasi wasi kidogo.

Halafu mwisho nizungumzie habari ya *CDF* kidogo hiki ni kitu muhimu sana kwa maslahi ya watu, Mhe. Spika, wewe utakuwa shahidi mara moja

tulikwenda kufanya utafiti kwa wenzetu Kenya wanatwambia mfuko huu wa *CDF* maendeleo ambayo wamefikia kwa muda wa miaka saba tu yanashinda maendeleo yaliyofikiwa kwa miaka 40 ya uhuru, sifa ya *CDF* inakwenda moja kwa moja kwenye *priority* za wananchi hasa vijijini, sasa nilikuwa naomba sana mfuko uimarishwe na ikiwezekana upate fungu kubwa zaidi la fedha na wala isitiwe wasi wasi kwa sababu watu wamekuwa na wasi wasi kwamba mfuko huu utakuwa unamsaidia Mbunge zaidi au Muwakilishi. Mimi nafikiri tukiweka taratibu zetu vizuri Mwakilishi au Mbunge atakuwa haugusi huu mfuko, mfuko una wenyewe ni wananchi wa jimbo maalum kuna kamati za maendeleo ndio wanaokaa kupanga vipaumbele, labda kazi yake muwakilishi ni ndogo sana kuwakilisha tu lakini utumiaji wa pesa hautamhusu Mwakilishi na utawahusu wananchi wenyewe kupitia kamati zao za majimbo. Sasa nilikuwa nadhani ni kitu muhimu na watu wasikifanyie wasi wasi kitawasaidia wao wenyewe katika kiwango kikubwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache mimi naunga mkono hoja mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii nikatoa mchango wangu mdogo kuhusiana na bajeti hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima na mwelekeo wa kuchangia katika bajeti hii. Pia namshukuru Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa bajeti yake ambayo imekwenda katika maudhui mara baada ya kuchaguliwa kwake, ziara zake anazofanya katika maeneo mbali mbali pia tunapongeza juhudi za ivongozi wetu watatu kwa kuanza kuitangaza Zanzibar katika ulimwengu na kuweza kuipatia misaada na michango mbali mbali kutokana na wenzetu. Mhe. Rais mwenyewe, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kama alivyojieleza mwenyewe katika kitabu chake. Mhe. Spika, tuna miezi minane tu sasa hivi lakini kuna dalili nzuri kwamba mwelekeo wetu utafikia pahali pazuri.

Mhe. Spika. juhudi zetu za viongozi wetu wakuu pamoja na Mawaziri na wananchi kwa jumla zina vikwazo hilo ndio tatizo moja kubwa, vikwazo hivi huwezi kuelewa kwa nini viendelee hata katika jamii mzee akimuona mwanawe anatabika humpatia nyenzo ili ziweze kumsaidia, lakini huwezi kumkuta mwanao au jamaa yako au rafiki yako anateseka na wewe ukamsaidia kumtoa roho. Serikali ya Jamhuri ya Muungano haiisaidii Zanzibar na maneno haya ninayosema hapa mimi niliwahi kusema mbele ya Gavana wa BOT mbele ya Kamishina wa TRA, na ni sehemu ya nchi mmoja ya Jamhuri ya Muungano na wao tumeungana nao hata kama sisi tulikuwa tunateleza wao ilikuwa watusaidie ndivyo zinavyokwenda nchi zilizoungana. Lakini licha ya kwamba sisi hatutelezi lakini wanatutelezesha halafu wakatukwamisha,

Mhe. Spika, suala langu la mwanzo nilimuuliza Mhe. Waziri huyu huyu Makamo wa Pili wa Rais hii Zanzibar ikienda katika mazungumzo ya Muungano kikatiba inawakilishwa na nani, jibu sasa hivi hii inaitwa *marriage of convenience* huu Muungano wetu sasa hivi tunauita *marriage of vonvenience* kwa sababu Rais kajichukulia madaraka ya kuteua watu wa kwenda kutatua matatizo, si kweli Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema Mahakama maalum ya katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Lakini la pili ilipoondoshwa nafasi ya Makamo wa kwanza wa Rais kuwa Rais wa Zanzibar tumeondolewa nguvu za kwenda kuzungumza kikatiba tunakwenda pale kujipendekeza tu na kuwashauri wenzetu wakikubali basi hawakukubali basi, si kweli hatuna uwezo wa kikatiba katika mazungumzo yale tulikuwa na uwezo wa kikatiba alipokuwa Makamo wa Kwanza wa Rais ni Rais wa Zanzibar. Mimi nilizungumza na wazee waliokupo katika Afro Shirazi walishuhudia kiongozi Marehemu Mzee Abeid Amani Karume amemuita Zanzibar Waziri wa Fedha nae Marehemu Ameir Jamar kwa suala ambalo lilikuweko, akamwambia baada ya leo nitakufunga hapa hapa Zanzibar ukisema maneno hayo alitumia njia yake ya kwamba yeye ni Makamo wa Kwanza wa Rais na alikuwa na uwezo wa kikatiba kumuita Waziri aliyiekuwemo ndani ya ile Wizara za Muungano.

Sasa leo sisi Rais wetu ni Waziri asiye Wizara maalum katika Muungano atakayemuita nani, ndio nikasema hapa naunga mkono sana maelezo aliyosema Waziri wa Katiba na Sheria kipindi hiki kujitafutie yale mambo ambayo tumeteleza au yamekosekana katika kuudumisha huu muungano, kila mmoja anataka udumu huu muungano kwa sababu katika ulimwengu hatuwi kuishi peke yetu lakini tuwe na muungano uliokuwa wa uhakika. Muungano uliokuwa wa uhakika jambo la mwanzo tupate kiongozi wa kikatiba atakayekwenda kuiwakilisha Zanzibar ndani ya Muungano hilo la mwanzo.

La pili hata yule mshauri wa mafuta aliyekuja yule haitakiwi kwa nini viongozi ndio wanaojifanya kwamba wa Mahakama, mfano sisi tulipokuwa tukijadili kwamba Zanzibar ni nchi au sio nchi viongozi wakuu ndio waliojibu, wakati katiba ya jamhuri ya Muungano hii hapa, sehemu ya saba ukurasa 106 kutakuwa na Mahakama maalum ya Jamhuri ya Muungano ambayo mamlaka yake muundo wake na sehemu ya shughuli zake ni kama ilivyoelezwa katika vifungu vifuatavyo. Na humu mmeelezwa nani watakaokuwa *component* sawa sawa majaji sawa sawa idadi baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, hii inaeleza humu humu na wanasema hasa kama jaji mmoja tu hayupo basi kikao hakipo lakini sasa katiba inakiukwa sisi tunakwenda kufanya vikao vya kubembelezana. Kwa hivyo Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Makamo wa

Rais yale maradhi makubwa tuliyokuwa nayo hilo ndio nilikuwa nataka kulisema.

La pili Mhe. Spika, ninalotaka kulizungumza ni suala la shughuli za kuratibu katika shughuli za serikali kama ilivyotajwa katika kitabu chake hichi, moja katika shughuli kubwa ya Ofisi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ni uratibu wa shughuli za serikali, sasa inaelekea wizara nyingi zinafanya kazi peke yake peke yake haidhuru tunasikia kuna vikao vya makatibu Wakuu. Lakini kwa sababu sisi hatujaingia katika hivyo vikao hatujui kinachozungumzwa, lakini tukienda katika ukaguzi katika shughuli za kamati unaweza kuona hasa suala hili lilikuwa lizungumzwe baina ya Wizara hii na Wizara hii kwa nini linafikia kiwango hichi halijatatuka.

Kwa hivyo tunamuomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kuziunganisha hizi Wizara ili lengo likawa moja, kwa mfano utakuta kwamba kuna Idara ya Ardhi ina viwanja inavyotoa kwa wawekezaji, lakini ile idara ya Uwekezaji ambayo ni ZIPA ina maneno mengine na hawa wanaokuwa na Wizara ya Ardhi wana maneno mengine, kila mmoja anasema sivyo ambavyo mwenzake anavyo na ukiitizama hakuna tatizo kubwa. Kuna ukatikanaji wa mawasiliano baina ya Wizara zetu na hivi hatutokwenda kwa sababu hii serikali ni kitu kimoja. sisi wizara katika lugha ya kiarabu Waziri ni mshauri, kwa hivyo Wizara ni chombo cha ushauri katika serikali katika yale mambo yaliyokabidhiwa sasa anayeshauriwa atakuwa ni mmoja tu Mhe. Rais kwa hivyo inaonyesha wote wale wakimshauri vilivyo hatoteleza Rais, kwa hivyo tunaziomba sana shughuli kama hizi ziweze kushughulikiwa.

Hapa pametajwa kuwa msemaji mkuu wa serikali. Hapa kidogo naomba aje atufafanulie wakati atakapokuja. Yeye mwenyewe ndiye msemaji mkuu wa serikali au kuna ofisa ambaye ameteuliwa kuwa msemaji mkuu wa serikali. Kwa sababu kama Marekani kule tunaona likitokezea jambo mtu anayetoka *White House* anakwenda sio Rais, anakwenda kusema mambo yaliyotokea.

Hii kwa sababu kuna baadhi ya waandishi wa habari wameni–*approach* mimi wakanambia kwamba wanapata tabu sana likitokezea jambo kumpata msemaji mkuu wa serikali. Tunataka utueleze kidogo linapotokea jambo la nchi msemaji mkuu wa serikali ni nani na wananchi wasikie kutoka kwa nani.

Mhe. Spika, nimeona katika ukurasa wa 32 - 33 moja katika shughuli za Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ni Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Mimi kidogo nina maneno hapa. Sherehe kwa maana yake ni kufurahia jambo, lakini Waswahili wanasema “Mno wadhuru” Mimi hapa Mhe. Spika, kama

ulikuwepo wewe siku ile nilimpa ombi langu Mhe. Waziri wa Elimu, nikamwambia 2014 Zanzibar itaadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi matukufu.

Kwa nini basi hatuweki lengo la kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu, kila kijana wetu akakaa juu ya kiti skuli au juu ya deski. Hapa namuuomba ofisi ya makamo wa pili, tukate sherehe kubwa kwa madhumuni tuje tushereheke sana. Naomba sana Mheshimiwa, watu hawatufahamu tukisema kuwa hatuna pesa halafu tukafanya sherehe kubwa, wananchi wetu wenyewe hawatufahamu. Hebu tukateni kidogo, tuweke sherehe ndogo 2012, sherehe ndogo 2013, lakini 2014 kwa sababu miaka 50 tutayarishe bonge la sherehe lakini kila kijana wetu awe amakaa juu ya kiti chake au deski lake maskuli. Hapa sote pamoja na wananchi wetu tutawapongeza na tutachangia siye hizo sherehe za Mapinduzi ili zifanyike.

Mhe. Spika, suala ambalo la mwisho nitakalolizungumza ni usemi uliotoka kwa mchumi mmoja. Juzi nilipokuwa nikichangia bajeti ya serikali ilikuwa *point* hii niiseme lakini kama ulivyojua Mhe. Spika muda wangu ulikuwa muda wa kumalizia. Lakini leo nataka niliseme. Mchumi mmoja alisema au aliulizwa au aliulizwa hebu tueleze kwa nini jumuiya yetu. Wanayo jumuia sitaki kuitaja, maana nikiitaja hapa ndio nitachomoa kile kidogo cha OIC. Ikiekeza katika nchi huwa ina vigezo gani. Sasa naomba niitaje leo kwa kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili auone ule uzito.

Mhe. Spika, wenzetu wanasema wachumi, hawa watu wanaoekeza, yaani wanaofanya *investment* hasa kubwa, mbali ya urasimu ambao upo ambao umewafanya wakaja au wasije, lakini kuna mambo matano wanayatizama.

- Wanatizama viwango vya elimu vilivyomo katika nchi ile wanavyoelekeza. Je, elimu yao wale watu tunaokwenda inatosha kwamba kazi zetu zitafanya wafanyaji. Wakati sisi tunasema ya kuwa watu wetu waweze kupata ajira.

- Wanatizama bidii ya wale watu katika kufanya kazi wanaweza kujituma kiasi gani. Wanawapima watu kwa *performance* ya ile nchi.

- Kitu kingine wanachokitizama ni ufanisi wa kazi uliokuwepo pale. Je, wale watu wanajua kulifanya jambo mpaka likamaliza.

- Kigezo cha tatu wanasema wanachotumia ni uaminifu uliojengeka miongoni mwa watu wa sehemu ile. Ikiwa watu ni wadokozi sana hawaji.

Mheshimiwa sisi tulitembelea viwanda ni magofu sasa hivi cha magodoro, cha vyandarua n.k. nasikia vitu vilikuwa vikirushwa juu ya ukuta. Magodoro yanatengenezwa watu wanayarusha juu ya ukuta watu wengine wanayapokea upande wa pili. Hamjasikia nyie? Miye Mpemba nimeyasikia je, nyie? Sasa kwa hivi hawaji Mheshimiwa kama hatukujenga uaminifu.

Maana yake nini nikaizungumza hapa, hivi sasa tunataka ndani ya Mawizara tujenge uaminifu. Serikali ishughulikie kwamba kweli watu wamekuwa waaminifuu halafu ndio watu watakuja kuwekeza. Wakituona kwamba sisi ni wezi, *Allahu Akbar*, hawaji. Lazima tujenge watu wetu wawe waaminifu ndio wawekezaji watakuja. Leo tumesikia hapa mtu anakuja kuweke hoteli siku mbili anamkabidhi mwengine. Ni hizo hizo hoteli ndogo ndogo, hao ndio watakaokuja.

Mimi namalizia hapa Mhe. Spika, kwa kuunga mkono bajeti ya Mhe. Makamo wa Rais. Lakini lazima utendaji wetu serikalini ubadilike, ubadilike. Bila ya hivyo tutachukua muda mrefu sana na tutaanza kulaumu kwamba hivi na hivi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika bajeti hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Nianze kwa kumpongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba yake ya bajeti nzuri, ina mtazamo mzuri wa kuwasaidia wananchi na kuielekeza serikali yake na watendaji wake.

Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri wa Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais na watendaji wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kumuandalia Makamo leo hii akatupa hotuba mwanana kabisa.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu niende kwenye suala la Viongozi watendaji na watumishi wa serikali. Kwa kweli suala hili linauzito mimi naliona. Uwajibikaji kwa viongozi na watendaji katika serikali yetu uko duni sana, baadhi ya viongozi wa serikali na watendaji hawawajibiki, lakini sio wote. Hii inatupa mashaka sana kiasi kwamba wananchi wetu wanakosa imani na serikali kwa kutokuwajibikiwa. Maana yake wao ndio wenye ile serikali, lakini wanapofika kwenye ile miyonzi ya serikali wanakuwa kama wao ni watu duni sana kuliko wale waliokuwepo pale. Wakati wao ndio wawe wafalme pale kwa sababu ndio wenye serikali yenyewe waliyoiweka madarakani pale.

Mhe. Spika, hili ni tatizo na lipo kwenye nyanja nyingi sana, kuanzia watendaji wadogo wadogo, wapo wale wa kati na kati na wapo hawa wakubwa kabisa. Inakuwa ni mtihani kweli kweli. Unaweza kwenda kwenye ofisi saa 3:00

unakaa kusubiri, hajaingia ofisini sio kwamba kafika kaondoka, hajaingia kabisa ofisini. Sasa hili ni tatizo. Unaweza kukutana labda na ofisa mdogo mdogo tu. Lakini wale wa ngazi za juu unaowahitaji kwa ajili ya ile shughuli uliyoiendea hawapo. Unaweza ukafika saa 4 mtu hajaingia.

Ukienda kwenye hao watumishi wengine kazi ya kufanywa kwa siku moja, inachukua siku tatu, siku nne haijafanyika. Ukiuliza unaambiwa mtendaji hayupo, labda kaja katoka. Sasa sogea sogea mpaka ufike hapo mchana, akienda kuswali huyo ndio harudi tena, usubiri siku ya pili saa 3:00 tena au 3:50. Sasa kwa mwenendo huu Mhe. Spika, hatufiki.

Mimi ningemuomba sana Mhe. Makamo alisimamie vizuri hili la watendaji. Na hapa asiwakamate hawa wadogo tu aanze kuwakamata hawa wakubwa akiwashika hawa na hawa wadogo watawajibika, maana mkubwa akiwa anawajibika mdogo akimuona bosi wake anaingia kazini saa 1:30 hatokwenda saa 2:30, atakwenda saa 1:15 na yeye ili bosi akija amkute kafika. Mimi nilikuwa nashauri hilo na tujitahidi sana katika hili.

Nije katika suala la utunzaji na usimamizi wa rasilimali za serikali. Hapa napo pana mtihani Mhe. Spika. Rasilimali za serikali hazitunzwi au hazisimamiwi vizuri. Unaweza ukalikuta gari la serikali limetolewa leo hii ukiliona jipya, kaa baada ya miezi mitano 5, 6 ile yako wewe *used*, maana sisi tunanunua *used* tu, serikali ndio inakuwa inanunua gari mpya mara nyingi. Lakini hizi *used* zetu zitakaa, utatunza lakini hii ya serikali iliyonunuliwa mpya baada ya miezi 6 au mwaka mmoja unalikuta limeshagongwa au limeshalala kabisa. Utunzaji wa zile rasilimali haupo na haupo kwa sababu hawasimamiwi hawa. Maana mtu hata mtu kama gari kaligonga hakuna kinachoendelea, mimi sioni kama wanawajibishwa.

Mhe. Spika, nimetoa mfano wa gari tu lakini ni mambo mengi kabisa ya serikali yako hivyo. Hata utunzaji wa majengo ukiutizama uko hivyo. Kuna mali za serikali hapa zinachukuliwa tu na wajanja wachache basi wanauziana wenyewe, utasikia ishauzwa. Ukiuliza sababu ya kuuzwa kwake pengine serikali inahitaji zaidi. Unaweza kukuta kiwanja cha serikali kinauzwa wakati wizara hiyo hiyo yenyewe inatafuta kiwanja cha kujengea makao makuu ya wizara yake. Lakini kiwanja ilikuwa inacho imekiuza. Huku inakwenda tena kuomba kiwanja ili ijenge ofisi yake. Ukiuliza kimeuzwa vipi, hapo shughuli, utaanza kupewa hadithi nyingi mwisho wake utadondoshwa maana yake Wizara ya Fedha basi waliamua, uhakiki mali waliamua huko kwa hivyo sisi wametuletea tu taarifa hapa. Mimi nafikiri kuwepo na usimamizi mzuri juu ya utunzaji wa rasilimali za serikali. Hili mimi ningemuomba sana Mhe. Makamo alisimamie vizuri.

Nije kwenye hili hili suala la uwajibikaji. Mhe. Spika, uwajibikaji umepungua hata ile kasi ya usimamizi wa yale mambo yenyewe ya kiserikali inakuwa ni tatizo. Kwa mfano Mhe. Makamo wa Rais alikuwa kuna kipindi alikuwa anafanya ziara za kutembelea maeneo yanayojengwa ovyo. Akisha alikuwa anatoa maagizo sana nakumbuka nilikuwa namuona katika TV, hapa pavunjwe, hili lisimamishwe, sijui hapa hivi. Lakini kesho na keshokutwa ukenda katika maeneo yale yote, hakuna kilichovunjwa. Ina maana hata ile amri anayoitoa kiongozi huwa haisikilizwi. Utendaji hapa haupo, kwa hivyo hata wale watendaji hawasimamii maagizo ya watendaji wakuu wa serikali.

Mhe. Spika, hili ni tatizo ambalo limo ndani ya serikalii yetu. Ningemuomba sana Mhe. Makamo hawa watendaji wake awaangalie vizuri sana, ajaribu kuwa mkali zaidi awakemee, kwa sababu mtindo huu sio mzuri hata kidogo. Unatia aibu maana wananchi wanaona Makamo anakwenda TV zinakuwepo, anatoa maagizo lakini utekelezaji wa maagizo yale yakufanyiki kitu. Kesho na keshokutwa unamkuta mtu anacheka kabisa anaendelea na shughuli zake. Mimi ningeomba sana hili awe mkali kidogo.

Nije kwenye suala la madawa ya kulevya. Mhe. Spika, suala la madawa ya kulevya ni tatizo, tena tatizo hili ni sugu kweli kweli. Vijana wetu wanaharibika sana kwa suala hilo. Lakini mimi nahisi tutakuwa tunawalaumu bure hawa vijana kuharibika. Madawa haya hayatengenezwi hapa kwetu. Ni lazima yavushwe kutoka nje ndio yaletwe hapa. Mimi naona serikali inajikita zaidi katika kuwazuia hawa watumiaji tu, lakini hawa waletaji vipi na ni watu ambao wanajulikana. Ukienda mitaani sasa hivi ukiulizia utaambiwa aah fulani bwana muuza unga huyo. Na wengine wanakamatwa siku zake mbili utasikia kishindo siku ya tatu unamuona mitaani kama kawaida anadunda na biashara inaendelea.

Mimi nahisi serikali haijawa *serious* katika hili. Igeuze kibao kidogo, isiende kwa hawa walaji tu kuwakamata wale wanaosinzia kwenye vibaraza, igeuze kibao iende kwa hawa waletaji kabisa. Maana kuna waletaji na wasambazaji. Waletaji wanakuwa sio wengi sana maana yake wazito kweli kweli. Wasambazaji ndio wapo wengi kidogo, halafu watumiaji ndio wamezidi. Sasa mimi ningeiomba serikali hapa iende kwa hawa waletaji kabisa. Wanajulikana Mhe. Spika, hata watoto wadogo ukiwauliza mitaani watakwambia. Ukimuliza mtoto namuuliza mtu fulani, mtoto anakwambia aah! yule muuza unga. Sijui serikali inashindwa nini kuwashughulikia watu hawa. Tukiwakamata hawa au tukiwashughulikia hawa waletaji, hili tatizo litapungua au litaisha. Kwa sababu hawa wavutaji wenyewe watakuwa hawawezi kuvuta kama hicho kitu hakipo. Nishauri serikali hapa iwadhibiti zaidi hawa waletaji na wasambazaji.

Mhe. Spika, nisogee katika uwajibikaji wa taasisi za Muungano, kama vile Jeshi la Polisi, Idara ya Usalama wa Taifa, Uhamiaji na Majeshi. Mimi kidogo nahisi kuna tatizo Mhe. Spika. Ule uwajibikaji wao, hawa watu wanawajibika kwa nani. Vile vyombo nilivyovitaja viko hapa vya Muungano hivi, mawaziri wao wapo kule, Makatibu Wakuu wapo kule. Sasa kwa hapa Zanzibar wao wanawajibika kwa nani. Kwa sababu kuna tokezea kesi kwa mfano kama wananchi kupigwa na majeshi mfano. Ikienda kesi siku mbili tatu utaikuta imekufa kabisa. Wananchi ili kufatilia wapi wende inakuwa kidogo pagumu.

Nilikuwa nataka kujua hawa hasa wanawajibika kwa wizara ipi au waziri wao hasa hapa nani. Nilikuwa nataka kujua hilo ili tuone uwajibikaji wao ikiwa kuna tatizo hawa tunajua tunapakaba wapi. Maana Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais inashughulikia na mambo ya Muungano. Sasa sijui ndio wanawajibika kwake au vipi. Tuone kidogo hawa wapi wanawajibika. Maana yake mimi naona Waziri wao Bara, Katibu Mkuu wao yupo kule, na mambo yao yote yanakuwa yanatokea kule. Kwa hivyo kwenye SMZ nahisi wanakuwa kama ni watu ambao wapo pembeni, hata wakifanya jambo kuguswa kwao kidogo kugumu. Kidogo naomba nipate ufafanuzi juu ya hili.

Nije katika changamoto za kitaifa. Kuna jambo humu limezunguzwa. Kuna mdudu mmoja hapa katajwa anaitwa rushwa. Huyu mdudu sugu kweli kweli. Suala la rushwa ni suala gumu kweli kweli, kwa sababu limo ndani ya damu hili naona. Ili mtu afikie mahala kuwa aache hasa hili jambo labda amwagwe damu yote halafu atiwe mpya, iwe haina huyu mdudu, suala hili ni tatizo kubwa katika jamii yetu Mhe. Spika.

Wananchi wetu wanapata matatizo wanapokwenda kutaka huduma lazima watoe kitu kidogo. Watu wa Kenya wanatumia neno hilo utoe kitu kidogo. Na ni hili hili la hawa watendaji au watu waliopewa dhamana katika serikali. Masikini hana sauti kwa sababu hana chochote. Lakini tukumbuke ni wananchi wetu hawa na wao ni masikini mno. Hawana uwezo huo wa kwamba wakupe wewe na akailipie huduma, inakuwa tabu. Na hii haipo kwenye taasisi moja tu ya serikali, karibu taasisi zote zina tatizo hili. Ukisema wenyewe wanakuwa wakali aah hakuna. Lakini kwa kweli lipo, tukubaliane na ni tatizo Mhe. Spika.

Huduma hazipatikana kwa utaratibu ule ambao serikali umeupanga, kwamba mtu anahitaji huduma fulani akienda hapa atapewa huduma hii na hii. Inatajwa tu, itazungumzwa, lakini akienda kama hakutoa kitu kidogo hapati hiyo huduma. Mifano ipo mingi sana Mhe. Spika. Mengine imeshatukuta sisi wenyewe, maana sisi ni viongozi na ndio kwanza tunaingia kwa hiyo wengine hawatufahamu. Unakwenda mtu anakwambia hasa kabisa tengeneza basi kitu

kidogo tumalize. Unashangaa kidogo, mpaka akishituliwa huku tena, anasema duuh! Samahani bwana tena, unajua mambo yenyewe, nikuwa nakutania, sijui nilikuwa hivi. Lakini kwa kweli hili jambo Mhe. Spika, lipo, limeenea mote.

Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Makamo wa Rais hili jambo alivalie njuga kweli kweli. Kwa sababu bila ya hivyo jitihada za serikali zitakuwa hazifikiwi. Jitihada za serikali ni kuwasaidia wananchi wake. Wananchi wetu wanajulikana ni wanyonge mno. Hawana uwezo asilimia kubwa kabisa ni wakwezi na wakulima.

Mhe. Spika, ningeomba sana suala hili likawa ni moja kati ya vipaumbele vya serikali vya kuhakikisha kwamba inalitokomeza ili wananchi wetu waweze kuwa wanapata huduma hizi kama ambavyo serikali yenyewe imewapangia wazipante bila ya kutoa kitu kidogo.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kutoa rai kuhusu jengo la Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Nimechungulia kitabu sikuona kama kuna ujenzi wa jengo jipya labda la Ofisi ya Makamo ya Pili wa Rais. Maana mimi kwa mtazamo wangu kwa hadhi ya Makamo wa Pili wa Rais na jengo analotumia lile linastahiki kwa sasa aondoke. Nimeshawahi kumkuta pale anashuka gari na mvua inanyesha ikawa shughuli pale. Maana inabidi arowe kwanza ndio aingie ofisini. Kwa hadhi yake nahisi itakuwa si sahihi. Mimi nilifikiria kwenye kitabu chake leo hii tungeona ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, lakini badala yake nimeona mwaka uliopita kulikuwa kuna ukarabati wa kupiga rangi na mambo kama hayo. Mimi nafikiria ni vyema tukabadilisha hii tukamuwekea utaratibu mwengine.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi pamoja na wananchi wangu wa jimbo la Mkwajuni naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kunipatia nafasi hii. Awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu (SW) aliyetujaalia uhai, uzima, kutekeleza majukumu yetu haya katika Baraza lako Tukufu kwa nia ya kuwatekelezea wananchi wetu kwa kuwatakia maendeleo ya kweli.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sina budi pia Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kunipatia nafasi hii jioni hii kuweza kuchangia na mimi mawili matatu katika hii hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, naichukua tena nafasi pia adhimu pia kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba yake nzuri iliyojaa hekima na busara na utekelezaji wa malengo yote ya awamu ya saba ya serikali yetu hii katika kipindi cha Bajeti cha Mwaka 2011/2012.

Nikianza kusema niseme Mhe. Makamo wa Pili wa Rais mimi ni Mbunge wangu katika jimbo la Kitope. Hivyo basi inamuelewa vyema Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Namfahamu kwamba huyu ni mtu mahiri, makini na ana uwezo mzuri na anaposhauriwa hushaurika. Nimeuwona utendaji wake wa kufatilia huduma za kijamii na pale alipochangia katika skuli ya Fujoni ambayo wanafunzi walikuwa na matatizo makubwa lakini ameshatusaidia makompyuta na vikalio. Nasema kwamba katika utekelezaji wa majukumu katika serikali hii ya Umoja wa Kitaifa akiwa yeye ndiye makamo wa pili wa Rais ndiye mtendaji mkuu wa shughuli za serikali nina imani kwamba atayatekeleza yote ambayo ameyaahidi katika kipindi cha awamu hii ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo sasa nianze na mchango wangu moja kwa moja. Nianze na ukurasa wa 13 kwenye kifungu cha 27, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, kuandaa utekelezaji wa mradi hasa wanawake na vijana.

Mhe. Spika, nimwambie Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwamba haya mambo yapo, wizara imeundwa lakini kuna matatizo ambayo hujitokeza katika kutekeleza miradi hii.

- Ni kukosa wanawake taaluma pamoja na vijana wa kuiendeleza miradi hiyo.

- Ubunifu wa miradi endelevu ambayo inaweza kuwazalishia na kuwaletea tija na kuwaondolea umasikini.

- Pia wanapatiwa mitaji midogo ambayo inakuwa haiwezi kuwazalishia na kuwaongezea tija.

Hivyo ningemuomba Waziri wa Uwezeshaji kupitia Makamo wa Pili wa Rais watakapoandaa kutoa fedha hizo basi ziwe zimeongezwa na kufanyiwa utaratibu maalum ambao unaonesha wazi kwamba watakapopewa watamudu kweli kuendesha miradi yao na kuweza kujikwamua kweli kiuchumi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu mwengine niende katika sekta ya viwanda na biashara katika ukurasa wa 13 kifungu Nam. 30. Nina imani kwamba serikali hii ya awamu ya saba nimefurahi sana kuona kama Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ameligusa hili neno la viwanda. Mhe. Spika, kwa

upande wangu na wanawake wenzangu tunasema kwamba hii ni faraja ya aina yake. Kulitaja eneo hili la viwanda ni kutwambia kwamba anatutayarishia ajira kwa wale wasiokuwa na kazi, vijana ambao wataweza kuajiriwa katika hivyo viwanda ambavyo vitabuniwa.

Mhe. Spika, katika kitabu chake hiki cha hotuba amesema ni kuvifufua vile ambavyo vimekufa. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais mimi nakuomba ufanye juhudi na maarifa yako yote na kwa ninavyokufahamu hili unaliweza hapana shaka utalitekeleza. Mhe. Spika, utakapofanya hivyo hata wakulima nao watafaidika, wale wanaolima matunda na mazao mbali mbali nao watapata nafasi ya kupeleka katika viwanda hivyo na kuweza kuzalisha mambo mbali mbali na kujiongezea kipato. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Makamo wa Pili hili alisimamia kwa nguvu zake na juhudi zako zote.

Mhe. Spika, nikitoka hapo sasa nije katika ukurasa wa 16 kuhusu utalii na kumbukumbu za kihistoria. Mhe. Spika, Mhe. Makamo amesema kweli kwamba utalii ndio mguu tunaotembelea kwa sasa hivi kwa shughuli zetu kuu za kiuchumi kwa kutuletea pato la taifa. Lakini ule utalii ambao upo wa kihistoria sasa hivi umekuwa unaharibiwa sana. Mhe. Spika, maadili ya Kizanzibari ambayo yalikuwepo yakiwavutia sana wageni wetu waliokuwa wakitoka huko sasa hivi sote na sisi tumebadilika tumekuwa wazungu. Mhe. Spika, tumebadilisha utamaduni wetu, tumeacha mila na desturi zetu ambazo zilikuwa nzuri na walikuwa wakizipenda sana wageni ambao walikuwa wanafika hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, ningependa kumwambia Mhe. Makamo kwamba mimi nina kumbukumbu ya historia zetu ambazo zinapendwa kuna daraja moja linaitwa maji mekundu ambalo Mhe. Balozi analifahamu vizuri katika Wilaya ya Kaskazini "B" katika Jimbo lake la Kitope. Mhe. Spika, daraja hili ni la kihistoria limejengwa tangu mwaka 1927, daraja hili wakati wa miundombinu ilipopita kujengwa barabara mpya limebomolewa. Mhe. Spika, kwa bahati mbaya daraja linabomolewa nilikuwa safarini lakini niliporudi nimesikitika, nilisema ningelikuwepo ningelisema historia hii isingestahiki kuondolewa pale kwani ni moja katika kivutio maana maji yaliyopo katika daraja hilo ni rangi nyekundu. Mhe. Spika, naamini waheshimiwa wengi katika Baraza lako hili tukufu hawalielewi hilo, kwamba kuna daraja lina maji mekundu.

Mhe. Spika, wengi wa wageni wetu walipokuwa wakitoka kuelekea Mangapwani kuangalia historia nyengine basi walifika pale na kuonesha kuwa wamevutiwa mno na hali ile. Kwa hivyo, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais hili jambo la kuzitunza kumbukumbu zetu za kihistoria ni jambo la msingi sana na

nakuomba uliweke katika historia na wananchi walielewe vizuri ili tuweze kujiletea tija na kujikuzia uchumi wetu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo sasa niende katika sekta ya uzalishaji yaani kilimo. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais naamini kwamba umekwenda sambamba na ule mswada ambao tumeupitisha hapa wa uhakika wa chakula na lishe. Ni imani yangu kwamba unataka kumsaidia Waziri wa Kilimo alitekeleze kwa juhudi na maarifa hili lengo na dhamira ya dhana ya chakula na lishe.

Mhe. Spika, naamini kwamba tunaelewa sote kuwa wengi wa Wazanzibari ni wakulima, lakini ni wakulima wa kijembe kongoroka, tena wakulima wenyewe hususan ni wanawake, wengi wa wanaume wanakwepa jukumu la kuzalisha mali kupitia kilimo. Mhe. Spika, wengi wao wameingia katika miradi mengine kwa uhalisia lakini kwa Wilaya ya Kaskazini "B" mheshimiwa atakuwa shahidi kwamba wanawake kwa asilimia 80 ndio wazalishaji wakubwa wa chakula pamoja na matunda.

Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba Mhe. Makamo atakapofanya juhudi ukasimamiwa kwa kina ubadilishaji huu wa kilimo kuletwa matrekta, pembejeo pamoja na vingi kabisa vile kwa ajili ya kukisimamia kilimo hiki. Hivyo ni imani yangu kuwa uchumi na kipato cha wananchi kitainuka na hii hali ngumu ya maisha inaweza ikatukimbia. Lakini hayo yote lazima yanahitaji ipatikane taaluma ya kutosha, mabwana shamba wa maofisini tuwaache ni lazima mabwana shamba wapite katika maeneo ya mashamba na sio kubakika katika maofisi. Mhe. Spika, yakiwezekana hayo ni imani yangu kwamba tunaweza tukazalisha chakula chetu na pia tukapata hakiba na hatimae tukaweza kuuza.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika sekta ya uvuvi sekta ambayo mara nyingi inakwenda sambamba na sekta ya kilimo. Mhe. Spika, nimwambie Mhe. Makamo nimefurahi sana kusikia kuwa kuna ufugaji wa samaki na yeye tayari ameshawatayarisha vijana. Hili nasema nampa hongera sana.

Mhe. Spika, kwa kweli tuna bahari lakini wavuvi wetu bado hawajawezeshwa ipasavyo na hata wakati mwengine huwa wanavua mavuvi makubwa na kupata tija na samaki wengi. Lakini kinachosikitisha ni soko hawana pa kuwapeleka wala pa kuwauza, inaishia kuliwa tu na pato la mvuvi linakuwa duni na hafifu sana na wakati mwengine hushindwa hata kurudi baharini kuweza kuendelea tena na mavuvi kwa vile petroli imepanda na huku bei hakuna. Kwa hivyo, jambo hili linawasababishia wavuvi wetu hawa kuweza kuvunjika moyo na kubadilisha mfumo wa shughuli yao ya kazi. Hivyo ningemuomba mheshimiwa ili tuweze kukwamuka kiuchumi kikweli kweli na kuweza kuwaletea tija

wananchi wetu na kuweza kuwaondolea umasikini kwa kina kupitia sekta hii ya uvuvi, basi itiliwe maanani zaidi ufugaji wa samaki na pia kuwe na viwanda vya usindikaji kwa ajili ya usafirishaji.

Mhe. Spika, pia nimeona katika kitabu hiki cha hotuba kinasema kwamba kinatilia maanani namna ya afya na kusema kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja anataka kuifanya hospitali ya rufaa. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nasema huu ndio wakati tosha wa kufanya mageuzi mazuri sana katika sekta ya afya. Hii ni sekta ambayo inategemewa sana na Wazanzibari wengi walio katika kipato cha chini kwani hawamudu afya na pia jengo hili la Hospitali ya Mnazi Mmoja limekuwa halikidhi haja kwa wakati huu.

Mhe. Spika, umefika wakati kuwa naamini kwa juhudi na maarifa yako unamudu sana jambo hili kwani wewe ni mtembezi unatoka nje katika mataifa tofauti, lakini unapofika huko huendi kufanya mazungumzo ya lele mama, unakwenda huko na kuibua mambo ya msingi kwa ajili ya maslahi ya Wazanzibari. Mhe. Spika, naomba utekelezaji huu uende sambamba.

Mhe. Spika, pia umesema kwamba unataka kupandisha daraja Hospitali ya Kivunge na Makunduchi kwa Unguja, Micheweni, Vitongoji, Wete na Abdalla Mzee kwa Pemba. Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa hali iliyo katika hospitali hizi ambazo unataka kuzipandisha daraja ni mbaya sana. Mhe. Spika, mimi binafsi yangu leo nina siku ya tatu tu nimetoka katika Hospitali ya Kivunge, hali niliyoikuta huko ni ya ajabu sana, nimekuta madaktari hawapo, nimekuta watoto wamelazwa na vigodoro chini bila ya kuonekana daktari, kichumba chenyewe ni kidogo mno, hali ya uchafu ambayo haihitaji hata fedha basi niliona ajabu hata fyagio nalo hakuna. Mhe. Spika, nimeelewa wazi kwamba na usimamizi nao unachangia kwa asilimia 90 baadhi ya mambo yetu kutokutekelezeka.

Mhe. Spika, hivyo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais una kazi kubwa na ngumu kwa kuyatekeleza haya majukumu ambayo umeyapanga kuyatekeleza katika kipindi hiki. Mhe. Spika, watendaji wa serikali, mawizara na maidara yako wamekuwa wamelaa kushindwa kujiongoza na kuacha maadili ya kazi. Wamekuwa ni watu wa maajabu kila mmoja anasera na utaratibu wake wa kuingia katika ofisi za serikali. Mhe. Spika, huduma zote zinapatikana katika misingi ya tabu sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Balozi afanye mageuzi yako yakiwa kwenye kilimo na uvuvi, lakini hata katika sekta za serikali ili tupate watendaji ambao wana wajali wananchi wao.

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo pia ningemuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aende moja kwa moja kwenye uwajibikaji. Mhe. Spika, Wazanzibari

kuwajibika hatutaki, Wazanzibari tumekuwa wavivu, Wazanzibari hatuna dhamira ya kujitendea mambo mazuri bila ya sisi wenyewe hakuna mtu mwengine atakayetufanyia. Mhe. Spika, kuna mambo mengine ni watu kupewa madaraka au kazi ambazo hawana taaluma nazo, hii inachangia kwa asilimia 90 kushuka kwa pato la nchi, kushuka kwa maendeleo ya taifa. Mhe. Spika, umefika wakati sasa wanaopewa wizara na maidara wawe na uwezo wa kuzimudu kazi hizo.

Mhe. Spika, kama tunataka tubadilike kweli basi tumefika mahala lazima anayeajiriwa awe na sifa ile ambayo inamuingiza katika hiyo sehemu anayopewa. Lakini leo wanaajiriwa watu ambao uwezo hawana wa kufanya hizo shughuli, na ndio maana asiyejua hajui kufanya anapewa shughuli ambayo hana ujuzi nayo, hana taaluma nayo na hana ubunifu nayo. Mhe. Spika, siku zote unalikuta linatangazwa jambo linasemwa na viongozi wakuu wanalisema kwa nguvu na imani juu ya raia zao lakini halitekelezeki kwa sababu wanaopewa majukumu hawana uwezo wa kuyatekeleza hayo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa niaba ya wanawake wenzangu nasema umefika wakati serikali iwajibike na wananchi wawajibike kwa ajili ya taifa lao ili kwa ajili ya maslahi ya taifa letu. Mhe. Spika, hapa ndio petu sisi hatuna pengine sisi ndio Wazanzibari na viongozi tuliowachagua ni Wazanzibari hivi kwa nini hatuna ari ya kuindesha nchi yetu tuna nafasi ya kusifu mataifa mengine tu. Mhe. Spika, umefika wakati wa kubadilika, viongozi na watendaji wa serikali tufanye huruma na tuoneane vibaya na tuone kwamba tunafanya dhambi pale ambapo mtu hawajibiki jambo ambalo analiweza.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niseme kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia. Kwanza nimpongeze Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba yake ya aliyoitoa leo ili tuweze kuichangia sisi wawakilishi.

Mhe. Spika, mimi naanza kuhusu mgogoro wa ardhi, mgogoro wa ardhi umeendelea sana katika nchi yetu na wala hauleti tija kwa wananchi wetu hasa waliokuwa masikini wenye kunyanganywa maeneo yao ya ardhi. Mhe. Spika, mimi namuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais suala hili aliangalie kwa makini sana.

Mhe. Spika, vile vile namuomba Mhe. Makamo nguvu zake alizoziacha mwanzo kwa kushughulikia mgogoro wa ardhi aendelee wala asisite hata kidogo. Mimi nasema hayo kwa sababu migogoro ya ardhi kule kwetu imeenea

sana hasa kwa wale wenye kujenga mahoteli yanayowekeza. Jambo hili mimi nilikuwa namuomba Mhe. Makamo alishughulikie hasa katika Jimbo la Matemwe kwani kuna migogoro mingi inayosababishwa na wawekezaji pamoja na ugomvi mwingi na wana kijiji.

Mhe. Spika, katika shehia ya Pwani Mchangani kuna mgogoro wa ardhi baina ya muekezaji na wana kijiji cha Pwani Mchangani. Suala hili linataka kufuatiliwa na mheshimiwa ili ahakikishe wananchi wa Pwani Mchangani eneo lile wanalipata wenyewe ili wapate kupita vizuri katika njia yao na wasipate kuzunguka wanapokwenda safari zao. Mhe. Spika, jambo hilo likiwekwa sawa basi watu wa Pwani Mchangani hawatoweza kujichukulia hatua wenyewe.

Mhe. Spika, mimi ningemuomba jambo hili Mhe. Makamo alishughulikie kwani watu wa Pwani Mchangani ni wakaidi sana, nadhani hapo nyuma imewahi kutokea kesi wamezipeleka kunakohusika hivyo wamedharauliwa basi wamechukua hatua wao wenyewe. Kwa hivyo, mimi nasema kabla hili halijaleta madhara ya aina yoyote kwa wananchi wale kutokana na eneo lile na pamoja na yule muekezaji aende akawasilikilize wana Shehia ya Pwani Mchangani pamoja na muekezaji yule ili abomowe ukuta wake watu wa Pwani Mchangani wapate kupita njia ile.

Mhe. Spika, sasa nije kuhusu ukimwi, kweli ukimwi upo lakini sisi wenyewe serikali ndio tunaouchangia ukimwi. Mhe. Spika, kwa nini yawepo magesti na magesti haya yanachangia kueneza kwa ukimwi. Mimi naomba Wazanzibari tubadilike naamini sote ni waislamu hivyo serikali ichukue juhudi ya kuyaondoa magesti hayo ili watu waondokane na maambukizi ya ukimwi.

Mhe. Spika, pia nije kwenye utalii tukiangalia kwa kina kabisa ni kwamba utalii una faida yake na una hasara yake. Lakini tukitizama upande mmoja tuhakikishe tutakula hasara, hivyo lazima tuangalie na upande mwengine. Mhe. Spika, utalii kweli unatuletea tija katika nchi yetu lakini pia utalii unatutilia hasara kwa vijana wetu. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais awaekee sheria maalum wale watalii wetu ambao wanaotembea katika vijiji vyetu kwa sababu wanatembea wako uchi, vichupi vitupu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, wawekezaji wa mahoteli huwa wanawanyanyasa sana wakulima wa mwani, hapa kidogo nimepatwa na wasi wasi sijui ni sheria kuuzwa kule baharini au vipi mimi hapa sijaelewa. Mhe. Spika, kwanza hapa mimi nataka akija mheshimiwa aniweke sawa kwa sababu yakishajengwa yale mahoteli wakulima wa mwani eneo lile wanaondolewa na huku sisi tunasema watu wajiajiri wenyewe, na wanawake kwa kule kwetu kujiajiri kwao ni kilimo cha mwani. Kwa hivyo, muekezaji yule akishajenga hoteli yake katika eneo hilo

huwa anawafukuza wakulima wa mwani. Je, kweli wakulima wetu wataondoka na umasikini au wananchi wetu wataondoka na umasikini kwa hali hii?

Mhe. Spika, Kwa hivyo, namuomba Mhe. Makamo aweke sheria maalum kwa kuwa wawekezaji wale huuziwa sehemu ya nchi kavu, basi sehemu ya baharini wawe hawana ruhusa ya kuingia ili wananchi wetu waendelee kulima kilimo chao cha mwani. Mhe. Spika, mimi naiunga hoja hii mkono kwa niaba ya wanawake wa Kaskazini "A" asilimia mia kwa mia, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana angalau na mimi kunipatia fursa hii kuweza kueleza chochote juu ya hoja iliyopo mbele yetu. Mhe. Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimae kutupa nguvu na uwezo pamoja na maarifa ya kuweza kuichangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwa hili Mhe. Spika, nasema hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikuitumia fursa hii kukushukuru wewe uliyenipa nafasi ya kuweza kueleza machache kuhusu hoja iliyopo mbele yetu, pamoja na kwamba watu wengi wameshachangia mambo na mimi nitatia nyalio nyalio tu kidogo.

Mhe. Spika, niitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kuwa Makamo wa Pili wa Rais. Kwa kweli ni miongoni mwa kiongozi mahiri na makini katika nchi yetu, anatuonesha utumishi ulio makini, mahiri na wenye kutukuka. Kwa hivyo, mimi nasema ahsante sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, katika hoja iliyopo mbele yetu moja kwa moja mimi niende kwenye mambo haya ya Muungano. Katika ukurasa wa 7 mpaka wa 12 Mhe. Balozi amezungumzia kuhusu Muungano sana kuhusu kero pamoja na mabadiliko ya katiba. Mimi nataka niweke kitu cha tatu yaani ile sura ya Muungano wenyewe.

Mhe. Spika, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni miongoni mwa Muungano iliyofanyika katika ulimwengu huu, kwa kweli Muungano wetu ni mzuri kwa sababu umedumu mpaka leo hii tunao. Lakini naomba sasa nieleze mapungufu kidogo yaliyomo katika Muungano wetu.

Mhe. Spika, kabla ya kueleza mapungufu hayo niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kupanua demokrasi. Mhe. Spika, kwa sababu kipindi kile tulipokuwa na *Presidential decree* ukisema tu kuhusu

Muungano siku ya pili hajuulikani ulipo, kwa sasa tunakosoa na tunaelekeza. Mhe. Spika, kwa hili nashukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar kwa kweli una mapungufu yafuatayo. Kwanza Muungano huu umekosa *democratic legitimacy* kwa sababu sisemi kwamba hawakuwa na *democratic main dent* yakuunganisha kwa wakati ule. Lakini kwa wakati tulionao sasa hivi tunazungumzia demokrasia na utawala bora kuendelea kukaa na Muungano wa 1964 wa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na Marehemu Julius Kambarage Nyerere, kwa kweli inakuwa ni kwenda kinyume na utawala bora pamoja na demokrasia.

Mhe. Spika, katika Muungano ule viongozi wawili hawa waliunganisha nchi hizi na wakaweka *articles of union* na *articles of union* hizi zilihitajika kuwa *ratified* na kwa upande wa Tanzania Bara hizi *articles of union* zilikuwa *ratified*, lakini hakuna maandishi yoyote hadi leo hii. Mhe. Spika, tumejaribu kuangalia vitabu kadhaa, tumejaribu kuwauliza wanasheria kadhaa lakini *articles of union* kwa upande wa Zanzibar haikuwa *ratified*. Kwa hivyo, tunasema kwamba umekosekana ule uhalali wa kisheria.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika hili basi mimi sisemi kwamba Muungano huu ni mbaya au ni mzuri lakini kwa sababu yakuwepo kwa hili suala la utawala bora, demokrasi pamoja na utawala wa Katiba na Sheria ni vyema sasa Muungano tukauangalia kwa sura na kuujadili na kuwauliza watu wanataka Muungano wa aina gani.

Mhe. Spika, wakati nchi hizi zinaungana nadhani sisi Wazanzibari kama tulibatishwa katika ndoa ya mkeka, kwani kila tutakapokwenda umuage mume na mambo mengine tunapangiwa na mengine hatupewi. Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima nitamtaka Balozi baadae anijibu tangu tuungane mwaka 1964 kuna asasi nyeti kama vile za Mkuu wa Majeshi, *AGP* pamoja na Mkuu wa Usalama wa Taifa kawahi kutoka Zanzibar? Mhe. Spika, hii ni double standard mimi naamini kwamba kuna watu makini na walikuwepo watu makini akina Brg. Yussuf Himidi walikuwa wanaweza kuwa ma-*CDF* kwa nini hawakuwa? Mhe. Spika, nadhani hii ni double standard na kwa sura hii nadhani hatutendewi haki Wazanzibari.

Mhe. Spika, mimi naamini humu kwa ninavyoona hawa *backbenchers* wa humu wanaweza kuwa Mkuu wa Usalama wa Taifa wa Tanzania nzima akina Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi naamini anaweza kuifanya kazi hii vizuri. Lakini kila kukicha wanatupeleka Bara mimi nakuhakikishia mheshimiwa

katika hili hatuko radhi na sasa umeshafika wakati wakuulizwa kama Muungano huu mnaendelea kuutaka au hatuutaki.

Mhe. Spika, sisi hapa tulitaka kuingia katika *OIC* tukaambiwa hapana, na sasa tumepelekwa katika *East African Community* kama tumebebwa mgongoni, sisi sio watoto wachanga ni watu wazima tena tunajiweza na tuna uwezo na wataalamu tunao nikiangalia huko mbele safu iliyopo inaweza ikatuwakilisha katika *East African Community* kama nchi. Mhe. Spika, mimi nasema Zanzibar sasa ni nchi kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanywa Zanzibar ni nchi na hatuwezi kuingia katika *East African Community* tukiwa tumebebwa mg ongoni mwa Tanganyika tuingie kama Zanzibar, kinyume na hivyo itakuwa tunasababisha matatizo tena.

Mhe. Spika, nimalizie hapo sasa niende katika ukurasa wa 13 hapa Mhe. Balozi ameeleza kuhusiana na mambo ya kuimarisha kilimo na uvuvi. Mhe. Spika, mimi natokea katika Kijiji cha Vitongoji ni *far Eastern bay* ya Kisiwa cha Pemba, sisi kazi yetu kule ni kulima tungule, tunalima tungule na hulazimika kuuza katika soko la Chake Chake tungule zetu. Sasa Mhe. Spika, huwa tunapata tatizo moja, kwamba tungule wakati wa mwanzo wa mazao bei inakuwa nzuri, lakini baada ya mazao kushamiri inabidi debe zima la tungule tunauza kwa shilingi mia tano, ile ndoo nzima kubwa ya plastiki. Kwa hivyo, kilimo kile hakitusaidii, hakitusaidii kwa sababu sisi wenyewe kama wakulima hatuna *marketing board* ya kuweza ku-*stabilize* bei ya lile zao.

Sasa Mhe. Spika, namuomba Mhe. Makamo wa Pili hapa atueleze, atawezaje sisi wakulima wa tungule kule Vitongoji kuweza kuuza tungule zetu kwa bei nzuri tangu mwanzo wa mazao mpaka mwisho wa ule msimu wa zao kumalizika.

Mhe. Spika, kesi hii hii ni katika upande wa uvuvi. Katika uvuvi nako kuna tatizo, uvuvi uliopo pamoja na kilimo kuwa unachangia mapato ya nchi, lakini hakitusaidii sisi wavuvi. Kwa mfano, sehemu za kwetu kule Wesha ni wavuvi sana wa madagaa, siku za mwezi wa giza huwa tunavua madagaa mengi, lakini hatuna pa kuyauza kwa sababu ndoo nzima ya dagaa nayo tunaiuza kwa shilingi elfu moja. sasa huu MKUZA jamani unatsaidia nini sisi watu wa kule? Huu MKUZA unatusaidia nini sisi wavuvi wa madagaa Wesha na wakulima wa tungule kule Vitongoji?

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nadhani wakati umefika sasa wa kufanya kilimo cha kitaalamu, serikali lazima itusaidie kwa kutuwekea *marketing boards* ndani ya visiwa hivi kuweza ku-*stabilize* hizi *agricutural* price kinyume na hivyo tutakuwa masikini milele. nadhani ni kitu rahisi tu, badala ya watu

kuwahamasisha kujenga mahoteli makubwa makubwa hapa wakenda na vishuka ni kuwahamasisha wakaja wakatuwekea hizo *processing industry*, (viwanda vya kusindikia mazao yetu). Naamini serikali itakuwa imetufanyia vyema sana, sasa muelekeze nguvu zenu kwenye kilimo sio kwenye utalii tu. Hilo ni jengine Mhe. Spika.

Sasa niende katika ukurasa wa 29 hapa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais amezungumzia sana jinsi ya watoto wetu na wanawake wanavyodhalilishwa kijinsia. Inasikitisha sana, maana yake sio kudhalilisha kijinsia tu, mpaka utumikishwaji, watoto wanatumikishwa katika kazi za nguvu, pamoja na serikali kujitahidi sana lakini bado inaonekana kwamba iongeze nguvu zake katika kuwaondosha watoto kwenye madhila ya utumikishwaji. Kama utakwenda katika Bandari ya Wesha basi wanaopara samaki ni watoto wadogo, kama utakwenda Micheweni kwa Mhe. Subeti Khamis Faki watoto wadogo wanavunja kokoto vidole kucha zimetoka ni tatizo, kama utakwenda kwetu sehemu za uwandani watoto wanabeba matofali kupeleka katika magari. Nadhani umasikini umekuwa mkubwa sana na Mhe. Makamo tunaomba utumie uzoefu wako ulionao katika mambo ya kuendesha serikali, uzoefu wako ulionao katika mambo ya mlahaka na nchi za nje, uangalie wenzetu wanafanyaje kuwanusuru watoto katika kutumikishwa.

Sasa katika udhalilishwaji inasikitisha sana, naanza na watoto halafu nitakuja kwa watu wazima wanawake. Watoto Mhe. Spika, kama ukenda kule Jela kule. Jana liliulizwa swali na Mhe. Jaku Hashim kuhisu jela kuwa hakuna gereza. Mimi ni mzoefu Mhe. Spika, katika mambo ya jela, kila ukija uchaguzi mimi lazima niende jela ni mzoefu sana, isipokuwa mara hii napenda sana niishukuru serikali hii ya Umoja wa Kitaifa uchaguzi umemalizika salama usalimini na mimi sikwenda jela nashukuru sana, nampongeza Mhe. Balozi Seif Iddi kwa hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mhe. Spika, jela kuna tatizo, watoto wakienda jela ni tatizo kwa sababu wanalazimika kukaa vyumba vya wakubwa na wanatumia mtondoo katika kujisaidia mbele ya watu wazima na bangi kule inaliwa. Mtoto anakwenda kujisaidia kwenye mtondoo hapo hapo anafanywa vibaya, jamani ni tatizo hili. Mimi nashauri kitu kimoja serikali, waweke vyoo kabla ya kujenga hizo jela za watoto ili watoto waende wakajisaidie kwenye vyoo watoto wananajisiwa vibaya mule.

Sasa nije kwa watu wazima jinsi ya kudhalilishwa kijinsia kwa watu wazima wanawake. Mhe. Spika, kuna mwanafalsafa mmoja anaitwa Shaban Robbat naomba ninukuu maneno yake alisema, “Msiba wa kujitakia hauna matanga

wala kilio". Mhe. Spika, mavazi yanayovaliwa na watu wazima wanawake inasikitisha sana, yanapelekea mambo hayo wakati mwengine.

Mimi nadhani Marehemu Mzee Abeid Amani Karume Mwenyezi Mungu amrehemu alikuwa makini katika kudhibiti hili, watalii walikuwa wakifika *air port* wanavishwa mashuka pale na ukivaa chupa kama ni raia unapigwa viboko, ukivaa buga yaani Mzee Karume alijitahidi sana. Kwa nini hatufuati mawazo ya Marehemu Baba wa Taifa hili kuwataka hawa kinamama wavae mavazi ya heshima, ukimwi utapungua sana. Kwa sababu anakupita mwanamke kvaa kisuruali kifupi Mhe. Spika, na wewe mtu ni mzima hujaumwa hivi utafanya nini? Nadhani Mhe. Balozi Seif Ali tusaidie katika hili angalau kwa kuletwa sheria hapa ya mambo ya mavazi, hii itasaidia sana kupunguza ukimwi. Ilikuwa niende kwenye Ukimwi lakini sitaki niende tena natoa rai tu, kwamba iletwe sheria itakayohusiana na mambo ya mavazi ili kujiepusha na mambo ya ukimwi.

Mhe. Spika, mimi kwa sababu point nyingi zimeshasemwa ila nilikuwa nadangadanga tu humu, kwa hivyo nimalizie kwa kusema kwamba Muungano uliopo ni tatizo, wananchi wanataka waulizwe. Lau kama Mhe. Balozi unatuachia sisi *back benchers* wiki mbili, nilisema juzi kama tunaachiwa serikali miezi mitatu tu sisi basi nakuhakikishia baada ya miezi hiyo wananchi watakuwa wameshaulizwa kwamba mnautaka Muungano au hawautaki na kama hawautaki basi unakatika hapo hapo.

Kwanza mimi niseme kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano haihitaji kufanyiwa marekebisho inatakiwa katiba mpya. Mhe. Spika, naomba radhi kidogo kwa sababu nilikuwa nataka kupandisha maneno juu, lakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano haihitaji marekebisho kwa sababu katiba ni mali ya wananchi, katiba iliyopo hii haikutokana na watu kwa sababu haikufuata ile *constitutional making process*, ndio tunapata kero za muungano. Katiba iliyopo ya mwaka 1977 ni Katiba ya Tanganyika tu ile, imeondoshwa Tanganyika imewekwa Tanzania pale, sasa hatukushirikishwa wananchi na katiba ni mkataba baina ya wale wanaoongozwa na wanaoongoza, katiba inatakiwa itoke katika mishipa ya walioko katika *grass root,* ndio utakuta milele na milele matatizo ya Muungano hayaishi kwa sababu wananchi hawakushirikishwa katika kutunga katiba yao Mhe. Spika.

Kidogo nimalizie kwa kueleza vipi katiba ya kisasa na ya demokrasia inatungwa. Mhe. Spika, katika utungaji wa katiba kwanza unatakiwa utoe timu ya wataalamu ili kuratibu maoni ya wananchi, wanaita *teem of intellectual,* sitaingia katika *different professions, then* hiyo timu ya wataalamu iitishe makongamano katika maeneo kadhaa kuchukua maoni ya wananchi ili

kutayarisha rasimu ya katiba ipite itayarishe *International Convention* katika nchi nzima ipite kuzungumza kuchukua maoni. Kisha kuna kitu kinaitwa Bunge la Kutunga Katiba sio kama lile liliopo, liweko bunge maalum la kutunga katiba, mawazo yale yapelekwe katika bunge hilo ile rasimu.

Baada ya mawazo yale kupelekwa katika Bunge likishapitisha bado haijawa katiba hata ikapita hiyo rasimu bado haijawa katiba, linalofuata ni kuitisha *referendum* ili wananchi kuikubali ile katiba. Katiba hiyo itakuwa haina mizozo milele, lakini sisi katiba ya mwaka 1977 nakumbuka Mwalimu Nyerere aliita Bunge la kutunga Katiba hakukufanywa lolote maneno alikaa nayo mwenyewe Mwalimu Nyerere wakayapeleka kwenye Bunge la kutunga katiba na alikuwa *bias*, naomba radhi kwa hili. Kwa sababu kule walikuweko watu waliobobea kwenye lile bunge. Tanganyika walikuweko akina Mzee Spika Marehemu, alikuwepo Mhe. Pius Msekwa, Dkt. Aron Chiduo wataalamu mbali mbali sisi huku alikuja akachukuliwa Mzee Pasiganda kule Pemba, unaona?

Mhe. Spika, nakusudia katiba hii ya 1977 liwe bunge la kutunga katiba, matakwa ya Wazanzibari hayakuwasilishwa vyema. Kwa sababu Tanganyika walitoka wataalamu kwenda kwenye lile bunge huku Zanzibar wamechukuliwa watu hata si wataalamu wana siasa tu kina mzee Pasiganda, Juma Mtori Marehemu pale Vitongoji, hao wanasimamia nini? Kwa hivyo, Mhe. Spika, *solution* ni kuppeleka *referendum* kwa wananchi waulizwe kwamba Muungano wanautaka au hawautaki. Naunga mkono hoja Mhe. Spika.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kidogo sitaki niseme sana kwa sababu naona maneno yashamalizwa. Kwanza Mhe. Spika, nakupongeza kwa kunipa hii nafasi, halafu nampongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba yake nzuri na kitabu alichotuletea kimemaliza mambo yote ndio ukaona watu wameshavimbiwa hapana ta la kusema.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja kabla sijaichangia. Kwanza nataka nianze na habarai. Mhe. Spika, katika hii mitambo sisi tuna tatizo sana katika Idara yetu ya Habari Maelezo. Sasa hivi wenzetu Pemba saa zote wanatupigia simu kuwa hawatuoni, vifaa hatuna, mitambo tunaitembelea kule wakati huo uliponiweka Ustawi wa Jamii mara nne tukienda tunaambiwa chombo kitafungwa kesho, kila siku tukienda tunaambiwa chombo kitafungwa kesho, tunasikia mtambo huu upo Uwanja wa Ndege Mhe. Spika, umeletwa na nani aliyekuwa hasaini tukaupata wenyewe ukafungwa? Tupewe mtambo wetu ufungwe idara isipate shida hii, hatuoni chochote Mheshimiwa Televisheni Zanzibar.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, nitakuja kidogo kwenye UKIMWI. Mhe. Spika, tuna matatizo sana ya Ukimwi kwa takwimu zinazotoka kila siku. Juzi zilipotoka takwimu niliumwa na kichwa, kwa sababu huko Chake Chake ndio kitomvu mimi nilikotoka kijiji kidogo cha Wawi, Mabaoni ndiko alikotoka mama yangu, baba yangu ndio katika Ole. Kwa hivyo, sisi ikitajwa takwimu tunaumia sana, haya mambo ya Ukimwi tutayadhibiti vipi? Tunamuomba Mhe. Makamo aweke mkakati maalum, kwa sababu utapotembea humo barabarani basi ndio kama hivyo watu wanavyosema, uwekwe mkakati wa sheria ya kivazi watu wanakwenda uchi, lakini mimi nasema na mambo mengine yanatuchangia.

Mhe. Spika, tunasafirishwa hapa, lakini tunakokwenda kokote hata haya macho unapigwa picha, ukitoka na kibiriti utajulikana umekichukua wewe, sisi petu ni utandawazi watu wanaingia kila siku watoto wetu wanaiga matendo ya wale watu wanayokuja nayo hapa. Sasa haya pia yanachangia kwa watoto wanawake na wanaume, kuweza kujizuia na tukaweza kuudhibiti ukimwi basi patafutwe mambo ya namna ya kuweza kuudhibiti, si hivyo Mhe. Makamo miaka kumi ijayo watu wote watakuwa wana virusi vya Ukimwi Mwenyezi Mungu labda atatunusuru sisi tuliokuwa 'madingi'.

Mhe. Spika, Ukimwi ni hatari kwa janga la taifa tunapoteza watoto wetu. Tukindoka hapo ni madawa ya kulevya ndio yanayochangia sana, pombe, tunaomba serikali ituone kuweza kudhibiti mambo ya vilabu na kupika ulevi pamoja na kuuza kukemewe, hapa labda tunaweza kunusurika. Watoto wadogo wanaingia ndani ya majanga ya kulewa.

Mimi nikitoka hapa nakwenda zangu Amani basi nitakopita kote watoto wote hakuna anayejijua, ile gari wakati mwengine tusimame tuwapishe wao wote wako utemba, lazima ijulikane jamani watoto wanatumalizikia.

Mhe. Spika, halafu nije katika wanawake kuwaimarisha kiuchumi. Mhe. Spika, ujasiriamali umetusaidia sana wanawake, tukija kwenye *TASAF II* mimi nilikuwa ni mjumbe, tumepewa vikundi vingi, lakini vikundi havina usimamizi. Tunavitembelea vikundi ukienda humjui katibu, mhasibu wala mshika fedha; ukimuuliza umefanya vikao vingapi kwa miezi mitatu hana jawabu, keshapewa shilingi milioni kumi hajui alivyozitumia, utakwenda pale watu wale wamekaa tu mwisho mabanda ya kuku yanauzwa na kuku wanauzwa, umasikini itakuwa unaturudia pale pale.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tunaomba tutakapopewa nyezo na wale wanaotupa wasituondokee kutupitia mara kwa mara katika vile vikundi, isiwe tena mtu keshapewa kikundi akaachiliwa ikawa ndio basi.

Mhe. Spika, mimi nafarajika sana kwa Mhe. Waziri alivyokipanga hiki kitabu, nitakuja huku nyuma kidogo kwa sababu sitaki nichangie sana nikaharibu kwa sababu watu washachangia na lile la kusema halipo, naona watu tumekuwa tunazungumza tu. Nirudi kidogo huku nyuma kwenye Muungano. Muungano Mhe. Spika, sisi tunauenzi na tunaenzi wale wazee wetu walioleta huu Muungano, lakini la kusikitisha Makamo wetu wa Kwanza awe ni Rais wa Zanzibar atakapokwenda apate ile hadhi ya umakamo. Leo sisi tunamchagua rais wetu lakini kule keshachaguliwa makamo, wewe akienda pale hatujui anakwenda kama nani. Tunaomba Mhe. Spika, Muungano wetu ni mzuri na hatuwezi kuuvunja, kwa sababu bila ya Muungano hatui, watoto wetu wote wamejenga Bara mimi siko tayari kura yangu kuseme Muungano usiwepo.

Watoto wote wako huko, wajukuu, dada zangu, bibi zangu wako kule, tukivunja muungano watakwenda wapi? Lakini tunataka utaratibu wa kuweza kutuweka pazuri katika Muungano, tunaomba rais wetu arudi awe ni Makamo wa Rais ndilo tunaloliomba. Katika hizo katiba wanasheria wetu watakaokwenda wairudishe hadhi ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar awe ndiye Makamo wa Rais na ndivyo matakwa yao walivyotaka hawa, sio kuwa tuuenzi lakini kule kuwe kuna makamo yeye tumemchagua hapa kuwa ni rais keshakuwa yeye kule ana makamo wake, lakini akienda kule hadhi yake hatujui ni ipi tutaambiwa tujue hadhi ya rais wetu akienda kule ni ipi katika Muungano.

Kwa sababu ni kumdhalilisha rais wetu atakapokwenda kule kukiwa kuna makamo yeye atakuwa anakwenda kama nani? Basi tunaomba nafasi yetu hii turudishiwe kama Wazanzibari.

Mhe. Spika, sina mengi niliyotaka kuchangia isipokuwa nikitaka niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa asilimia mia moja pamoja na wanawake wenzangu wote. Mwenyezi Mungu atujaalie tuipitishe na tuweze kufanikisha yaliyomo.

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Raya Suleiman kwa kuchangia kwa muda mfupi kabisa, kumbe ukipanga *point* vizuri unaweza kutumia muda mchache lakini ukasema mengi. Kwa maana hiyo basi, kwa mujibu wa idadi ambayo maombi ninayo inaelekea kesho kipindi cha asubuhi na hasa kwa kuwa ni siku ya Ijumaa. Basi niombe radhi sana Waheshimiwa Wajumbe tuje kutumia si zaidi ya dakika 15 ili tupate wajumbe angalau 12 kuweza kuchangia hoja hii na baadae jioni tumuombe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais baada ya kusaidiwa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wakati ambapo Waheshimiwa Mawaziri wengine ambao tayari maombi yapo wawe nao

wamemsaidia Mhe. Makamo wa Pili kwa mujibu wa yale mambo ambayo yanaangukia kwenye sekta zao.

Waheshimiwa Wajumbe labda Mhe. Salum Mtondoo nasikitika sana kwamba nilikwita mapema mno kwa sababu uliomba mapema lakini nilipokwita kwa bahati mbaya hukuwepo na nafasi ikachukuliwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Sasa kama muda utakuwepo Mwenyekiti kesho akiingia hapa nafikiri anaweza akatizama namna ya kukusaidia, lakini vyenginevyo nafasi uliipoteza. Kwa sababu uliomba mapema na nikafuata mtiririko lakini kwa bahati mbaya sana ikawa hupo.

Baada ya machache hayo basi Waheshimiwa Wajumbe naahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 24/06/2011 saa tatu za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 24/06/2011 saa 3:00 asubuhi)